**18 MEI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

__________

# MAJADILIANO YA BUNGE

___________

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 18 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 362

### Vijana wa Mtwara kunufaika na programu za kukuza ujuzi

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, kwa kiasi gani vijana wa Mtwara wamenufaika na programu ya kukuza ujuzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum Mtwara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mtwara jumla ya vijana 1,663 wamenufaika kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi. Kati ya vijana hao, 891 wamenufaika kupitia mafunzo ya uanagenzi katika fani za uashi, uchomeleaji, ufundi bomba, ufundi magari, ufundi rangi, umeme wa majumbani, umeme wa magari, upishi, useremala, na ushonaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, vijana 772 wamenufaika na Mpango wa Urasimishaji Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na kupewa vyeti katika fani za useremala, uashi, ufundi magari, uungaji na uchomeleaji vyuma, ufundi umeme, ubunifu wa mavazi na teknolojia ya nguo, uandaaji na upishi wa vyakula, utandazaji na ufungaji mabomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza: -

Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini kwa vijana hao ambao wamepatiwa mafunzo ya uanagenzi katika Mkoa wa Mtwara na nchi nzima ili kuona kama hiyo programu ina tija?

Swali la pili, hao vijana ambao hawajapatiwa vyeti kwa maana ya kutambuliwa ama kurasimishwa, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba vijana hao wamepatiwa vyeti na kutambulika katika elimu isiyo na mfumo rasmi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kufanya tathmini na siyo kwa Mkoa wa Mtwara pekee, ni nchi nzima kwa sababu sera hii ni kwa ajili ya wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, kwa kipengele cha pili, wale ambao wamekidhi vigezo vya kupatiwa vyeti, utaratibu utafwatwa na watapatiwa vyeti vyao. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 363

**Kupandisha hadhi shule za sekondari – Buyungu**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, lini shule za sekondari Nyamtukuza, Muhange, Shuhudia, Kasanda na Gwanumpu zitakuwa za kidato cha tano na kidato cha sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Muhange imekaguliwa na wadhibiti ubora wa shule ikaonekana ina mapungufu ya mabweni mawili, mapungufu hayo yakikamilishwa itapandishwa hadhi ya kuwa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, Shule za Nyamtukuza, Shuhidia, Kasanda na Gwanumpu zinaendelea kuongezewa miundombinu ya majengo, ikikamilika zitakaguliwa na wadhibiti ubora wa shule na kuombewa kupandishwa kuwa za Kidato cha Tano na Sita. Hata hivyo, shule moja mpya ya kidato cha tano na sita imesajiliwa ambayo inaitwa Amani Mtendeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza maswali naomba niweke kumbukumbu sawa ni Shule ya Sekondari Gwanumpu na Shule

ya Sekondari Shuhudia. Baada ya masahihisho hayo ninashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kakonko inayo shule moja tu ya sekondari ambayo ni Shule ya Sekondari Kakonko, na katika majibu ya Serikali amebainisha kwamba Shule ya Sekondari Muhange inapungukiwa mabweni mawili tu.

Je, lini sasa Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga hayo mabweni mawili ili masomo yaweze kuanza pale?

Swali la pili, amebainisha shule hizi za Sekondari Shuhudia, Kasanda, Nyamtukuza na Gwanumpu zinapungukiwa miundombinu mbalimbali, lakini kinachohitajika hapo ni fedha. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miundombinu hii inayopungua inakamilika na masomo yaweze kuanza katika shule hizi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la kwanza la lini fedha itakwenda kukamilisha mabweni haya ambayo tayari yameshaanza kujengwa. Serikali itapeleka fedha kadiri ya upatikanaji wake na tutaangalia katika bajeti hii iliyopitishwa ya mwaka wa fedha 2023/24 kuona kama hiyo shule imetengwa fedha, kama haijatengewa tutajitahidi tuitengee fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili kuhusu Shule za Gwanumpu, Shuhudia na Nyamtukuza ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, tutaangalia vilevile kuona uwezekano wa kuzitengea fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

Na. 364

**Kutangaza Mji wa Bagamoyo kuwa Halmashauri**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE K.n.y. MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatangaza Mamlaka ya Mji Mdogo Bagamoyo kuwa Halmashauri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipokea mapendekezo ya kupandishwa hadhi ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo kuwa Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya tathmini ya kina imebainika kuwa, Halmashauri hii bado ina upungufu wa miundombinu mbalimbali yakiwemo majengo ya utawala na huduma za kijamii na mapato yasiyotosheleza kuipandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo kuwa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali kwa sasa ni kuboresha miundombinu katika maeneo ya utawala yaliyopo na siyo kuanzisha maeneo mapya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Sensa ya Watu na Makazi iliyokuwa imefanyika hivi karibuni, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuweza kutoa tamko kwamba irudi tu katika mfumo ule wa zamani wa vijiji kuliko hivi sasa kuweza kusubiri kwa sababu imekuwa ni muda mrefu, tangu mwaka 2009?

Swali la pili, pale kwenye Jimbo la Kibiti, Kata za Kibiti, Dimani na Mtawanya ilitangazwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo tangu mwaka 2014, shughuli za maendeleo, vikao vya kisheria, mali zimekuwa haziwezi kumilikiwa ipasavyo.

Je, Serikali ina tamko gani kuhusiana na suala hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la kwanza la tamko la kurudisha kuwa na vijiji badala ya Mamlaka ya Mji Mdogo. Nirejee kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba vigezo vya kupandisha Mamlaka za Mji Mdogo kuwa Halmashauri za Mji zimewekwa wazi kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa na Mamlaka nyingi za Miji Midogo hizi bado hazijakidhi vigezo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna Mamlaka za Miji Midogo asilimia 67 ambazo haziwezi kufikia malengo yao wanayojiwekea ya kibajeti na ni asilimia 33 tu ambazo zinafikia malengo yao ya kibajeti kwa asilimia 100, ikiwemo Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo. Serikali itaendelea kuliangalia hili na pale tutakapokuwa tumeboresha miundombinu katika maeneo ya kimamlaka yaliyopo sasa tutaendelea kufanya *review* na kuona ni namna gani tunakwenda kuzipandisha hadhi mamlaka hizi.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la Kibiti. Vivyo hivyo kama nilivyotoa majibu yangu kwenye swali la nyongeza namba moja, kwamba tunaangalia vigezo vya mapato vilevile na kuweza kufanya huduma mbalimbali za kijamii, wao wenyewe kupitia mapato yao ya ndani. Mji Mdogo wa Kibiti tutafanya tathmini kama unakidhi vigezo vile vya kimapato basi tutaona ni namna gani ambavyo unaweza kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo katika Mji wa Kibiti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 365

**Bajeti ya *TARURA* kwa ajili ya ukarabati wa barabara Kyerwa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, kiasi gani cha bajeti kimetengwa *TARURA* miaka mitatu mfululizo kwa ajili ya ukarabati wa barabara Kyerwa na upi ufanisi wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka wa fedha wa 2020/2021 hadi 2022/2023, Wilaya ya Kyerwa imetengewa jumla ya shilingi bilioni 7.34, ambapo mwaka 2020/2021 shilingi bilioni 1.26 zilitengewa, mwaka 2021/2022 shilingi bilioni 2.89 na shilingi bilioni 3.18 zimetengwa katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ufanisi uliopatikana ni kuwa, barabara zenye kiwango cha changarawe zimeongezeka kutoka kilomita 185.46 hadi kilometa 261.71 na barabara za udongo kupungua kutoka kilomita 711.96 hadi kilometa 634.81 na makalvati 95 yamejengwa, ikiwa ni pamoja na barabara za lami zenye urefu wa kilometa 4.2 katika Makao Makuu ya Wilaya na Mji Mdogo wa Biashara wa Nkwenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mpaka sasa barabara za vumbi ni zaidi ya asilimia 70 na barabara ya lami ikiwa ni asilimia 0.4 na changarawe asilimia 29.

Swali la kwanza, ni kwa nini bajeti imeendelea kuwa kidogo, ambayo ni shilingi bilioni tatu, wakati barabara za vumbi na za udongo bado ni zaidi ya asilimia 70?

Swali la pili, ni lini itatengenezwa barabara ya kutoka Kyerwa kwenda *STAMICO* ambako kuna biashara kubwa ya madini ya bati, ni lini barabara itatengenezwa, sambamba na kuunganisha Kata ya Mabira na Kata ya Kibale?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoa maelezo katika majibu yangu ya msingi, bajeti imeendelea kuongezeka ndani ya miaka hii mitatu. Ukiangalia *trend* mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti katika Wilaya ya Kyerwa ilikuwa shilingi bilioni 1.26 tu, lakini hivi tunavyozungumza bajeti hiyo imekwenda mpaka shilingi bilioni 3.18 kwa maana imeongezeka mara mbili ya vile ilivyokuwa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, hiyo inaonesha dhamira ya dhati ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuiboreshea nchi yetu barabara zake za vijijini na mijini kupitia Wakala wa Barabara *(TARURA)*. Kwa hiyo, nikutoea mashaka Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kuweka fedha kuangalia ni namna gani barabara hizi zinatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la barabara hii ya Kyerwa – *STAMICO* kupitia Kata ya Mabira na kadhalika, tayari katika kiwango cha lami tulianza kwa kujenga kilometa mbili kwenye Mji Mdogo wa Nkwenda, kuna barabara ambayo ipo kutoka Kido Hospitali katika Mji wa Kyerwa, vilevile tutakwenda sasa kuangalia hii kwenye bajeti zijazo tuweze kutenga fedha kwa ajili ya barabara hii ya Kyerwa mpaka *STAMICO.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza

niipongeze Serikali kuendelea kuongeza bajeti kwenye barabara za *TARURA* Wilayani Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kasoni kwenye Kata ya Nyakatuntu kwenda mpaka Mkuyu Kata ya Kikukuru niliiombea fedha na fedha imeshapatikana.

Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha changarawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Kasoni – Nyakatuntu – Mkuyu kwa maana imetengewa fedha kwenye bajeti hii ambayo tunaanza kuitekeleza tarehe 1 Julai mwaka huu, tutahakikisha kwamba barabara hii inapatiwa mkandarasi haraka ili iweze kuanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza jitihada za Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Bilakwate, kwa maana amekuwa akiifuatilia sana barabara hii na kuhakikisha kwamba inatekelezwa kwa wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 366

**Upatikanaji wa fursa za kiuchumi zinazotokana na ushiriki wa Mikutano ya Kimataifa**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, kwa kiasi gani ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa unazingatia upatikanaji wa fursa za kiuchumi na utekelezaji wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa unalenga kupata na kutumia fursa za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kupata mitaji, uwekezaji, masoko ya bidhaa na huduma, kukuza utalii, miradi ya kisekta, mikopo ya masharti nafuu na misaada, kujengewa uwezo wa kitaalamu na upatikanaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa umewezesha Tanzania kupata masoko ya bidhaa mbalimbali, kama vile mbogamboga, matunda, korosho, nafaka, utalii, malumalu na bidhaa za kioo. Vilevile nchi yetu inanufaika kwa kupata wawekezaji katika sekta mbalimbali,

ikiwa ni pamoja na utalii, viwanda, kilimo, uvuvi, mifugo, madini na nishati anuwai.

Mheshimiwa Spika, kadhalika katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita, ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa umeiwezesha Tanzania kupata misaada mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha kutoka Shirika la Fedha Duniani kiasi cha shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya kukabiliana na janga la UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia kutenga kiasi cha dola za Marekani bilioni 2.1 (sawa na shilingi trilioni 4.8) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 na 2024/2025, na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo *(IFAD)* kutoa dola za Marekani milioni 58.5 kwa ajili ya miradi ya kilimo kwa mwaka 2021/2022. Aidha, kupitia ushiriki katika Mkutano wa 27 wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi *(COP 27),* Benki ya Dunia ilizipatia Nchi za Afrika ikiwemo Tanzania, kiasi cha dola za Marekani bilioni 18 kwa ajili ya miradi ya nishati jadidifu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na kwa kutambua jitihada kubwa ambazo anaweka Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuimarisha diplomasia ya kiuchumi, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Je, Serikali haioni ipo haja ya kufanya *mapping* katika nchi za nje ili kujua katika kila nchi tunataka kuwauzia nini na pia kujua kutoka kila nchi sisi tunataka kuwauzia nini ili tuweze kuimarisha ushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na sekta binafsi na pia

kuziwezesha balozi zetu za nje kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi pamoja na balozi za nje hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Wizara ya Mambo ya Nje iko tayari kuandaa mfumo ambao utaweza kufanya *tracking* ya utekelezaji wa mafanikio yaliyoainishwa yanayotokana na ziara ya viongozi wetu kimataifa, kwa sababu utekelezaji wake haufanywi moja kwa moja na Wizara hii ya mambo ya nje, bali unafanywa na Wizara nyingine pamoja na taasisi nyingine? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kusaidiana na sekta binafsi katika kufanya *mapping* ya fursa ambazo zipo katika nchi mbalimbali huko nje. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ya Mambo ya Nje inafanya kazi kwa karibu sana na sekta binafsi. Kwanza sekta binafsi pia hushiriki katika ziara za viongozi wetu mbalimbali huko nje, ambapo Wizara hizo huwafungulia milango na kujua fursa mbalimbali za uwekezaji. Pia kupitia mabalozi wetu wa nchi mbalimbali, tumekuwa tukiwaunganisha na sekta binafsi ili kujua fursa mbalimbali ambazo ziko huko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ufuatiliaji wa yatokanayo na safari za viongozi wetu, hili ni suala muhimu sana, nasi tuna wajibu sana wa kufuatilia kwamba ziara za viongozi wetu zinaleta matunda ipasavyo. Hivyo, uko mfumo maalum wa kuhakikisha kwamba sekta zote ambazo zinaguswa na ziara hizo tunakaa pamoja, tunafanya mkutano na kuainisha utekelezaji wake ili kujua changamoto na faida zake ili kupatiwa ufumbuzi ipasavyo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Thea Merdad Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 367

**Adhabu kali kwa wanaolawiti na kubaka watoto na wanawake**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta muswada wa sheria ya adhabu kali kwa wanaobaka na kulawiti watoto na wanawake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vifungu 130, 131, 131A na 154 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, ni makosa ya jinai kwa mtu kubaka na kulawiti. Makosa yote haya adhabu yake ya juu ni kifungo cha maisha jela, na adhabu ya chini ni kifungo cha miaka 30 jela. Aidha, kwa makosa yote hayo yakitendeka dhidi ya mtoto mwenye umri chini ya miaka 10, adhabu yake ni kifungo cha maisha jela.

Pamoja na adhabu hizo, Mahakama ina mamlaka ya kutoa amri ya ziada ya kumlipa fidia mwathirika chini ya kifungu cha 131(1) cha Kanuni za adhabu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali katika kutekeleza maelekezo ya Bunge, inafanya utafiti zaidi ili kuona kama kuna hitaji la kufanya maboresho au marekebisho ya sheria hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Merdad Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yanayoleta tumaini. Nami nashukuru mmesema kwamba mmechukua, mkalifanyie kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 368

**Kunufaika na vijana wanaopata mafunzo ya kilimo Israel**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, kwa kiasi gani Taifa linanufaika na vijana wanaopelekwa kwenye mafunzo ya kilimo Israel?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Israel zilikubaliana kushirikiana kwa kuanzisha programu ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaomaliza Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati vya Mafunzo ya Kilimo na Mifugo nchini Israel. Lengo la programu hiyo ni kuongeza ujuzi na maarifa juu ya teknolojia za kisasa.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2015 hadi sasa, jumla ya vijana 261 wa Kitanzania wamenufaika na mafunzo ya kilimo kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Israel *(Ministry of Foreign Affairs Israel's Agency for International Develeopment Cooperation)* kupitia *Agrostudies*.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza kuwatumia vijana waliohitimu mafunzo kwa vitendo nchini Israel kupitia programu ya *BBT* na *Block farm* ambapo wanapata fursa ya kuwashirikisha na vijana wengine uzoefu wao kutoka nchini Israel. Hadi sasa jumla ya vijana 79 walioshiriki mafunzo nchini Israel ni miongoni mwa vijana 812 walio kwenye mafunzo ya kilimo biashara katika Vituo Atamizi. Baada ya kipindi cha mafunzo, watapata fursa ya kufanya kilimo biashara kupitia mashamba ya pamoja ya *block farms* chini ya *BBT*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na majibu ya Serikali. Naomba kutumia nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali, kwa maana ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Wizara ya Mambo ya Nje kwa programu hii ya kuwajengea vijana uwezo na mafunzo ya ziada, na pia kuipongeza Serikali hususan Wizara ya Kilimo kwa kuwajumuisha hawa vijana 79 katika programu ya *BBT*. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Kwa kuwa vijana hawa tayari walishasoma vyuo vikuu na vyuo vya kati na wakapata ujuzi wa ziada huko Israel; je, Serikali kwa maana ya Wizara ya Kilimo iko tayari sasa pamoja na kuwahusisha kwenye *BBT* kuanzisha hiyo programu ya mashamba makubwa *(block farming);* na kwa kuwa tayari wenyewe ujuzi wanao; na tayari hawa 79 wanatumika kule lakini hawa waanze kabisa kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa sababu Serikali imetenga fedha nyingi na inajenga miradi mingi ya umwagiliaji ambayo bila shaka itahitaji wataalam katika kuiendesha katika kuwasaidia wakulima wetu; je, Serikali iko tayari kuwatumia baadhi ya vijana hawa kwa mfumo hata wa kuwalipa japo posho ya kujikimu ili wawasaidiwe wakulima wetu katika hii miradi mikubwa ambayo imetekelezeka hususan kule Mtura?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cosato Chumi kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza vijana wote ambao wanaenda Israel kwenye sekta ya kilimo mazao, wapo wengine ambao hawaendi kwenye sekta ya kilimo mazao; wengine wanaenda kwenye mifugo na maeneo ya namna hiyo. Kwa hiyo, wale ambao wako kwenye sekta ya kilimo mazao, tumeanza kuwa-*incorporate* kwenye programu ya *BBT* kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi. Wapo ambao tayari wanafanya shughuli za kilimo ambapo tumeanza kuwatambua sasa hivi, wanafanya shughuli za uzalishaji katika maeneo yao na tumewaingiza kwenye *component* ya pili ya programu ya *BBT* ya kuwapa *grants* na mikopo nafuu ya asilimia 4.5. Kwa hiyo, tumeshaanza kuwatambua na kuwaangalia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuwatumia kama *extensional officers,* nilitaka tu niliambie Bunge lako tukufu kwamba, kuanzia mwaka ujao wa fedha na tutakapoleta mabadiliko ya Sheria ya Umwagiliaji na Ugani hapa ndani ya Bunge lako, tunaangalia namna ya kuwatumia vijana waliopo mashuleni kwenye programu za *extension* ambao wanafundishwa katika vyuo vyetu vya kilimo. Vile vile vijana ambao wana utaalam wa kilimo ili kuanza kuanzisha kampuni binafsi za *extension services* kwa wakulima na waweze kutoa huduma za namna hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi. Naishukuru Serikali kwa majibu. Je, Serikali haioni kuwa sasa shule zetu za sekondari za kata zimekuwa na wanafunzi wengi wasiopata kuendelea na masomo ya juu na kwa hiyo, vijana hao wangekuwa sehemu moja ya kuwajengea uwezo wale wanafunzi walioko shuleni kwa kuanzisha mashamba madogo ya majaribio na mafunzo katika shule hizo katika kanda na wilaya zetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna mchakato unaendelea wa mapitio ya sera ya elimu, nami naishukuru Wizara ya Elimu kuweza kuchukua *component* ya *agriculture* kuwa sehemu ya mapitio haya ya sera. Mawazo kama haya tutaendelea kuyapokea na siwezi kutoa *commitment* sasa hivi kwamba tutaanza kuweka mashamba darasa katika kila sekondari, lakini ni wazo na ninashukuru, nasi kama Serikali tumelipokea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa mafanikio makubwa ya kilimo Israel ni yale ya *Kibbutz Farms* na vijana wa kitanzania waliofanikiwa nadhani hayo ndiyo pia wanaenda kujifunza: Je, Serikali iko tayari sasa kutumia vijana hao kuwarejesha katika maeneo yao ya vijijini kwa sababu Watanzania wengi na karibu wote ni wakulima wadogo wadogo ili wanufaike?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mama Shally Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi na maswali aliyouliza Mheshimiwa Cosato, namna ya kuwatumia vijana hawa ni lazima tuwe na mfumo wa ugharamiaji kwa sababu huwezi kutaraji kumpeleka kijana kijijini ukamwambie akatoe elimu bila kuwa na mfumo wa ugharamiaji.

Mheshimiwa Spika, tumepokea mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na wadau wengi wa sekta ya kilimo namna ya kuwatumia vijana walioenda Israel, walioenda nje lakini wapo vijana ambao wamesoma katika vyuo vyetu, wamesoma kilimo na wana utaalam wa kilimo cha kisasa, lakini bado wapo mtaani. Kwa hiyo, kama Wizara, tunapoenda kupitia mapitio ya sheria ambayo tutaileta ndani ya Bunge lako tukufu ya *Irrigation and Extension Services,* tuta-*incorporate component* ya vijana ambao wana elimu ya *extension* namna ambavyo watatumika na namna gani tutakuwa na mfumo mzuri wa ugharamiaji wa huduma zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Wilaya ya Kahama haijanufaika na mradi wa *BBT;* na kwa kuwa Halmashauri ya Msalala sasa tuko tayari kupokea mradi huu kwa vijana wetu: Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri utafika katika Halmashauri ya Msalala ili tuweze kuanzisha mradi huu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Iddi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara iko tayari kushirikiana na Halmashauri yoyote katika nchi yetu ambayo iko tayari kutenga eneo la kilimo kwa ajili ya mfumo wa *block farm* na kwa ajili ya mfumo wa *BBT*. Mfano mzuri ni Halmashauri ya Makete ambao wameamua kutenga *ten percent* yao kuwakopesha vijana, na sisi Wizara tukawapatia pembejeo kwa maana ya mbegu za bure kwa ajili ya kilimo cha ngano. Kwa hiyo, nihamasishe Waheshimiwa Wabunge ninyi ni wajumbe wa Baraza la Madiwani, ni wajumbe wa Kamati za Fedha tengeni maeneo na kuwa tayari kutenga sehemu ya asilimia kumi za Halmashauri kuwasaidia vijana katika maeneo yenu, na Wizara tuko tayari kuja ku-*support initiatives* za namna hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza. Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa nchi yetu imejaliwa wahitimu wengi wa vyuo vikuu kila kona wakiwemo kule Nachingwea. Je, Serikali inachukua vigezo gani kuwapeleka

hawa vijana wetu ambao wametapakaa nchi nzima huko Israel? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, cha kwanza hii programu inakuwa *coordinated* na Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje kwa kushirikiana na taasisi ya *Ministry Affairs* ya *Israel for International Development and Corporation*. Mara nyingi Serikali huwa inatoa *window* na huwa kuna utaratibu maalum ambao unatumika namna ya kuwapata vijana wanao-*apply* na kuweza kwenda kushiriki katika *windows* za namna hii.

Mheshimiwa Spika, tumekutana na ubalozi wa Israel hivi karibuni na kujadiliana nao namna ya kuboresha huduma ya kuwapata vijana, kwa sababu wapo vijana ambao wana *apply* kwa ajili ya kwenda kufanya jambo A, wakifika kule wanajikuta wamekuwa *committed* kufanya jambo lingine tofauti na kile ambacho walitarajia. Tumeongea na Ubalozi wa Israel, tunaendelea nao na mazungumzo tukishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje, badala ya kuwasafirisha hao vijana. Tunavyo vituo vingi katika nchi yetu. Ushirikiano ule wa utalaam tuweze kuutumia ndani ya nchi na waweze kuja kutusaidia ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

Na. 369

**Ujenzi wa barabara ya Mtwara Mjini - Msimbati kwa kiwango cha lami**

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayotoka Mtwara Mjini kuelekea Msimbati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara inayotoka Mtwara Mjini mpaka Msimbati ni barabara ya Mangamba – Madimba hadi Msimbati yenye urefu wa kilometa 35.63 inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii imekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii ya uchumi, ni nini hasa mkakati wa Serikali kuhakikisha inajenga barabara hii kwa haraka?

Swali langu la pili, Jimbo la Mtwara Mjini lina changamoto kubwa sana ya barabara; je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuliangalia jimbo hili kwa jicho la tatu ili iweze kulijengea barabara nyingi za lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua umuhimu wa barabara hii kama Serikali na ndiyo maana tumeshafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na tunahakikisha ya kwamba barabara hii inapitika kila mwaka. Katika mwaka wa fedha ujao imetengewa takribani shilingi milioni 188.435 na katika mwaka ujao pia tutafanya usanifu wa kina ili iwe maandalizi katika kujenga katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, barabara katika Mkoa wa Mtwara hususan Mtwara Vijijini na Mjini, Serikali inatambua umuhimu wa barabara kuboreshwa katika Mkoa huo. Ndiyo maana hivi sasa kuna miradi ile ya *EPC + Financing,* kuna barabara ambazo pia ziko katika Mkoa wa Mtwara na ambazo hivi karibuni tutaenda kusaini mkataba kabla ya mwezi wa sita mwaka huu, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Barabara ya Mbulu – Karatu – Haydom – Sibiti mliahidi kujenga kwa kiwango cha lami na kipande hiki cha Mbulu – Haydom, Mheshimiwa Waziri uliahidi utasaini mkataba kabla ya

bajeti yako Jumatatu. Hebu tuambie leo na uwambie wananchi wa Mbulu, mkataba huo utasaini lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia sana suala la barabara hii na wewe ni shahidi kwamba Mheshimiwa Mbunge, katika Bunge lililopita alipiga sarakasi kuhusiana na suala hili la barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Sikivu. Sasa, tunakwenda kusaini mkataba kesho na tutasaini pale Haydom. Kwa hiyo, niwatangazie wananchi wa jimbo hili kwamba kesho ni siku muhimu kwao katika kushuhudia kusainiwa mkataba wa ujenzi wa barabara hii. Hongera sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia barua hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Singida – Ilongero hadi Haydom upembuzi yakinifu umekwishafanyika; je, Serikali itakamlisha lini barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekwisha kamilika na sasa Serikali inatafiuta fedha ili tujenge kwa kiwango cha lami barabara hii, ahsante.

**SPIKA**: Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Kufuatia ujenzi wa bandari ya uvuvi unaoendelea pale Kilwa Masoko. Nini mpango wa Serikali kupanua barabara ya kutoka Kilwa Masoko mpaka Nangurukuru ili iweze kukidhi haja ya wakati wa sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli pale Kilwa Masoko tunajenga bandari ya kisasa ya uvuvi na katika mipango yetu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia *TANROADS,* tutaboresha pia barabara hii kutoka eneo la bandari ri kwenda katika eneo la pale mjini na kwa maana hiyo Mheshimiwa Mbunge katika mwaka wa fedha ujao barabara hii tumeitengea fedha kwa ajili ya kuboresha katika ujenzi wa kiwango cha lami. Ni sehemu ya mradi huu wa uijenzi wa hii Bandari ya Kilwa Masoko, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya kutoka Igawa kuelekea Mbeya inapita Jimbo la Makete. Ni barabara yenye *volume* kubwa ya magari na inachangia uchumi wa Tanzania kwa kiwango kikubwa sana. Je, ni ipi *commitment* ya Serikali ili iweze kujenga barabara hii ambayo pia anaitumia Mheshimiwa Spika na imekuwa ni nyembamba kwa kiwango ambacho inahatarisha sana usalama wa wapitaji wa barabara ile? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hii aliyoitamka ya Igawa kwenda Makete inapita milimani na ni barabara muhimu sana katika uchumi wa wananchi wa maeneo hayo. Pia amesema kwamba ni barabara ambayo Mheshimiwa Spika anapita. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa maeneo hayo kwamba, hii barabara ni miongoni mwa barabara ambazo ziko kati ya huu Mradi wa *EPC + Financing* kuanzia Igawa – Mbeya mpaka Tunduma.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambazo zinakwenda kusainiwa, kwa ridhaa yako naomba nizitaje hapa ili Waheshimiwa Wabunge wasipate nafasi ya kuwa na mashaka.

(i) Ifakara – Malinyi – Lumecha hadi Songea;

(ii) Igawa - Mbeya – Tunduma;

(iii) Karatu – Haydom – Mbulu – Sibiti hadi Maswa;

(iv) Mafinga – Mgororo;

(v) Masasi – Nachingwea – Liwale;

(vi) Kongwa – Kibaya – Arusha; na

(vii) Handeni – Kiberashi – Chemba - Kwa Mtoro hadi Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zitasainiwa mwezi wa sita, na tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, katika historia ya nchi hii tunakwenda kusaini kilometa zaidi ya 2000 na Mheshimiwa Waziri alikwisha tamka akiwa pale Singida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nilitaka nimuulize tu Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini sasa mtakuja Kiteto kusaini mkataba wa hii barabara ya Kongwa – Kiteto mpaka Arusha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hii ni miongoni mwa barabra ambazo nimezitamka hapa kwamba zitasainiwa kabla ya mwezi wa sita. Barabara ambazo ziko katika *EPC+ Financing*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na umuhimu mkubwa wa kiuchumi na shughuli za kijamii kwa wananchi wa Ngoreme hasa upande ule wa Majimoto, Busawe na Iramba. Ni lini sasa barabara ya Musoma kutoka pale makutano ya Nyakanga mpaka Sirori Simba kupitia Iramba - Majimoto mpaka Nyasirori itajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitamka Mheshimiwa Mbunge, ni barabara ambayo katika mwaka huu wa fedha tulikuwa tumeifanyia upembuzi yakinifu wa awali na katika mwaka wa fedha ujao tutaifanyia upembuzi yakinifu wa kina kama maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 370

**Ujenzi wa barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya – Tabora na Singida**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa barabara inayounganisha Mikoa ya Mbeya, Tabora na Singida inayoanzia Makongolosi hadi Rungwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi – Rungwa – Mkiwa yenye kilometa 503.36 kwa awamu. Sehemu ya Mbeya – Chunya – Makongolosi yenye kilometa 111 ujenzi umekamilika. Ujenzi wa sehemu ya Noranga - Itigi (Mlongoji) kilometa 25 umefikia asilimia 12 na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi sehemu ya Noranga – Doroto kilometa 6 na Itigi – Mkiwa kilometa 25.6 zimekamilika na Mkataba umesainiwa. Kwa sehemu iliyobaki ya Makongolosi – Rungwa - Noranga kilometa 356 na Mbalizi – Makongolosi kilometa 50 Serikali inaendelea kutafuata fedha kwa ajili ya ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza niseme sijaridhishwa na majibu ya Serikali kwa namna ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema. Kwa sababu tarehe 17 mwezi huu, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi akiwa Singida akisaini mikataba aliitaja barabara yetu ya Makongolosi kuelekea Mkiwa kuwa na yenyewe itajengwa kwenye mradi huu wa barabara ambazo amezitaja hapa lakini majibu ya Serikali yanaonekana kugongana.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo niweze kuuliza sasa. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri, alikwishasema fedha zipo za kuweza kujenga zaidi ya kilometa 2300. Je, ni lini sasa Serikali

itatoa pesa hizi ili barabara yetu ya Makongolosi kwenda kuunganishwa mpaka Mkiwa iweze kujengwa kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana kiuchumi kuunganisha Mkoa wa Mbeya na Singida?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara ya kuanzia Makongolosi kupita mpaka Mkwajuni mpaka Mbalizi ni barabara ya vumbi na imeahidiwa muda mrefu kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami na tayari Serikali imeshatenga kilometa 50 kuweza kujengwa. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kuanzia Makongolosi hadi Mkwajuni ili iweze kuunganishwa mpaka Mji mdogo wa Mbalizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Njelu Kasasa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Lupa, kwa kufuatilia barabara hii ambayo ni *shortcut* ya kwenda katika Mkoa wa Mbeya kutokea Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii kama nilivyokwisha jibu kwenye majibu yangu ya awali yenye kilometa 503, tumekuwa tukijenga awamu kwa awamu. Pia hadi sasa tumesaini mkataba wa kipande hiki cha Noranga - Doroto kilometa sita na Itigi – Mkiwa kilometa 25.6. Maana yake nini? Maana yake tunaendelea na ujenzi mpaka Makongolosi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, nikuhakikishie ya kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kujenga barabara hii na katika mwaka wa fedha ujao pia tumetenga fedha kwa ajili ya kutoka Makongolosi kwenda Singida.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, barabara ya Makongolosi – Mbalizi. Barabara hii imekuwa ikitengewa fedha kila mwaka na mwaka huu imetengewa kilometa 50 na mwaka ujao pia tumewekea fedha za kuanza ujenzi wa barabara hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba barabara hii katika mwaka ujao wa fedha itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya Majita – Musoma – Busekela yenye urefu wa kilometa 92 imechukua muda mrefu sana kukamilika. Hadi sasa imekwishajengwa kwa kilometa tano tu.

Je, Serikali ni lini ina mpango wa kupeleka fedha za kumalizia barabra hiyo ukizingatia itaongeza au kukuza uchumi kwa wana Musoma Vijijini na Mkoa wa Mara kwa Ujumla?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, Agnes Marwa, kuhusiana na suala la barabara hii ya Majita – Musoma. Ni kweli tumekwishajenga kilometa tano na suala la kupeleka fedha tutaendelea kupeleka fedha katika barabara hii ili ikamilike kwa ukamilifu wake, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na foleni inayotokana kati ya Mkoa wa Morogoro na

Pwani. Ni lini ujenzi wa barabara nne kuanzia Chalinze mpaka Morogoro Mjini utajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christine Ishengoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ya Chalinze kwenda Morogoro ni barabara ambayo tumeifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kupitia makampuni ya Korea Kusini na mwezi wa nne walileta ripoti maalum inayoonesha ni kwa kiwango gani tujenge. Je, iwe ni kwa mfumo wa *PPP* ama iwe ktika mfumo wa *EPC + Financing?* Sasa Serikali imeona umuhimu wa barabara hii iwe katika mfumo wa *PPP*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge niwahakikishie na wananchi wote wa eneo hilo kwa sababu ni barabara kuu, kwamba barabara hii itajengwa kwa mfumo wa *PPP* na tayari tumeshaanza ku–*engage* na wakandarasi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALILY A. MLAGHILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya Uyole – Kasumulu ina zaidi ya miaka 35 sasa, muda ambao imekwishapita *design age* yake. Je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi wa kuanza kuiwekea hata *layer* ya juu badala ya kusubiri ibomoke yote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Jumbe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia barabara hii na nimhakikishie tu kwamba kwa kuwa hapa Kasumulu ni lango muhimu la kwenda katika Nchi Jirani ya Malawi. Katika bajeti zetu za *TANROADS* kupitia Mkoa wa Mbeya tumetenga fedha kwa ajili ya kuboresha barabara hii iweze kupitia wakati wote, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kwanza Waheshimiwa Wabunge, nimuombe radhi Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, nilipokuita mtu aliyekuwa ameomba swali kumbe alikaa kwenye kiti chako lakini haukuwa wewe. Kwa hiyo, nilikuita wewe kumbe haukuwa wewe uliyeomba swali la nyongeza. Kwa hiyo, nikuombe radhi kwa sababu wananchi wanaweza wakajiua kwamba Mbunge wetu yuko wapi na anaitwa haitiki? Haya sasa umepewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. nilitaka kuuliza swali la nyongeza kwamba barabara itokayo Malagarasi kwenda Uvinza, kipande cha kilometa 51 kimekuwa na muda mrefu sana na sasa kimeanza kutengenezwa lakini kinasuasua sana.

Nini mpango wa Serikali kuhakikisha wanamaliza maana barabara hiyo ni kipande hicho ndicho kilichobaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kati ya maeneo ambayo barabara imechukua muda mrefu ni pamoja na kipande hiki

cha Malagarasi – Uvinza ili Mkoa wa Kigoma uweze kuunganishwa na mikoa jirani ikiwemo Tabora.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa Kigoma. Mtakumbuka ziara aliyoifanya Mheshimiwa Rais, alipokuwa Kigoma ni miongoni mwa barabara hizi ambazo alizotoa maelekezo kwamba ni lazima ikamilike. Sisi Wizara ya Ujenzi katika bajeti hii inayoendelea na inayokuja tumetenga fedha kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa mmesimama wengi. Mheshimiwa Mbunge wa Chemba

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru Serikali kwa barabara yetu ya Kiberashi – Handeni – Chemba hadi Singida lakini ili barabara hiyo iweze kutumika vizuri kuna *interchange* mbili. Kwanza ni kutoka Zamahelo mpaka Donsee nyingine ni kutoka Goima hadi Bicha. Sasa nataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha *interchange* hizo zinajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Monni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pongezi za Serikali nazipokea kwa niaba lakini pongezi hizi ziende kwa Mheshimiwa Rais, maana yeye ndiye anayetoa hizi fedha na hususani katika ujenzi wa barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge umeizungumzia. Kwa kuanzia kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii nafikiri itakuwa vema zaidi tukianza kama ambavyo Serikali imepanga ndipo tuanze na hizo zingine kwa kuwa hii ndio itakuwa lango muhimu

la kuunganisha kati ya Mkoa wa Dodoma na Mkoa jirani, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya Mpanda – Kaliua – Ulyankulu mpaka Kahama yenye urefu wa kilometa 472 iko kwenye Ilani ya Uchaguzi 2015/2020 lakini iko kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025. Je, barabara hii sasa ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya kilometa 472 ni kweli iko kwenye Ilani ya 2025 na Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza ilani hii ya 2025. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba kwa kuwa bado tunaendelea na utekelezaji wa ilani hii, uwe na uhakika kwamba pia barabara yako itajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi. Ipo barabara ya kutoka Mbezi kwenda Mpiji Magohe au barabara ya *Victoria Road*. Ni barabara ambayo iko ndani ya mpango kwa miaka mingi na bajeti lakini iko chini ya ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini ndani ya ilani kwa miaka 10. Ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hii iko kwenye Ilani lakini pia tumekwisha ifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na katika bajeti ijayo nikuombe Mheshimiwa Mbunge tutakayoisoma jumatatu na jumanne, tuipitishe bajeti hiyo ili barabara hii iweze kujengwa kwa kuwa ni miongoni mwa barabara hizo pia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo kabla hatujaendelea na ratiba yetu. Tutaanza na tangazo linalohusu wageni waliopo Bungeni siku ya leo.

Kwanza tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika, na hawa tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; yupo Ndugu Amon Mpanju ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, ameambatana na mke wake Mrs. Analise Christian Mpanju, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Riziki Kingwande ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Wanawake Tanzania - Chama cha Mapinduzi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Neema Majule, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania CCM, Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Mwantumu Mahiza Mwenyekiti Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Fatuma Kange ambaye ni Mwenyekiti wa Jukwaa la uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Taifa. Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Stella Manda, Mwakilishi *UN Women,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Lilian Liundi, Mkurugenzi Mkuu wa *TGNP*. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mary Ngowi, muasisi wa *don't touch,* karibu sana. *(Makofi)*

Hawa wameambatana na viongozi mbalimbali, wapo Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wadau wa maendeleo kutoka *NMB, TCB, Azam TV* na *Manara TV,* karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia watangazaji wa Kipindi cha Dadaz kinachotetea Haki za Wanawake cha *EATV,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Mabalozi wa kueneza ujumbe wa kupinga ukatili, mabalozi, haya ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo pia wawakilishi wa jumuiya mbalimbali, Shirikisho la Machinga Taifa, Baraza la Wazee Taifa na Chama cha Wajane, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambaye ni mume wake, Wakili Msomi Muthesela Gwajima, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Mwanaidi Ally Khamis ambaye ni Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, na hawa ni Ndugu Seif Selemani ambaye ni Mume wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Zeyana Mohamed Ali huyu ni mtoto wake, lakini pia yupo Ndugu Ali Mohamed Ali ambaye pia ni mtoto wake, Seif Selemani ni yupi? Ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao pia wapo hapa Bungeni; tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni wafanyakazi kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge leo Mheshimiwa Angelina Malembeka anatimiza mwaka mmoja tangu alipougua sana na akaweza kuhudumiwa vizuri sana na Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa. Kwa hiyo, amewaalika leo akiwa anasherehekea mwaka mmoja baada ya matibabu aliyoyapata. Amenitumia ujumbe hapa kwamba anawashukuru sana wahudumu wote, madaktari wote na manesi wote ambao mlimuhudumia vizuri sana kuhakikisha mnarejesha afya yake. *(Makofi)*

Pia amewatumia salamu Waheshimiwa Wabunge anawashukuru sana kila mmoja wenu kwa mchango mliotoa kwa ajili ya kuhakikisha afya yake inatengemaa. Kwa hiyo

anawashukuru sana, sana, sana kwa maombi kwa michango na kwa wale walioweza kwenda kumuona. Mheshimiwa Malembeka tunakutakia kila la kheri sasa katika utekelezaji wa majukumu yako baada ya kupona. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sijazungumza sana kuhusu Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa kwa sababu tumetoka kupitisha hapa bajeti, na tuliwasifia sana, kwa hiyo sina haja ya kuzirejea hizo. Kwa hiyo, pongezi zile mnazichukua na za leo zote pamoja Hospitali ya Benjamin William Mkapa mnafanya kazi nzuri sana, tunawashukuru sana kwa kuendelea kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana, na nikisha keti hapa ninyi mnaruhusiwa kutoka hata kama hamjaitwa ili mwende mkaendelee kutoa huduma maana mmekuja wengi.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Cecil Mwambe kutoka Taasisi ya *Binti Lindi Initiative,* Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Amina Mzee kutoka Jijini Dar es salaam na Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni wasimamizi wa majengo *NSSF* kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni viongozi wa matawi kutoka Mbozi Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga kutoka Mkoa wa Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambaye ni Diwani kutoka Msalala Mkoa wa Shinyanga, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni viongozi wa uwekezaji kiuchumi kwa akina mama kutoka Mkoa wa Kagera. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Mohamed Monni na hawa ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 80 na walimu nane wa Shule ya Sekondari Bahi ya Jijini Dodoma, karibuni sana *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote na watumishi Ofisi ya Bunge kuwa madaktari kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Magonjwa ya Moyo *(JKCI)* wapo katika kituo chetu cha afya hapa Bungeni tangu tarehe 8 Mei na watamaliza kesho tarehe 19 kwa ajili ya kutoa huduma ya afya.

Madaktari hao ni hawa wafuatao; sijui kama wapo hapa Bungeni lakini nimeletewa na majina ya hao madaktari; Dkt. Damas Baruti ambaye ni Daktari wa Uzazi na Vizazi kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; Dkt. Salehe Mwinchete, Daktari wa Moyo kutoka *JKCI*; Dkt. Catherine Makunja ambaye ni

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka Mloganzila; yupo pia Ndugu Abubakari Mzee, Afisa Lishe kutoka Mloganzila; yupo pia Ndugu Leah Msigaro, Mtaalamu wa Magonjwa ya Macho na Uono kutoka *DRRH*; yupo pia Ndugu Shukuru Mbilinyi, Muuguzi kutoka *DRRH*, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huduma hizi zinaendelea kutolewa na siku ya leo na kesho baada ya hapo wataondoka. Kwa hiyo, wale ambao bado hawajaenda kupata hiyo huduma wanaweza kwenda ili watazamwe afya zao.

Baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa Mwaka 2023 *[The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

### Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA- KATIBU MEZANI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 *[The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023]***

*(Kusomwa Mara ya kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane miswada imeshasomwa kwa mara ya kwanza Miswada mitatu na miswada hii yote tutapata fursa ya kuijadili katika kipindi cha Bunge hili la bajeti. Ni miswada ambayo imeletwa kwa hati ya dharura na itatazamwa kwa mujibu wa kanuni zetu zinaruhusu jambo hilo. Ni miswada ya muhimu kwa hiyo itapelekwa kwenye Kamati zinazohusika. Wale ambao watakuwa wamepitia hiyo miswada na wanaona wana mawazo watayapeleka kwenye hizo Kamati zinazohusika. Kwa hiyo kamati zinazohusika zitapelekewa miswada hii na Wabunge wenye mawazo kuhusu miswada hiyo wanaweza kupeleka huko, lakini pia tutapata nafasi nzuri kabisa ya kuijadili hapa bungeni wakati utakapofika.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Dorothy gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia

Wanawake na Makundi Maalum, aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba hotuba yangu kama ilivyo wasilishwa kwenye kitabu changu cha hotuba iingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa mwaka 2022/2023 na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/2024. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali kwa kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, Kipekee niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Natambua kuwa Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa

ya kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika, na utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninamuahidi kwamba nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo anayoyatoa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 5 Aprili, 2023 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na weledi wa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchapakazi wake uliotukuka. Mwenyezi Mungu awajalie utashi, weledi na ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo, Waheshimiwa Wabunge mnajadili mambo ya muhimu sana na ya msingi lakini niwaombe mjadili kwa sauti ya chini au kama

inashindikana kabisa mnaweza kwenda nje kidogo mkajadiliana halafu mrejee hapa ndani ili tuweze kusikiliza hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, vilevile, nawapongeza sana Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Nawatakia majukumu mema katika kuliongoza Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Dkt. Moses Mpogole Kusiluka kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti hii. Kipekee namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis Mbunge, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa kwa jitihada zake za dhati katika kufikia kizazi chenye usawa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa

huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha mafanikio katika Nyanja za Maendeleo na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru kwa kuunda Kamati Maalum ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Aidha, nawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge walioteuliwa kutekeleza majukumu yao katika kamati husika. Kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Mb), na Makamu wake, Mheshimiwa Riziki Said Lulida (Mb), kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia wenye lengo la kuboresha huduma za ustawi na maendeleo ya jamii. Ninawaahidi kwamba, Wizara ninayoiongoza itazingatia ushauri na maelekezo yao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar. Pia naomba kutoa pole kwa Serikali na Chama cha Mapinduzi kufuatia kifo cha Ndugu Bernard Kamilius Membe aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje katika Serikali ya Awamu ya Nne na Mbunge wa Jimbo la Mtama, Lindi.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa pole kwa Uongozi wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na wafanyabiashara ndogondogo wote Mkoani humo, kufuatia vifo vya wafanyabiashara 13

vilivyotokana na ajali ya gari iliyotumbukia katika Mto Njoka tarehe 9 Aprili, 2023, wakati wakitokea mnadani. Vile vile, natoa pole kwa uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam na wafanyabiashara ndogondogo wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Wafanyabiashara Ndogondogo (SHIUMA) ngazi ya Mkoa, Ndugu Masoud Issa Chauka kilichotokea tarehe 19 Februari, 2023. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali, napenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023; Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nikianza na mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023; Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sera, mpango na mkakati pamoja na makubaliano Kitaifa na Kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa saba wa kitabu changu cha Hotuba. Katika mwaka 2022/2023, Wizara ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zilizoainishwa kwenye ukurasa wa nane na wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara Fungu 53; katika mwaka 2022/2023, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 8.5 kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo tumeviainisha kwenye ukurasa wa tisa wa kitabu. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 3,025,562,821.01 sawa na asilimia 35.59 ya makadirio ya mapato.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa makusanyo ya mapato kunatokana na wanafunzi wengi kutoripoti kama ilivyokadiriwa na vyuo. Tumeziweka takwimu kwenye ukurasa wa 10 kwenye aya ya 16. Aidha, ulipaji wa ada kwa muhula wa pili unatarajiwa kufanyika katika kipindi cha Machi hadi Juni, 2023, hivyo tunasubiri kipindi hiki kifike. Vile vile, Wizara imefuta usajili wa mashirika yasiyo ya Kiserikali 4,898 kutokana na ukiukwaji wa sheria na kanuni na miongozo. Hii yote pia imeathiri makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya matumizi ya shilingi 43,403,061,000, mchanganuo kamili wa idhinisho hili uko ukurasa wa 10. Vile vile, baada ya kuidhinishiwa bajeti hiyo, Wizara iliongezewa kiasi cha shilingi 22,925,892,250 kwa ajili ya kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo (Machinga), hivyo kufanya jumla kuu kuwa shilingi 66,328,953,250. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwajali sana Wamachinga ambao ni sehemu kubwa ya wafanyabiashara ndogo ndogo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi 31,792,546,707.44, hizi ni kati ya Shilingi 43.4 zilizopitishwa kabla ya nyongeza. Hii ni sawa na asilimia 73 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo kwa kina uko ukurasa wa 11 aya ya 18. Kuhusu shilingi bilioni 22.9 kwa ajili ya kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo zilizoongezwa baada ya kupitishwa zile za awali, Wizara inakamilisha taratibu za kuzipokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara; katika mwaka 2022/2023, utekelezaji wa majukumu ya

Wizara ulilenga kuboresha huduma mbalimbali ambazo tumeziainisha ukurasa wa 12 katika aya ya 19. Nianze na huduma za maendeleo ya jamii kwa ufupi. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika halmashauri zote nchini wameendelea kutoa mchango wao wa utaalam katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996, kupitia Programu ya Kuamsha Ari ya Jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo, ikiwemo Kampeni ya Kitaifa ya Ujenzi wa Makazi Bora na Kukuza Moyo wa Uzalendo na kufanya kazi kwa bidii, ili kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Makazi Bora Nafuu kwa kutumia mifumo ya asili ya kusaidiana, tumeuainisha kwa kina ukurasa wa 13 ambapo jumla ya nyumba 730 zimejengwa na kufanya ongezeko la asilimia 14 kutoka 5,002 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia 5,732 Aprili, 2023. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022, hadi Aprili, 2023, Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na mamlaka za uongozi ngazi mbalimbali wameendelea kutumia taaluma yao kuhamasisha jamii kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye mikoa yetu yote 26. Jumla ya miradi 10,211 imetekelezwa, hii ikiwemo afya, elimu na yote ambapo wale wataalam wa maendeleo ya jamii wanakua mstari wa mbele. Tumeeleza kwa kina kwenye ukurasa wa 14.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuchochea hamasa na utayari wa wananchi kushiriki kwenye kujiletea maendeleo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeandaa Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi tunaita *bottom up* wa mwaka 2022/2023 tunakwenda nao 2025/2026. Lengo la Mpango huo ni kuwezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo ngazi ya jamii na Taifa kwa kutumia rasilimali walizonazo. Kimsingi, utekelezaji wa Mpango huo utachochea na kufanya mageuzi ya kifikra, mtazamo na utendaji kwa timu ya wataalam ngazi

ya kata, ambao wataalam hawa kwa ufupi tumewataja ukurasa wa 14 mpaka wa 15.

Mheshimiwa Spika, Mpango huo wa Maendeleo ngazi ya Msingi umeendelea kutekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetoa vibali na kutangaza nafasi za ajira 800 za Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao watakuwa chachu ya kufanya mageuzi ya fikra na kuchochea utekelezaji wa mpango huo wa *bottom up*. Aidha, katika kuimarisha na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, Wizara yangu imenunua na kusambaza pikipiki 85 kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote za ushirikishaji jamii zinazofanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii Nchini, bado tuna upungufu wa Maafisa hawa kwa takribani asilimia 56 kama ambavyo takwimu tumeziweka ukurasa wa 22. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa nafasi za ajira 800 za wataalam hawa wa maendeleo ya jamii, hivyo sasa uwepo wa maafisa hao umepanda hadi kufikia asilia 71.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kwa ufupi kuhusu uratibu wa shughuli za kiuchumi za makundi maalum; Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia mipango na programu mbalimbali za kuwezesha na kuendeleza kiuchumi makundi maalum ya wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo Machinga, Mama na Baba Lishe, waendesha bodaboda na bajaji ambao hupata changamoto za kuzifikia fursa zilizopo ili wajikwamue kiuchumi. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya kuhifadhi *Data* Kimtandao *(NIDC)*, Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)*, Wizara za Kisekta pamoja na wadau tumekamilisha maboresho ya Mfumo Jumuishi wa Kidijitali wa

Usajili na Utoaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini. Mfumo huo upo kwenye hatua ya majaribio na tunataka uanze kutumika rasmi Mwaka huu wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya shilingi milioni 260 tayari zimetolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Oktoba, 2022, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake ya tarehe 17 Mei, 2022 ya kuwezesha ujenzi wa Ofisi za Machinga ngazi ya mkoa nchi nzima. Hivyo nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza ahadi yake ambayo itasaidia upatikanaji wa ofisi za wafanyabiashara ndogondogo katika mikoa yote. Taarifa kwa kirefu iko ukurasa wa 25 mpaka 30.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye haki na maendeleo ya mtoto; Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa haki za msingi kwa mtoto ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na kutobaguliwa. Hata hivyo, baadhi ya watoto hawazipati haki hizo na hivyo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo vitendo vya ukatili katika familia na jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia changamoto za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta tumeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya upatikanaji wa haki za watoto na kupinga ukatili dhidi yao kupitia makundi yote katika jamii. Katika kufikia kundi kubwa la watoto kwenye shule, Wizara tumeratibu uundaji wa Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika shule za msingi na sekondari kama takwimu zilivyo ukurasa wa 31. Mkoa wa Dar es Salaam umeshaunda madawati haya kwenye shule zake zote za msingi, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa haki ya watoto ya kushiriki katika kujadili masuala yanayowahusu, tumeendelea kuhuisha na kuunda Mabaraza ya Watoto kuanzia ngazi za kijiji, mitaa hadi ngazi ya Taifa. Tuna mabaraza 592 sasa yameanzishwa na hii ipo ukurasa wa 32.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za usalama wa watoto katika mabasi ya shule na kuimarisha malezi, makuzi na usalama wa watoto shuleni; kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Serikali imetoa Waraka wa Elimu Namba Moja wa Mwaka 2023 kuhusu uboreshaji wa huduma ya magari na mabasi yanayotumika kusafirisha wanafunzi hawa. Maelezo yote haya yapo kuanzia ukurasa wa 34 mpaka wa 35.

Mheshimiwa Spika, katika azma ya kuongeza uelewa na hamasa ya jamii kwenye ushiriki wa malezi, makuzi na ulinzi wa watoto, tumeendelea kusimamia na kuratibu kampeni mbalimbali za kijamii ili kuwahamasisha washiriki mapambano haya. Kampeni hizi tumezieleza kwa kina ukurasa wa 35 mpaka 38 ambazo ni pamoja na Twende Pamoja Ukatili Sasa Basi, Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA) mtakuwa mnawaona huko kwenye mitaa yetu na kauli mbiu yao ni "Kataa Ukatili, Wewe ni Shujaa". Tuna kampeni nyingine ya kuwafahamisha wananchi kuhusu fursa za kiuchumi inayosema "Zijue Fursa, Imarisha Uchumi, Kataa Ukatili, Kazi Iendelee", au kifupi ZIFIUKUKI.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko la vitendo vya mmomonyoko wa maadili katika jamii, tarehe 15 Mei, hivi juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Familia, Wizara tumezindua kampeni yetu sote na sisi tushiriki inayohusisha wadau mbalimbali kulinda maadili, mila, desturi na tamaduni zetu. Kampeni hii inaongozwa na kaulimbiu "Taifa Letu, Maadili Yetu".

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhusisha wadau wenye ushawishi mkubwa kwa jamii katika kuimarisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia. Miongoni mwa wadau hao ni Klabu za Mpira wa Miguu ambapo tayari Yanga mabingwa kabisa na Azam wameunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwapongeza klabu ya Mpira wa Miguu Yanga kwa ushindi walioupata jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Mungu amewabariki kwa sababu na wenyewe wamebeba ajenda ya kutetea watoto na wanawake ambao wanakatiliwa. Hivyo, tunatambua mchango mkubwa wa vyombo mbalimbali vya habari ambavyo vimekuwa mstari wa mbele wakati wote na tunaendelea kutoa wito kwa vilabu vingine vyote vya michezo na vyombo vya habari na kila mdau mmoja mmoja kuingia kwenye mapambano haya na hususan Klabu ya Mpira wa Miguu Simba, tunawakaribisha sana tukaungurume, tukapambane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa haki za watoto kisheria, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeratibu ukusanyaji wa maoni ya marekebisho ya Sheria ya Mtoto, Sura Namba 13 ya Sheria za Tanzania sambamba na kufanya uchambuzi na hatimaye kupendekeza vifungu vinavyopaswa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kupitia Bunge lako tukufu kwa kutoa maelekezo kuhusu marekebisho ya Sheria za Makosa ya Jinai katika kuimarisha juhudi za kupambana na mmomonyoko wa maadili. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa

maelekezo ya namna ya kushughulikia masuala ya mmomonyoko wa maadili Nchini ambapo Wizara imeanza kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia changamoto za kundi la vijana balehe nchini; kundi hili lina tatizo, tumeeleza kwa kina kinachoendelea kwenye ukurasa wa 45.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue dakika chache kwenda huduma za ustawi wa jamii ambazo tumezielezea kwa kina ukurasa wa 49 mpaka wa 72. Wizara inaendelea na utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi kupitia Serikali za Mitaa katika halmashauri zote ambao unawezesha kuwasajili na kuwapa watoto huduma pamoja na kaya zao. Kwa kipindi cha utekelezaji tatizo la watoto wanaoishi kufanya kazi mitaani limepungua kwa asilimia 38. Nitoe rai kwa wazazi, walezi na jamii kuwajibika katika malezi, makuzi, matunzo na ulinzi wa watoto ili kuwezesha familia kuwa sehemu salama kwa watoto kuishi na kufurahia haki zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara, inaendelea kuratibu huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia ambayo hii nayo inachangia kuwapeleka watoto waende mitaani. Katika kipindi cha utekelezaji, migogoro ya ndoa imeshuka kwa asilimia 27 ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita kutokana na jitihada zinazoendelea kufanywa kwenye kutoa elimu ya athari ya migogoro ya ndoa katika familia kwa ujumla. Nitoe rai kwa wanandoa kutafuta suluhu ya mapema kwa kufika katika vyombo vya usuluhishi na upatanishi ikiwemo ofisi za ustawi wa jamii pale ambapo kuna dalili za mifarakano ili kuzuia migogoro au kuvunjika kwa familia.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuratibu utoaji wa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza na wasiokuwa na mtu wa

kuwahudumia katika makazi 14 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali na mengine makazi 15 ya taasisi binafsi. Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wazee wasiojiweza 259 wanahudumiwa katika makazi ya Wazee ya Serikali na wazee 268 katika makazi ya watu binafsi. Taarifa zaidi iko ukurasa wa 58 mpaka 59. Wizara inakamilisha Mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 ili kuendana na mahitaji ya wazee kwa kipindi cha sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za utoaji wa huduma za ustawi wa jamii, bado tunachangamoto ya maafisa hawa, ambapo kuna upungufu wa maafisa 20,057 hii ni sawa na asilimia 95.3 ya maafisa wanaotakiwa kama takwimu tulizoziainisha ukurasa wa 60.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake; Wizara katika kukuza usawa na uwezeshaji wanawake, inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi chenye Usawa kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2026 ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Kinara wa utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa Kiuchumi kwa Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu hii unajumuisha kuanzisha na kuendeleza vituo vya malezi na makuzi ya watoto; Kuongeza uwekezaji katika usambazaji wa maji, umeme na nishati mbadala; Kuongeza kazi zenye staha kwa kuendeleza biashara, urasimishaji wa biashara za wanawake; na Kuboresha upatikanaji na matumizi ya teknolojia nafuu na zinazofaa ili kuongeza uwezo wa wanawake kuzalisha bidhaa zenye ushindani wa soko la ndani na nje. Zipo afua zingine za programu hii kisekta maana sekta zote zimeingia kwenye utekelezaji. Sisi ni waratibu, hii iko ukurasa wa 63 hadi wa 82 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha malezi na makuzi ya awali ya mtoto kwa ustawi wa watoto na familia, Wizara kupitia Programu ya Kizazi chenye Usawa hii niliyoisema imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vituo vya malezi na makuzi ya awali ya mtoto ambavyo vinasaidia kutoa huduma ya uchangamshi wa awali inayowasaidia watoto kukua kimwili, kiakili, kiafya, kihisia na kimaadili. Vituo hivi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha ulinzi wa watoto wakati wazazi na walezi wao wakijihusisha na shughuli za kiuchumi yaani kwenda kazini.

Mheshimiwa Spika, takwimu chache ziko hapa katika kipindi cha utekelezaji jumla ya vituo 148 vya kulelea watoto mchana vimeanzishwa na kufikia jumla ya vituo 2,833 vyenye Watoto. 175,039 ni idadi ya watoto ambao wapo kwenye vituo hivi vya malezi na makuzi. Vile vile, Wizara imeratibu uanzishwaji wa vituo vya kijamii vya malezi na makuzi ya watoto na kufanya jumla ya vituo kuwa 3,033. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu ya Nchi ya Kizazi chenye Usawa hii niliyoisema, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Jana tumezindua Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Taifa na Mwenyekiti wetu Fatma Kange yuko hapa umetoka kumtambulisha. Hivyo, jumla ya majukwaa 3,091 yameanzishwa katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, halmashauri 140 na kata 1,149, vijiji na mitaa 1,776.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa majukwaa haya umeanza kujidhihirisha kwa baadhi ya mikoa na halmashauri ambapo Jukwaa la Mkoa wa Dodoma limeanzisha *SACCOs* ya wanawake yenye wanachama 322 na Jukwaa la Halmashauri ya Ushetu limeanzisha Mradi wa Kampuni ya Usafi wa Mazingira na Usindikaji wa Mboga za Majani maarufu kwa jina la *Nsansa*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa kuhusu kizazi chenye usawa ni maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa ambapo Tanzania imeendelea kung'ara na kuheshimika kutokana na mafanikio yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wake. Kupitia Jukwaa hili Tanzania imechaguliwa kuwa kiongozi wa kundi la kimataifa linalojumuisha nchi saba zinazotoa mwongozo wa utekelezaji wa maeneo yote ya Kizazi Chenye Usawa. Yaani Tanzania ingara ng'aring'ari Kimataifa kwenye eneo hili na inang'ara ng'ari ng'ari katika ya Nchi kiongozi zingine pamoja na Tanzania ni Marekani, Ufaransa, Mexico, Sweden, Afrika Kusini na Georgia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ikiwa mojawapo ya Nchi za Kusini mwa Afrika imepewa heshima ya kuwa mwenyeji mwenza wa mkutano wa mapitio ya nusu ya kipindi ya utekelezaji wa jukwaa la kizazi chenye usawa na mkutano huo utafanyika Septemba, 2023. Heshima hii imetokana na kudhihirika umahiri wa ukinara wa Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza maono ya jukwaa hili la kizazi chenye usawa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa masuala ya Jinsia yanazingatiwa katika sera, miongozo, mikakati na bajeti za Serikali, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha uandaaji wa nyaraka za uingizaji wa masuala ya jinsia katika Ofisi hiyo. Kwa kutekeleza hili, Wizara sasa itaweza kufahamu kwa kina utekelezaji wa bajeti ya Serikali inavyozingatia masuala ya jinsia *(gender compliance budget),* hivyo kuiwezesha Wizara kuandaa na kutekeleza mikakati ya ufumbuzi kwa maeneo yenye upungufu kwa sekta husika.

Mheshimiwa Spika, maneno machache kwenye uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali tumeendelea kusajili na kuratibu na kufuatilia mashirika haya kwa kuzingatia Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Namba 56. Wizara ilifanya uchambuzi kwa uzingatiaji wa sheria na miongozo ambapo ilibainika kuwa kufikia Aprili, 2023 kati ya mashirika 14 na 59 yaliyokuwa na usajili 4,898 yalibainika kutozingatia sheria ambapo Januari 2023 Bodi ya Uratibu wa Mashirika haya iliyafutia usajili. Taarifa kwa kina iko ukurasa wa 83 hadi 90.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kupongeza mashirika yote yanayofanya kazi kwa kuzingatia sheria za nchi pamoja na nyaraka za usajili wao. Ninayakumbusha mashirika yote kufuata misingi ya sheria na kuzingatia mila na desturi na tamaduni za Kitanzania katika utekelezaji wa majukumu yao. Ninaiasa jamii kuendelea kufichua vitendo vilivyo kinyume na maadili endapo vitaonekana vina fanywa na baadhi ya mashirika tuliyoyasajili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu wa utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa wa kupambana na kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto, wizara imekuwa ikitekeleza mpango kazi huu kuanzia Juni mwaka 2017/2018 - 2021/2022. Ajenda ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni endelevu, hivyo pamoja na utekelezaji wa mpango huu awamu ya kwanza kukamilika, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zikiwemo kukamilisha mpango wa awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekubaliana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ajenda hii ya kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto au ukataili wa kijinsia na kwa watoto itakuwa ya kudumu kwenye vikao vyote vya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuhakikisha mamlaka za Serikali za Mitaa

zinatunga sheria ndogo za kupinga ukatili katika maeneo yao. Maelezo kwa kina yako ukurasa wa 90 hadi 93.

Mheshimiwa Spika, tunatekeleza pia majukumu katika taasisi zilizo chini ya Wizara yetu, taasisi hizi ni Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Taarifa kwa kina iko ukurasa wa 94 hadi 104 na katika kipindi hiki Taasisi ya Ustawi wa Jamii imefanya mambo mengi pamoja na ya Tengeru lakini niisemee hii Taasisi ya Ustawi wa Jamii imepeleka jumla ya wahitimu 12 Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni Tanga na wahitimu 67 katika Halmashauri na mashirika binafsi. Wahitimu hawa 12 walio Kijiji cha Msomera wanatoa huduma mbalimbali za ustawi wa jamii kwa kipindi cha miezi sita kwa wananchi waliohama kutoka Ngorongoro na wenyeji wa eneo hilo kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maendeleo. Katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, Wizara tumeendelea kutekeleza afua mbalimbali za miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika taasisi na vyuo vilivyo chini yetu. Katika kipindi hiki cha utekelezaji tumeweza kupokea fedha za ndani za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 4.97 ili kutekeleza mradi wa ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kwa shilingi bilioni 3.97 na mradi wa huduma za ustawi wa jamii kwa shilingi bilioni moja. Tumechanganua kwa kina ukurasa wa 105 mpaka 107.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kuzungumzia vipaumbele vya Wizara, bajeti, mapato na matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2023/2024. Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele 10 ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Vipaumbele hivyo ni pamoja na: -

(i) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi;

(ii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;

(iii) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi *(Bottom Up);*

(iv) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo;

(v) Kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo niliowataja ili kuboresha mazingira ya biashara zao;

(vi) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi za Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii na Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii;

(vii) Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwepo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali;

(viii) Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki za watoto na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee;

(ix) Kuimarisha mifumo ya malezi, ulinzi na maendeleo ya watoto na familia; na

(x) Kuimarisha utendaji kazi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ili mchango na ushiriki wa mashirika hayo katika maendeleo ya Taifa uweze kutambulika na kuwa na tija kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa mwaka ujao wa fedha 2023/2024 imekadiria kutumia kiasi cha shilingi bilioni 74.2 katika kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya maeneo ambayo tumeyatengea fedha kwa kuoanisha vipaumbele vyetu: -

(i) Katika eneo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi tumetenge shillingi bilioni 4.9 kwa ajili ya kuratibu shughuli za usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi;

(ii) Katika eneo la kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, tumetenga shilingi bilioni 1.3;

(iii) Katika eneo la kutambua na kuratibu shughuli za kiuchumi za Makundi Maalum hususan wafanyabiashara ndogondogo niliowataja tumetenga shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza mahitaji na kuboresha shughuli zao za kiuchumi;

(iv) Katika eneo la watoto, tumetenga shilingi bilioni 3.6 kuwezesha utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi mazingira hatarishi na marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria, kufuatilia utoaji wa huduma katika makao ya watoto, nyumba salama na vituo mbalimbali vya kulelea watoto wadogo mchana na wale wengine wanaolelewa kwenye vituo vyetu katika umri wa aina mbalimbali. Pia fedha hizi zitatumika kukarabati shule ya maadilisho ya Irambo mahabusu za watoto za Upanga, Arusha, Mbeya, Moshi na Tanga na kukamilisha ujenzi wa mahabusu ya watoto Mkoa wa Mwanza;

(v) Katika eneo la wazee, tumetenga shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi kwa wazee wasiojiweza katika makazi yetu 14 kama nilivyoeleza pamoja na kukarabati miundombinu yao;

(vi) Kwenye eneo la taasisi na vyuo, tumetenga shilingi bilioni 3.1 na hii ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, vyuo vitatu vya Maendeleo ya Jamii vya Uyole, Monduli na Misungwi;

(vii) Katika oparesheni zote za kuratibu Mashrika Yasiyo ya Kiserikali, tumetenga shilingi bilioni 2.6 tuweze kuyasajili na tuweze kuyafuatilia na kuhakikisha wanatekeleza mpango wa uendelevu wa Mashirika haya Yasiyo ya Kiserikali wa mwaka 2022/2023 hadi 2025/2026 na kuratibu jukwaa la mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na vikao vya bodi yetu inayoratibu au ku-*regulate* mashirika haya;

(viii) Eneo la maendeleo ya jamii limetengewa kiasi cha shilingi milioni 283 kwa ajili ya kutekeleza kampeni ya kitaifa ya kuamsha ari ya jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi na kutekeleza ule mpango wetu wa kuhamasisha na kusimamia maendeleo ngazi ya msingi *(bottom up)* katika mikoa yote 26; na

(ix) Katika eneo la ufuatiliaji na tathmini wakati wa utekelezaji, tumetenga shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu. Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki,

Mashirika ya Kimataifa na Sekta mbalimbali zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki zikiwemo Marekani, Ufalme wa Uingereza, Ufalme wa Sweden, Ufalme wa Norway, Falme za Nchi za Kiarabu, Japan, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Canada, Ufalme wa Denmark, Ireland, Jamhuri ya Uswisi, Italia, Bangladesh na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara, hawa ni pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo *UN-Women, UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, ILO, IOM, FAO, WFP, UNHCR* na *UNESCO*. Vilevile, ninashukuru Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Umoja wa Afrika. Pia nayashukuru Mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation*. Pia, nazishukuru Taasisi za Kifedha za hapa nchinini kwetu ambapo ni pamoja na Benki za *NMB, CRDB*, Benki ya Biashara Tanzania - *NBC*, *Stanbic*, Azania, *Equity*, Benki ya Mkombozi, Akiba *Commercial Bank* na Benki ya Watu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nayashukuru Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi na Mashirika ya Dini kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Hawa ni pamoja na *Foundation for Civil Society*, *WiLDAF*, *ICS*, *TAWLA, TAYOA, LSF, SOS Children's Village* Tanzania, *Railway Children* Tanzania, *BRAC* Maendeleo Tanzania, *Plan International* - Tanzania, Kivulini*, FSDT, WFT, TANLAP, The Aga Khan Foundation*, *HelpAge International*, *Save the Children, World Vision, PACT* Tanzania*, Equality for Growth,*

*Landesa*, *CAMFED*, *CSEMA*; *REPPSI*, Amani *Girls Home*, *Pelum Tanzania*, *LHRC*, Haki Elimu, *TWCC*, *Compassion International, Care International* Tanzania, *TECDEN, EGPAF*, *Responsible Organization* Tanzania, *FAGDI*, *Safe Society Platform* Tanzania, *Both Ends Believing*, *MEWATA* na *Children in Crossfire*.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani zangu kwa Jumuiya za makundi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Wizara. Hawa ni pamoja na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jukwaa la Ulingo, Jumuiya ya Wazazi CCM, Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Baraza la Wazee Tanzania, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *TAWIA*, Chama cha Wazee Wanaume Tanzania, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA), Umoja wa Baba Lishe na Mama Lishe Tanzania, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA) na Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT).

Mheshimiwa Spika, pia naomba nizishukuru Klabu za Mpira wa Miguu Tanzania na hususan Yanga na Azam na vyombo vyote vya habari vinavyotuunga mkono kutoa taarifa zetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani zangu za dhati pia kwa viongozi wa taasisi za dini zikiwemo Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania *(TEC)*, Jumuiya ya Kikristo *(CCT),* Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania *(CPCT)* na Kanisa la Waadventista Wasabato *(SDA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Naomba kumshukuru Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu na Ndugu Amon Mpanju, Naibu Katibu Mkuu kwa mchango na

ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Nawashukuru Makamishna, Wasajili, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mahiri uliowezesha kukamilisha maandalizi ya hotuba yangu kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Maafisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii nchini kote ambao wamekuwa wakifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha wanagusa jamii katika maeneo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru Bodi na Menejimenti za Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane vya Maendeleo kwa ushirikiano wao mzuri unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. Nazishukuru sekta zote tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote wanaofuatilia Wizara yetu na kutupa ushirikiano. Nawaasa waendelee kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya Taifa letu wote wanaofanya kwenye taasisi hizi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI, nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote na wataalam wote nchini chini ya Ofisi zao na pia wadau wote wa sekta mbalimbali wanaowahudumia katika maeneo yao pamoja na wananchi mmoja mmoja na mitandao yote ya habari ya mtu mmoja mmoja ambao imekuwa ikipeleka taarifa zetu na kuleta tija kwenye jamii kujua nini kinaendelea, nini wafuatilie ili kuepuka ukatili wa kijinsia na kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu hususani mume wangu mpendwa

Wakili Msomi Methusela Gwajima ambaye leo tuko naye hapa na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu, kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Nawashukuru wananchi wote wa Tanzania ambao wamekuwa wakiunga mkono mapambano yote tunayoyafanya kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuwasilisha maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Mwaka 2023/2024. Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2023/2024 tumekadiria kukusanya shilingi bilioni 8.5 kutokana na ada katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya mafunzo ya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii na mapato mengine.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida. Katika mwaka 2023/2024 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 43,664,963,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 26,577,510,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 17,087,453,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo. Wizara inakadiria kutumia shilingi 30,558,230,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 26,800,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 3,758,230,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/2024 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Fungu 53 inaomba jumla ya shilingi 74,223,193,000 ili kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo na utawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum *www.jamii.go.tz*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, MHE. DKT. DOROTHY O. GWAJIMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka 2022/23 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/24. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2023/24.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Menyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kutuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika Nyanja

mbalimbali kwa kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake. Kipekee niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Natambua kuwa Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninamuahidi kwamba nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi pamoja na kuzingatia haki za wazee, wanawake, wanaume na watoto katika jamii. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo anayoyatoa mara kwa mara.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 5 Aprili, 2023 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2023/24.

**5.** ***Mheshimiwa Spika****,* ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na weledi wa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb),** Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

uchapakazi wake uliotukuka. Mwenyezi Mungu awajalie utashi, weledi na ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, nawapongeza sana **Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb)**, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na **Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Nawatakia majukumu mema katika kuliongoza Bunge.

**7. *Mheshimiwa Spika,*** aidha, napenda kumpongeza **Dkt. Moses Mpogole Kusiluka** kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti hii. Kipekee namshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb),** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

**8. *Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii, kumshukuru **Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb),** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa kwa jitihada zake za dhati katika kufikia kizazi chenye usawa nchini. Chini ya uenyekiti wake, Kamati imeweza kuanzisha na kutekeleza Programu ya Kizazi Chenye Usawa (Tanzania Generation Equality Programme - TGEP, 2021- 2026) inayoainisha afua muhimu zitakazo tekelezwa na Wizara za Kisekta na kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeachwa nyuma katika maendeleo na ujenzi wa Taifa

letu. Afua za Programu hiyo zimeanishwa katika Aya Namba 91 ya Hotuba hii.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha mafanikio katika Nyanja za Maendeleo na Ustawi wa Jamii yanafikiwa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika*,** nitumie fursa hii kukushukuru kwa kuunda Kamati Maalum ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Aidha, nawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge walioteuliwa kutekeleza majukumu yao katika kamati husika. Kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti **Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Mb)** na Makamu wake, **Mheshimiwa Riziki Said Lulida (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia wenye lengo la kuboresha huduma za ustawi na maendeleo ya jamii. Ninawaahidi kwamba, Wizara ninayoiongoza itazingatia ushauri na maelekezo yao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi kwa moyo wote ndani na nje ya Bunge.

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu **Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar. Pia naomba kutoa pole kwa Serikali na Chama cha Mapinduzi kufuatia kifo cha **Ndugu Bernard Kamilius Membe** aliyewahi

kuwa Waziri wa Mambo ya Nje katika Serikali ya Awamu ya Nne na Mbunge wa Jimbo la Mtama, Lindi. Aidha, natoa pole kwa uongozi wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na wafanyabiashara ndogondogo wote Mkoani humo, kufuatia vifo vya wafanyabiashara 13 vilivyotokana na ajali ya gari iliyotumbukia katika mto Njoka tarehe 09 Aprili, 2023 wakati wakitokea mnadani. Vilevile, natoa pole kwa uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam na wafanyabiashara ndogondogo wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Shirikisho la wafanyabiashara ndogondogo (SHIUMA) ngazi ya Mkoa, Ndugu Masoud Issa Chauka kilichotokea tarehe 19 Februari, 2023. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/24.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2022/23

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Mpango Mkakati pamoja na Makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee (2003) na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008). Vilevile, katika kuandaa mpango na bajeti, Wizara imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030); na Agenda ya Afrika

Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum – GEF, 2021 – 2026).

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa ngazi ya jamii;

(ii) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii;

(iii) Kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ili kuboresha mazingira ya biashara zao;

(iv) Kuratibu na kusimamia afua za upatikanaji wa haki za mtoto, ulinzi na malezi chanya ya watoto;

(v) Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum, huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia na huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

(vi) Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee;

(vii) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake uchumi na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee; na

(viii) Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa.

**Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara (Fungu 53)**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 8,500,000,000.00** kutoka kwenye ada za wanafunzi, uuzaji wa Mitaala ya kufundishia fani za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii pamoja na malipo ya hosteli katika vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Jamii na viwili (2) vya Maendeleo ya Jamii Ufundi. Vilevile, vyanzo vingine vya mapato ni ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ada za mwaka na faini kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 pamoja na marekebisho yake na mapato mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,025,562,821.01** sawa na asilimia **35.59** ya makadirio ya mapato.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** kushuka kwa Makusanyo ya Mapato kunatokana na wanafunzi wengi kutoripoti kama ilivyokadiriwa na Vyuo, ambapo katika mwaka wa masomo 2022/23, Vyuo vilikadiria kudahili Wanafunzi 8,191 lakini vilifanikiwa kudahili wanafunzi 5,255 ambao ni upungufu wa wanafunzi 2,936. Aidha, ulipaji wa ada kwa muhula wa pili unatarajiwa kufanyika katika kipindi cha Machi hadi Juni, 2023. Vilevile, Wizara imefuta usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 4,898 kutokana na ukiukwaji wa Sheria na Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za Mashirika hayo. Hatua hii pia imeathiri makusanyo ya mapato kwa kuwa ada za usajili na ada za mwaka za Mashirika haya ni moja kati ya chanzo cha mapato ya Wizara.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya matumizi ya **Shilingi 43,403,061,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 32,310,981,000.00**

ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 18,169,057,000.00** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 14,141,924,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 11,092,080,000.00** kilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 6,900,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 4,192,080,000.00** ni fedha za nje. Vilevile, baada ya kuidhinishiwa bajeti hiyo, Wizara iliongezewa kiasi cha **Shilingi 22,925,892,250.00** kwa ajili ya kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga) hivyo kufanya jumla kuu kuwa **Shilingi 66,328,953,250.00.**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 31,792,546,707.44 (kati ya Shilingi 43,403,061,000.00 zilizopitishwa kabla ya nyongeza)** sawa na asilimia **73** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 23,309,448,250.05** sawa na asilimia **72** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,127,015,771.05** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 12,182,432,479.00** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, **Shilingi 8,483,098,457.44** ni Fedha za Maendeleo sawa na asilimia **76** ya Bajeti ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 7,452,082,394.44** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,031,016,063.00** ni fedha za nje. Vilevile, kuhusu **Shilingi 22,925,892,250.00** kwa ajili ya kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga), Wizara inakamilisha taratibu za kuzipokea.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulilenga kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuchochea maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wa wanawake, kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za

maendeleo, kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Uratibu wa utekelezaji wa majukumu haya ulifanywa na Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali.

**ENEO LA 1: MAENDELEO YA JAMII**

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zote nchini wameendelea kutoa mchango wao wa utaalam katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996, kupitia Programu ya Kuamsha Ari ya Jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo, ikiwemo Kampeni ya Kitaifa ya Ujenzi wa Makazi Bora na Kukuza Moyo wa Uzalendo na kufanya kazi kwa bidii, ili kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Makazi Bora ulianza mwaka 2021/22 kwa lengo la kuhamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa gharama nafuu kwa kutumia mifumo ya asili ya kusaidiana kwa kuchangia nguvu kazi ikiwemo Msaragambo – Wapare na Mgoe - Wahehe. Aidha, jamii hutumia vikundi vya kuweka akiba na kukopa au mtindo wa kupeana fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya ujenzi kama vile saruji na bati. Ujenzi wa nyumba hizo hugharimu kati ya **Shilingi 7,000,000.00** hadi **10,000,000.00.** Katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, Kampeni hiyo imetekelezwa katika Mikoa yote isipokuwa minne ambayo ni Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro na Manyara. Utekelezaji katika Mikoa hii utaanza Julai, 2023. Jumla ya nyumba bora **730** zimejengwa na kufanya ongezeko la asilimia **14** kutoka **5,002** kwa mwaka 2021/22 hadi **5,732** kufikia Aprili, 2023. ***Nitumie fursa hii kuishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi***

***kwa Miongozo ya Kisera na OR-TAMISEMI kwa kusimamia utekelezaji wa Kampeni hii.***

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na mamlaka za uongozi ngazi mbalimbali wameendelea kutumia taaluma yao kuhamasisha jamii kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye Mikoa **26** ya Tanzania Bara. Jumla ya miradi **10,211** imetekelezwa, ikiwemo ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya **300**, ujenzi wa madarasa ya shule za msingi **1,911** na madarasa ya shule za sekondari **8,000** kama ilivyotajwa na **Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb)**, Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24. Ni dhahiri, uwepo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa kutosha utaongeza kasi na ari ya wananchi kushiriki na kumiliki shughuli za maendeleo.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuchochea hamasa na utayari wa wananchi kushiriki kwenye kujiletea maendeleo, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeandaa Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi (Bottom Up) wa Mwaka 2022/23 hadi 2025/26. Lengo la Mpango huo ni kuwezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo ngazi ya jamii na Taifa kwa kutumia rasilimali walizonazo katika kuibua changamoto, kupanga, kutekeleza na kufuatilia shughuli za maendeleo. Mpango huo umewasilishwa katika vikao kazi vya viongozi na watalaam wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo jumla ya viongozi na wataalam **833** walipewa mafunzo. Kimsingi, utekelezaji wa Mpango huo utachochea na kufanya mageuzi ya kifikra, mtazamo na utendaji kwa timu ya wataalam ngazi ya Kata wakiwemo Maafisa Watendaji wa Kata, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ugani wa Kilimo na Mifugo, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Afya na Waratibu Elimu kata

ili kuboresha utendaji na utoaji wa huduma katika sekta mbalimbali.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, Mpango huo wa Maendeleo ngazi ya Msingi umeendelea kutekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Wizara za Kisekta za Kilimo na Mifugo, Elimu na Afya kwa kusudi la kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa jamii katika ngazi ya Kata. Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali imetoa vibali na kutangaza nafasi za ajira 800 za Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao watakuwa chachu ya kufanya mageuzi ya kifikra na kuchochea utekelezaji wa mpango huo wa maendeleo katika jamii. Aidha, katika kuimarisha na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, Wizara yangu imenunua na kusambaza pikipiki **85** kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini. Vilevile, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imenunua pikipiki **900** kwa Watendaji wa Kata. Aidha, Wizara ya Kilimo imetoa pikipiki **5,889** kwa Maafisa ugani wa Kilimo katika mikoa 25 na Wizara ya Mifugo imetoa pikipiki **1,200** kwa Maafisa ugani wa Mifugo. ***Nitumie nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Wizara zote za kisekta kuweza kutekeleza mpango huo wa Maendeleo ngazi ya Msingi kwa kuendelea kujenga uwezo wa wataalam wao na kutoa vitendea kazi kwa wataalam ngazi ya Kata.***

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais -TAMISEMI ilifanya kikao kazi cha kuwajengea uwezo Maafisa Maendeleo ya Jamii **210** wakiwemo Wakuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii **184** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na Maafisa Maendeleo kutoka Sekretarieti za Mikoa **26**. Wataalam hawa walipewa mafunzo kuhusu:-

(i) Namna ya kuwezesha mijadala ya uzalendo, kufanya kazi kwa bidii na kujitolea ngazi ya jamii;

(ii) Usajili, Uratibu na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iii) Fursa za uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

(iv) Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kwenye Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa Tanzania;

(v) Mwongozo wa Malezi na Makuzi ya Watoto pamoja na Wajibu wa Wazazi katika Malezi; na

(vi) Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza Katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe.

***Nitoe rai kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na watendaji wote katika Ngazi ya Msingi nchini kuendelea kutekeleza wajibu wao kikamilifu kwani Serikali inatarajia kuona mabadiliko ndani ya jamii yanayolenga kuhimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii, kujitolea kwenye shughuli za maendeleo, kuwa wazalendo na kuipenda nchi yao.***

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Vyuo vya Buhare, Mlale, Monduli, Rungemba, Ruaha na Uyole pamoja na mafunzo ya Uhandisi Ujenzi na Maendeleo ya Jamii (Civil Engineering with Community Development) katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi Mabughai na Misungwi, kwa kusimamia ubora wa mafunzo na kuboresha miundombinu.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa miundombinu hiyo umewezesha kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi kutoka **5,135 (Me 2,112 na Ke 3,023)** kwa mwaka **2021/22** hadi wanafunzi **5,255 (Me 2,089 na Ke 3,166)** mwaka 2022/23, ikiwa ni ongezeko la wanafunzi **120** sawa na asilimia **2.3.** Aidha, mwaka

2021/22, wanafunzi **4,710** walihitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na wanafunzi **4,575** waliohitimu mwaka **2020/21** sawa na ongezeko la asilimia **3** ya wahitimu.

**28. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza programu ya uanagenzi kwa kuwaunganisha wanafunzi/wahitimu katika Vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Jamii na viwili (2) vya Maendeleo ya Jamii Ufundi kwenye Makampuni, Mashirika na Taasisi mbalimbali ili waweze kupatiwa ujuzi/kujengewa uwezo katika maeneo mahsusi kulingana na mahitaji yao. Katika mwaka 2022/23 jumla ya wanafunzi **578** walijiunga na programu hiyo ambapo kati yao wanafunzi **296** sawa na asilimia **51.2** wamefanikiwa kuhitimu mafunzo na miongoni mwao wanafunzi **55** wamepata ajira ambapo wanafunzi **17** wamejiajiri wenyewe na **38** wameajiriwa na Halmashauri. Tunazishukuru Halmashauri zilizoona umuhimu wa kuajiri vijana katika maeneo ya uhandisi ujenzi, uongozi, upangaji na usimamizi wa miradi, uundaji wa vikundi, utoaji wa ushauri nasaha, pamoja na uandishi wa miradi. Aidha, wengine wameajiriwa na Makampuni, Wakala na Mashirika mbalimbali. Kwa upande mwingine, wanafunzi **282** sawa na asilimia **48.8** wanaendelea na mafunzo hayo. Wizara imepanga kufanya ufuatiliaji maalum (tracer study) kwa wahitimu wa uanagenzi **241** ili kuwaelimisha kuhusu fursa za kiuchumi na ajira/kujiajiri pamoja na kuwashauri wajisajili kwa Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) ili waweze kuunganishwa na waajiri na kupatiwa nafasi za kujitolea.

**29. *Mheshimiwa Spika*,** katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru jumla ya wanafunzi **1,145** wa ngazi mbalimbali kuanzia cheti hadi shahada walijiunga na Programu ya Uanagenzi. Aidha, jumla ya wanafunzi **366** sawa na asilimia **31.9** walihitimu, wanafunzi **25** kati ya waliohitimu sawa na asilimia **6.8** walijiajiri, wanafunz**i 102** kati ya waliohitimu sawa na asilim**ia 27.9** waliajiriwa, wanafunzi **652** sawa na asilimia **56.9** ya wanafunzi

waliojiunga na Programu wanaendelea na mafunzo. Wizara itaendelea kuhimiza wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kujiunga na mafunzo ya uanagenzi ili kupanua fursa ya kuajirika, kujiajiri na kuajiri wengine kupitia miradi ya uzalishaji watakayoanzisha.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Jamii na vyuo viwili (2) Maendeleo ya Jamii Ufundi imeendelea kutekeleza programu mbalimbali zinazolenga kukuza ubunifu na maarifa. Katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya mawazo ya kibunifu **175 (wanafunzi 145 na wananchi 30),** yameibuliwa, na jumla ya mawazo ya kibunifu **(30)** yamefikia hatua ya kuendelezwa (kuatamiwa).

Kati ya hayo mawazo ya kibunifu **11** sawa na asilimia **6.2** yamekamilika na kuwa bidhaa au huduma ambazo ni pamoja na:

(i) Mashine ya kukaushia mboga iliyoibuniwa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba;

(ii) Maua na hereni kwa kutumia nyuzi na chupa; biskuti lishe; tambi lishe; maua ya karatasi na plastiki; zilizobuniwa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha;

(iii) Aidha, katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru wameibua bunifu zifuatazo:-

**(a)** ***Niuzie Point of Sale - POS"*** ambao ni mfumo wa kielektroniki unaowezesha Wajasiriamali kutunza kumbukumbu za mauzo, matumizi na manunuzi katika biashara na kusaidia wajasiriamali kukuza na kuendesha biashara kwa ufanisi. Hadi kufikia Aprili, 2023 mfumo umefanyiwa majaribio kwa wajasiriamali **20**.

**(b)** Mfumo wa "***Wajasiriamali Connect***" umetengenezwa kwa ajili ya kusajili wajasiriamali nchini na kurahisisha ufikiwaji katika kupata huduma.

**(c)** Mfumo wa ***"Ratiba Mtandao (etimetable)"*** unaowezesha kuandaa na kutumia ratiba kwa njia ya kielektroniki na hivyo kupunguza matumizi ya shajala. Mfumo kwa sasa unatumika na Taasisi katika kuandaa ratiba za masomo. Baada ya kukamilisha majaribio mfumo unaweza kutumika na Taasisi za Mafunzo na Shule za Msingi na Sekondari.

Mawazo haya ya ubunifu wa mifumo yamefikia katika hatua ya sampuli kifani (Prototype) na wabunifu husika watapewa rufaa kwenda katika kituo cha ubunifu cha Taifa ili mawazo yao yaweze kuboreshwa.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza programu ya ushirikishaji jamii zinazozunguka Taasisi na Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii kutatua changamoto zinazoikabili jamii kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka. Katika mwaka 2022/23, jumla ya wananchi **7,960** walipata mafunzo mbalimbali yakiwemo: elimu ya lishe **(3,003),** taratibu za unyonyeshaji **(250),** namna ya kutengeneza barabara za vijiji **(244),** elimu ya ujasiriamali kwa vikundi vya wanawake **(648),** elimu ya uhifadhi wa mazingira **(3,000)** na jinsi ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia **(815)** katika vijiji na mitaa inayozunguka vyuo.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi zote za ushirikishaji jamii zinazofanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini, bado tunakabiliana na changamoto ya uhaba wa Maafisa hao ambapo, kati ya **5,296** wanaohitajika waliopo kufikia Aprili 2023 ni **3,003** tu hivyo, upungufu ni **2,293** sawa na asilimia **56.7** kama inavyoonesha katika ***Jedwali Na. 1***. Mahitaji makubwa zaidi ya wataalam hawa yapo ngazi ya Kata ambapo kuna changamoto nyingi za jamii zinazopaswa kushughulikiwa.

**Jedwali Na. 1: Idadi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Ngazi Mbalimbali**

| NA. | NGAZI | MAAFISA WANAO-HITAJIKA | MAAFISA WALIOPO | | UPUNGUFU/ ZIADA | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | IDADI | % | IDADI | % |
| 1. | Mkoa | 52 | 48 | 92.3 | 4 | 7.6 |
| 2. | Halmashauri | 1,288 | 1,568 | 121.7 | 280 | 21.7 |
| 3. | Kata | 3,956 | 1,387 | 35.1 | 2,569 | 64.9 |
| | **JUMLA** | **5,296** | **3,003** | **56.7** | **2,293** | **43.3** |

***Chanzo: OR-TAMISEMI, 2023***

**33**. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa nafasi za ajira **800** za Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kati ya **2,293** wanaohitajika hivyo, kufanya uwepo wa maafisa hao kuwa asilimia **71.8** kutoka asilimia **56.7**.

***Nitoe rai kwa Wadau wa Maendeleo yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa ajira za muda kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii hususan katika ngazi ya Kata ambapo kuna upungufu mkubwa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa afua za kutatua changamoto zinazoikabili jamii yetu.***

**ENEO LA 2: URATIBU WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA MAKUNDI MAALUM**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia mipango na programu mbalimbali za kuwezesha na kuendeleza kiuchumi Makundi Maalum. Makundi yanayolengwa ni Wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo

Machinga, Mama/Baba Lishe, Waendesha Bodaboda na Bajaji ambao hupata changamoto kuzifikia fursa zilizopo kujikwamua na kukua kiuchumi kutoka kwenye taasisi za fedha kwa kuwa hawatambuliwi rasmi na pia hawana dhamana za kuwawezesha kukopesheka kwenye taasisi hizo.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC), Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Wizara za Kisekta pamoja na Wadau imekamilisha maboresho ya Mfumo Jumuishi wa Kidijitali wa Usajili na Utoaji wa vitambulisho kwa Wafanyabiashara ndogondogo nchini. Mfumo huo upo kwenye hatua ya kufanyiwa majaribio na utaanza kutumika rasmi mwaka wa fedha 2023/24 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Morogoro. Zoezi litaendelea katika Mikoa mingine iliyobaki na litakuwa ni zoezi endelevu. Mfumo huo ulioboreshwa utaisaidia Serikali kukusanya taarifa na takwimu muhimu za wafanyabiashara ndogondogo nchini katika sekta isiyo rasmi na hivyo kurasimisha utambulisho wao, kuwawezesha kupata fursa za mikopo yenye masharti nafuu kwenye taasisi za fedha, kurahisisha utengaji maeneo ya kufanyia biashara na kuwapanga katika maeneo yaliyo rafiki. Aidha, katika kipindi hiki cha mpito kabla ya mfumo huo kuanza kutumika, mfumo wa utoaji vitambulisho vya Machinga kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania utaendelea kutumika.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu mafunzo kwa viongozi 803 wa Wafanyabiashara ndogondogo kupitia Shirikisho la Wafanyabiashara ndogondogo (SHIUMA) tarehe 16 hadi 19 Mei 2022 hapa Jijini Dodoma. Kupitia mafunzo hayo, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alishiriki kwa njia ya simu na aliahidi kutoa **Shilingi Milioni 10** kwa kila Mkoa kwa ajili ya kujenga Ofisi za Wafanyabiashara ndogondogo ngazi ya Mkoa ili kuwawezesha kuondokana na upungufu wa Ofisi za kudumu.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jumla ya **Shilingi Milioni 260** zilizoahidiwa tayari zimetolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Oktoba 2022 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake ya tarehe 17 Mei, 2022 ya kuwezesha ujenzi wa Ofisi za Machinga ngazi ya mkoa nchi nzima kupitia OR – TAMISEMI. Vilevile, mikoa imetoa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo na ujenzi upo katika hatua tofauti ambapo baadhi ya mikoa ujenzi upo kwenye ngazi ya msingi na wengine kwenye uinuaji kuta. Aidha, kwa mikoa ambayo ujenzi haujaanza, natoa rai ujenzi uanze ili kuwezesha Wafanyabiashara Ndogondogo kupata ofisi za kudumu kwenye mikoa hiyo. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza ahadi yake ambayo itasaidia upatikanaji wa Ofisi za Wafanyabiashara Ndogondogo katika mikoa yote nchini.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa kwa kuendelea kushirikiana na wafanyabiashara ndogondogo ikiwemo kupitia Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) Taifa katika kuimarisha, kuendeleza na kuwezesha kukua kwa shughuli zao za kiuchumi ili waweze kuchangia Pato la Taifa. Mfano, kwa mkoa wa Dar es Salaam ushirikishwaji huo umewezesha viongozi 15 wa Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga) kunufaika na ziara ya mafunzo nchini Rwanda, ambapo walijifunza namna wafanyabiashara ndogondogo wanavyofanya biashara zao kwa kufuata sheria na taratibu za nchi pamoja na kushiriki katika utunzaji wa mazingira kwa kufanya usafi na kupanda miti. Aidha, viongozi hao kwa sasa wanaendelea na utoaji wa elimu hiyo miongoni mwao na ni mabalozi wa mabadiliko chanya kwa kushiriki katika shughuli za kijamii ikiwemo kufanya usafi, kupanda miti na kupendezesha miji yetu. Tunawapongeza Viongozi wa Mkoa huu na mikoa mingine yote ambao wameendelea kuwapatia fursa SHIUMA.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) Taifa kutoa elimu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini ili wazingatie utii wa sheria kwenye masoko nchini. Pia, ushirikishwaji huo umewezesha uhamishwaji wa wafanyabiashara ndogondogo kuingia kwenye masoko mapya kwa njia nzuri na shirikishi kwa maendeleo yao. Hivyo, ninawapongeza Wakuu wa Mikoa, Wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa hatua wanazochukua kuendeleza wafanyabiashara ndogondogo nchini pamoja na utayari wao wa kushirikiana nao kwa lengo la kuwawezesha kukua kiuchumi na kutatua changamoto zinazokwamisha maendeleo yao.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inawatambua wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo machinga kama kundi maalum linalohitaji kupewa kipaumbele katika kukuza uchumi wa nchi na kuzalisha ajira kwa wingi. Aidha, Serikali kupitia Halmashauri inaendelea kuweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kutenga na kuendeleza maeneo rafiki kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo kufanya biashara, ambapo hadi sasa jumla ya masoko 367 yameboreshwa nchini yenye uwezo wa kuhudumia wafanyabiashara ndogondogo 136,041. Baadhi ya masoko hayo ni pamoja na: Soko la Machinga *Complex Bahi Road* Jijini Dodoma linalohudumia takribani wafanyabiashara ndogondogo 3,000; Soko la Kigogo *Fresh* linalohudumia wafanyabiashara ndogondogo 430 na Soko la Bunju B linalohudumia wafanyabiashara ndogondogo 418 Jijini Dar es Salaam. Vilevile, ujenzi wa masoko hayo unaendelea katika Jiji la Tanga, Mbeya, Mwanza, Manispaa ya Morogoro pamoja na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Hivyo, napenda nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zinazowezesha ujenzi na uboreshaji wa masoko haya nchini.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetengewa jumla ya **Shilingi Bilioni 22,925,892,250** kwa ajili ya kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini mwaka 2022/23. Hata hivyo, kufuatia maelekezo ya Serikali kuwa fedha zitolewe kupitia mfumo wa kibenki, Wizara inakamilisha taratibu zote muhimu zitakazowezesha fedha hizo kuanza kutolewa kupitia mfumo wa kibenki ambao ni salama na rafiki kwa walengwa wakiwemo Wafanyabiashara Ndogondogo, mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji. Hivyo, mfumo huo wa kibenki utawezesha fedha hizo kuwa endelevu na utawasaidia walengwa kupata mitaji kwa ajili ya kupanua biashara zao.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa baadhi ya mikopo na utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa wafanyabiashara ndogondogo kupitia benki wanazohudumiwa ambapo kati ya Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya **Shilingi Trilioni 1.05** zimekopeshwa kwa wafanyabiashara ndogondogo **41,073**. Baadhi ya Madirisha yanayotumiwa ni pamoja na mikopo ya vikundi kupitia Tanzania Commercial Bank (TCB), Jikwamue *Loan Scheme* kupitia benki ya Azania pamoja na mikopo ya kilimo na biashara kupitia benki ya NMB. Hivyo, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa jamii pamoja na uhamasishaji wa taasisi hizo kuandaa bidhaa na fursa mbalimbali za kiuchumi kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo nchini. Pia, Wizara itashirikiana na taasisi hizo kuhakikisha kuwa bidhaa na huduma hizo zinawafikia walengwa kwa njia rahisi na rafiki hususan wale walioko vijijini.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na wafanya biashara ndogondogo ikiwemo viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) nchini kuhamasisha wafanyabiashara ndogondogo kushiriki katika shughuli mbalimbali za Kitaifa ikiwemo maonesho ya kibiashara. Jumla ya Wafanyabiashara ndogondogo 90 waliwezeshwa kushiriki

kwenye Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Maonesho ya Sabasaba) yaliyofanyika mwezi Julai, 2022. Vilevile, jumla ya wafanyabiashara 968 walishiriki katika Maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyofanyika Mkoani Mbeya mwezi Agosti, 2022. Hivyo, ushiriki wao katika maonesho hayo unawawezesha kujifunza pamoja na kupata fursa za kiuchumi zilizopo kwenye sekta zingine ndani na nje ya nchi.

**ENEO LA 3: HAKI NA MAENDELEO YA MTOTO**

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa haki za msingi kwa mtoto ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na kutobaguliwa. Hata hivyo, baadhi ya watoto hawazipati haki hizo na hivyo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo vitendo vya ukatili katika familia na jamii.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya sababu zinazosababisha ukatili dhidi ya watoto hapa nchini ni mwendelezo wa mmomonyoko wa maadili katika jamii unaoambatana na mila na desturi za jamii husika ambazo zinasababisha ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Kwa mantiki hiyo, Wizara itaendelea kutekeleza maelekezo ya mamlaka na viongozi wa kitaifa katika kuhakikisha elimu inatolewa kwa jamii ili kudhibiti vitendo vinavyoashiria maadili yasiyofaa pamoja na mila na desturi zenye madhara kwa wanawake na watoto. Wizara itazingatia maelekezo hayo wakati wote wa kutekeleza afua za ulinzi na usalama wa watoto.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kushughulikia changamoto za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta imeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya upatikanaji wa haki za watoto na kupinga ukatili dhidi yao kupitia makundi yote katika jamii. Katika kufikia kundi kubwa la watoto kwenye shule, Wizara imeratibu uundaji

wa Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika shule za msingi na sekondari nchini likiwa ni jukwaa mahsusi la watoto la kutoa taarifa za viashiria na vitendo vya ukatili vinavyofanywa ndani na nje ya shule kwa usaidizi wa walimu wa malezi na unasihi.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la kuunda madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto lilianza Julai, 2022 mara baada ya uzinduzi wa mwongozo wa Uundaji wa Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto ndani na Nje ya Shule. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya madawati 1,585 yameundwa katika shule za msingi (1,128) na sekondari (457) sawa na asilimia 6.1 ya madawati 25,773 yanayotarajiwa kuundwa katika shule zote nchini. Mikoa 12 iliyoanza kuunda madawati hayo ni Dar es Salaam (503), Shinyanga (243), Mwanza (97), Iringa (166), Tanga (155), Dodoma (75), Manyara (75), Geita (61), Rukwa (60), Arusha (50), Pwani (50) na Morogoro (50). Hadi Aprili, 2023 Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo mkoa pekee uliofanikiwa kuunda madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule zote za msingi na sekondari. Hivyo, nachukua fursa hii kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, Wizara inaandaa tuzo kwa ajili ya kuipongeza mikoa mitano (5) itakayofanya vizuri zaidi katika kuandaa jukwaa hili muhimu la ulinzi na usalama wa mtoto zitakazotolewa mwezi Juni, 2023.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kwamba Madawati hayo yanaundwa katika shule zote za Msingi na Sekondari; Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya uundaji wa madawati hayo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Elimu, Maafisa Ustawi wa Jamii na walimu wa ushauri na unasihi kwenye shule zote ili wakaunde madawati hayo. Aidha, Wizara itaendelea kushirikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na makundi mengine ya kujitolea kushirikiana na maafisa wa Serikali ili kusaidia katika zoezi hilo.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa haki ya watoto ya kushiriki katika kujadili masuala yanayowahusu, Wizara inaendelea kuhuisha na kuunda Mabaraza ya Watoto katika ngazi za Vijiji/Mitaa hadi ngazi ya Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya Mabaraza ya Watoto 592 yameanzishwa sawa na asilimia 3.6 ya lengo la kuanzisha Mabaraza 16,582. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeekeleza Maafisa Elimu na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri kuunda Mabaraza ya watoto 8,250 na kukamilisha ifikapo Juni, 2024. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia na kuratibu utendaji wa Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo linajumuisha wajumbe wawili (2) kutoka kila Mikoa katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na wajumbe 10 kutoka Zanzibar kwa kuzingatia uwiano wa jinsi. Pamoja na kuwashirikisha watoto kujadili masuala yanayowahusu, Mabaraza hayo hutoa fursa kwa watoto kujifunza masuala ya uongozi, uadilifu, uzalendo na maadili mema kwa Taifa na masuala mengine mtambuka ikiwa ni pamoja na masuala ya jinsia, mabadiliko ya tabia nchi, TEHAMA, VVU na UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeendelea kuelimisha na kufuatilia malezi na makuzi ya watoto ikiwa ni pamoja na usalama wa watoto wakiwa nyumbani, shuleni na kwenye jamii. Mfano, katika kipindi cha 2022/23 kwenye usafirishaji wa watoto katika baadhi ya mabasi ya shule yalibainishwa matukio mbalimbali ya ukatili kwa watoto ukiwemo ukatili wa kingono. Hatua za kisheria zimeendelea kuchukuliwa kwa waliotuhumiwa kufanya makosa ya ukatili dhidi ya Watoto. Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya matukio ya ukatili 15,901 yaliripotiwa Polisi. Aidha, sehemu kubwa ya jamii imekuwa ikioneana muhali kwenye kutoa ushahidi ili kesi itayarishwe vizuri kukidhi vigezo vya kufikishwa mahakamani. Hali hii inaathiri kasi ya haki kupatikana, mathalani kati ya matukio haya Kesi 671 ndiyo zilifikishwa mahakamani ambapo

kati ya hizo kesi 368 zilizotolewa hukumu na kesi 303 zinaendelea.

**51.** ***Mheshimiwa Spika****,* nitoe wito kwa jamii kuendelea kujitokeza mbele ya vyombo vya utoaji haki kutoa ushahidi ili kesi zote zilizopo kwenye mnyororo wa haki jinai ziweze kufika mwisho na haki ipatikane. Natoa pongezi kwa Jeshi la Polisi na mamlaka zingine za uchunguzi na maafisa wa Dawati la Jinsia katika taasisi mbalimbali ambao wamekuwa wakifanya kazi usiku na mchana kuwafikia watuhumiwa na kutoa faraja na huduma kwa manusura. Natoa rai kwa jamii kutoa ushirikiano kwa vyombo vyetu na ni vyema ifahamike endapo itabainika kuna watu wanaovuruga ushahidi watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto zinazoibuka za usalama wa watoto katika mabasi ya shule na kuimarisha malezi, makuzi na usalama wa watoto shuleni; Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa Waraka wa Elimu Na. 1 wa mwaka 2023 kuhusu uboreshaji wa huduma ya magari/mabasi yanayotumika kusafirisha wanafunzi ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa wahudumu wawili ambao ni mhudumu wa kike na wa kiume kwa kila gari mwanzo wa safari hadi mwisho; na inaposhindikana wote wawili; basi awepo mhudumu wa kike. Waraka huo pia umeelekeza kuacha kuweka muziki na video zisizo za maadili kwenye mabasi sambamba na kubandikwa kwa maelekezo ya kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya mtoto katika kila basi ili kuwakumbusha walimu, watumishi na jamii majukumu yao ya kuwalinda watoto.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imetoa Waraka wa Elimu Na. 2 wa mwaka 2023 ulioweka zuio la utoaji wa huduma ya kulaza wanafunzi wa bweni kwa ngazi za elimu ya awali hadi shule za msingi chini ya darasa la 5 **isipokuwa kwa kibali**

**maalum kutoka Ofisi ya Kamishna wa Elimu.** Waraka Na 1 na Waraka Na. 2 umeanza kutumika tarehe 01 Machi, 2023. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais TAMISEMI inakusudia kufanya tathmini ya utekelezaji wake ili kujiridhisha na utatuzi wa changamoto hizo.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika azma ya kuongeza uelewa na hamasa ya jamii kwenye ushiriki wa Malezi, Makuzi na Ulinzi wa watoto, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu Kampeni mbalimbali kuhamasisha jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwemo **"Twende Pamoja Ukatili Sasa Basi"** kampeni ambayo ilizinduliwa mwaka 2019 ikilenga kujumuisha makundi yote ya jamii katika kupambana na vitendo vya ukatili na Kampeni ya **Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA)** ambayo ni kampeni ya Wananchi Wazalendo waliojitolea kuelimisha jamii na kuibua changamoto za ukatili ili hatua stahiki zichukuliwe na mamlaka husika. Kampeni hii ilianza Julai, 2022 na inaendeshwa chini ya kaulimbiu ya **"Kataa Ukatili, Wewe ni Shujaa"**.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya wananchi 9,832 wamejiunga katika kampeni hiyo na kufanikiwa kutoa elimu kuhusu madhara ya ukatili dhidi ya watoto ikijumuisha yafuatayo: mikusanyiko na mikutano matukio (550), magulio na masoko (126), makanisa na misikiti (232), zahanati na vituo vya afya (50), vyombo vya habari (39), maonyesho (10), shule na vyuo vikuu (481). Vilevile, elimu ya ukatili dhidi ya watoto na usawa wa kijinsia imetolewa kwenye vituo vya basi na maegesho ya magari (56). Hivyo, kampeni imefikia Kata 1,000, Halmashauri 156 na Mikoa yote 26 ya Tanzania. Kupitia mitandao ya kijamii, kampeni ya SMAUJATA imepata wafuatiliaji wengi katika vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na jamii.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** tangu Kampeni ya SMAUJATA kuasisiwa kwa takribani mwaka mmoja sasa; tarehe 27 Mei 2023

utakuwa ni usiku wa kutathmini utendaji na mafanikio ya SMAUJATA kwa utendaji wake na kutoa tuzo kwa mashujaa hao inayojulikana kama **"SMAUJATA CHAMPIONS AWARD, 2023"**. Utendaji wa SMAUJATA umeamsha ari ya watanzania wengine wazalendo kuanzisha vikundi vipya vya kuunga mkono ajenda hii vikiwemo taasisi ya *Safe Society Platform Tanzania* iliyopo Mkoa wa Mara na Foundation for Ambassadors Gender Initiatives (FAGDI) yenye Kampeni yenye kaulimbiu ya **"Zijue Fursa, Imarisha Uchumi, Kataa Ukatili, Kazi Iendelee - ZIFIUKUKI"**. Kampeni hii ilizinduliwa kwa mafanikio makubwa mwezi Aprili, 2023 katika Mkoa wa Dar es Salaam ikihusisha Wahariri wa vyombo ya habari, Viongozi wa dini, Baraza la Wazee, Machifu na Wananchi kwa ujumla. Mwelekeo wa Wizara ni kuimarisha falsafa ya kuhamasisha utendaji shirikishi na jamii katika ngazi za msingi (Bottom Up) kwenye maeneo yote ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na jamii kumiliki Kampeni ya kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na kuelimisha juu ya fursa za kiuchumi. Nachukua fursa hii kuwapongeza viongozi wa SMAUJATA, SSPT, FAGDI na wengine wote wanaofanya kazi za jamii kwa dhana ya kujitolea muda na rasilimali zao kuenzi Taifa lao. Natoa wito kwa vikundi vingine vyote vyenye moyo wa kujitoa kushirikiana na Wizara.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ongezeko la vitendo vya mmomonyoko wa maadili katika jamii, tarehe 15 Mei, 2023 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Familia, Wizara imezindua Kampeni mahsusi inayohusisha wadau mbalimbali ili kulinda maadili, mila, desturi na tamaduni zetu. Kampeni hii inaongozwa na kaulimbiu **"Taifa Letu, Maadili Yetu".**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhusisha Wadau wenye ushawishi mkubwa kwa jamii katika kuimarisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia. Miongoni mwa wadau hao ni Klabu za Mpira wa Miguu ambapo tayari YANGA na AZAM wameunga mkono vita hii na wengine wanaendelea kujitokeza. Kwa

upande mwingine, tunatambua mchango mkubwa wa vyombo mbalimbali vya habari ambavyo vimekuwa mstari wa mbele wakati wote kufikisha sauti ya elimu kwa wananchi na wito kuingia kwenye vita hii. Aidha, Tunawapongeza sana wadau hawa na wengine wote wanaoguswa na maombi yetu ya kuungana kwenye vita hivi. Wito unatolewa kwa vilabu vingine vyote vya michezo na vyombo vya habari na kila mdau mmoja mmoja mwenye nguvu ya sauti kwenye jamii na wafuasi wengi kujitolea kuingia kwenye mapambano haya ya kulinda vizazi na Taifa letu dhidi ya mmomonyoko wa maadili, ukatili wa kijinsia na pia kuwajulisha wananchi fursa za maendeleo ya kiuchumi.

***59. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu huduma ya msaada wa simu bila malipo Na. 116 (*Child Helpline*) kwa ajili ya jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 jumla ya simu 11,316 kuhusu watoto zilipokelewa na kati ya simu hizo 10,777 zilikuwa na lengo la wazazi/walezi na watoto kupata elimu inayohusu masuala mbalimbali ya malezi. Katika eneo la ukatili, simu 539 zilihusu ukatili na utelekezaji wa watoto ambazo 81 zilipewa rufaa kwa Maafisa Ustawi wa Jamii na Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo mbalimbali vya Polisi nchini. Aidha, katika kupanua wigo wa kupokea changamoto za jamii ikiwa ni pamoja na ukatili dhidi ya makundi mbalimbali hususani Wanawake na Watoto; Wizara imeanzisha "call center" ambayo itaanza kutumika Juni, 2023. Vilevile, wananchi takribani 342 walifikisha malalamiko yao kwa kunitumia ujumbe wa simu kupitia namba yangu ya **0734124191 na 0765345777** ambapo niliwaunganisha na maafisa ustawi wa mikoa kwa huduma stahiki kama inavyoonekana kwenye **kiambatisho Na 1.**

***Nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Dawati la Jinsia Polisi kwa mchango wao***

***mkubwa wanaoutoa katika kushughulikia vitendo hivi hususan katika kutoa huduma kwa manusura wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Aidha, natoa wito kwa viongozi na watendaji wote kuendelea kuwa karibu na wananchi ili wapate huduma zote ngazi stahiki na kuepuka kuhitaji rufaa hata kwa masuala yenye ufumbuzi kwa ngazi husika.***

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa haki za watoto kisheria, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, Wizara za Kisekta na Taasisi za Kiserikali ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, imeratibu ukusanyaji wa maoni ya marekebisho ya Sheria ya Mtoto Sura ya. 13 ya Sheria za Tanzania sambamba na kufanya uchambuzi na hatimaye kupendekeza vifungu vinavyopaswa kufanyiwa marekebisho. Hatua inayofuata ni Wadau wote kutolea maoni mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo ili hatua zinazofuata ziweze kuendelea kwa lengo la marekebisho ya Sheria hiyo ili kuondoa changamoto za utoaji haki kwa watoto. Aidha, Wizara yangu kwa kipekee inatambua juhudi inayoendelea kufanywa na Wizara ya Katiba na Sheria katika mchakato mzima wa kufanya marekebisho ya sheria 29 zikiwemo Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria ya Ushahidi, Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi na Kanuni ya Adhabu ambazo marekebisho yake pamoja na mambo mengine yataimarisha ulinzi wa watoto, wanawake na jamii kwa ujumla.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa sasa tumeanza kushuhudia ukatili mpya wa watoto katika mitandao. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Ukatili wa Watoto Mtandaoni (Disrupting Harm Report in Tanzania – 2022) inaonesha kuwa asilimia 67 ya watoto wenye

umri wa miaka 12 – 17 hapa nchini ni watumiaji wa mitandao kwa kutumia simu na kompyuta ambazo huzipata kwa ndugu zao wa karibu wakiwemo wazazi, walezi, marafiki na ndugu wengine wanaowazunguka. Taarifa hiyo imeonesha pia kwamba asilimia 4 ya watoto waliotumia mitandao ni wahanga wa aina mojawapo ya ukatili mtandaoni ikiwa ni pamoja na kulazimishwa kujihusisha na vitendo vya ngono, kusambaza picha na video zenye maudhui ya kingono bila ridhaa yao na kurubuniwa kujihusisha na shughuli za kingono kwa kuahidiwa fedha au zawadi zingine.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uelewa wa athari za ukatili kwa watoto mtandaoni zinazotokana na matumizi yasiyo sahihi ya vifaa vya kieletroniki kama simu, kompyuta na runinga, Wizara imeandaa Vijarida vya kuelimisha watoto, wazazi na walimu kwa kutumia lugha nyepesi. Lengo ni kuhakikisha kuwa wazazi na walimu wanakuwa wasaidizi wa watoto ili kubaki salama mtandaoni. Aidha, Vijarida hivyo vitakuwa msaada mkubwa kwa watoto wanapokuwa mitandaoni. Kwa sasa Vijarida hivyo vinasambazwa kwa walengwa kwa njia tofauti ikiwa ni pamoja na kuvifikisha shule za msingi na sekondari nchini na kutumia wamiliki wa mitandao "bloggers". Vilevile, Vijarida hivi vimewekwa katika tovuti na mitandao ya kijamii ya Wizara ili kuweza kupatikana kiurahisi kwa watumiaji mbalimbali. Zoezi la kusambaza linaendelea.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kupitia Bunge lako Tukufu kwa kutoa maelekezo kuhusu marekebisho ya sheria za makosa ya jinai katika kuimarisha juhudi za kupambana na mmomonyoko wa maadili. Kipekee, namshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa maelekezo ya namna ya kushughulikia masuala ya mmomonyoko wa maadili nchini ambapo Wizara yangu imeanza kuyatekeleza.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutoa elimu kuhusu mila na desturi zenye madhara katika jamii. Pamoja na elimu hiyo, bado kuna baadhi ya jamii zinazoendeleza mila ya ukeketaji katika mikoa mbalimbali nchini. Kwa mujibu wa Taarifa ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya mwaka 2015/2016, mikoa yenye kiwango cha juu cha ukeketaji ilikuwa ni Manyara (58%), Dodoma (47%), Arusha (41%), Mara (32%) na Singida (31%).

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Kampeni ya kutoa elimu na ushawishi kwa makundi mbalimbali kuhusu kutokomeza ukeketaji imefanyika kwenye Mikoa minne (4) ya Manyara, Dodoma, Arusha na Singida. Kampeni hiyo imewafikia Maafisa wa Serikali ngazi za Mikoa na Halmashauri 385, shule za msingi 89 na sekondari 26, viongozi wa jadi 109, viongozi wa dini 98, watu mashuhuri 71, mangariba 40 na wawakilishi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 193. Katika kampeni hiyo, elimu ilitolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya hadhara, kutembelea na kutoa elimu kwa wanafunzi kwenye shule za msingi na sekondari pamoja na mijadala iliyohusisha makundi mbalimbali ya jamii. Vilevile, wataalam wa masuala ya afya na ukatili dhidi ya watoto walitembelea shule 25 za msingi kwenye Halmashauri za Mkoa wa Mara (Tarime, Butiama na Serengeti) na kutoa elimu kwa wanafunzi 14,897. Aidha, katika kuzuia vitendo vya ukeketaji visitokee, jumla ya watoto wa kike 806 kutoka Halmashauri za Tarime (486), Serengeti (201) na Butiama (119) waliokolewa na kutunzwa kwenye nyumba salama zilizopo katika Halmashauri husika.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi za Serikali na Wadau kuwatunza watoto ambao walikuwa wanakabiliwa na uwezekano wa kukeketwa katika kipindi cha ukeketaji, ilipofika Februari, 2023 ikiaminika kwamba kipindi cha ukeketaji kimepita kwa mujibu wa mila na desturi, jumla ya Watoto 71 katika

Wilaya ya Tarime walikeketwa. Napenda kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza **Mhe. Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee**, Mkuu wa Mkoa wa Mara kwa hatua ya kukemea tukio hilo pamoja na kuwakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria wazazi/walezi 51 ambao wameshiriki katika kuwakeketa watoto hao waliporejea majumbani. Ni matumaini yangu kuwa, hatua kama hizi zitaendelea kuchukuliwa kwa wazazi na familia zinazojihusisha na ukeketaji katika kutokomeza jambo hili.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kushughulikia changamoto za kundi la Vijana Balehe nchini, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa **Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza kwenye Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe Nchini yaani NAIA (2021/22 – 2024/25)** ambapo kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na Taasisi za Serikali imeandaa Mwongozo wa Uratibu wa Ajenda hiyo na kufanikiwa kuunda kamati za kitaifa na kuzijengea uwezo zenye jumla ya wajumbe 125 zikiwemo:- Sekretarieti ya Taifa yenye wajumbe 27, Kamati Tendaji ya Taifa (40), Kamati Elekezi ya Taifa (46) na Kamati ya Usimamizi na Ufuatiliaji (12).

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika uratibu wa usimamizi wa utekelezaji wa Ajenda hiyo hapa, wizara na wadau wake tumetekeleza afua za utoaji elimu ya afya ya uzazi, hedhi salama na kuwapa mafunzo wasichana kuhusu ujasiriamali ili waweze kutekeleza shughuli zao za kiuchumi. Katika programu hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Mashirika ya *Plan International, World Vision na Femina* imefikia jumla ya Wasichana Balehe 11,480 ambapo wasichana 5,152 walitoka Dar es Salaam, 2,354 (Pwani), 3,143 (Katavi), 1,907 (Tabora), 2,189 (Kagera), 1,897 (Mara) na 1,278 (Dodoma). Mafunzo haya yamewezesha wasichana balehe kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi na hivyo kuweza kujiajiri na kupunguza kiwango cha utegemezi katika familia. Katika kupima utekelezaji wa ajenda hiyo, Wizara inaandaa tathmini ya kati ya utekelezaji ya ajenda ya Taifa ya

Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe kwa lengo la kuainisha mafanikio, changamoto na kuboresha utekelezaji wake.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia jukumu la uratibu, Wizara imeshirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ufadhili wa Mfuko wa Kimataifa wa UKIMWI (Global Fund) kutekeleza Mradi wa Kutokomeza maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI kwa Vijana Balehe wenye umri wa kati ya miaka 10 hadi 24 unaojulikana kama "Timiza Malengo". Mradi huo umetekelezwa katika Halmashauri 18 kwenye mikoa mitano (5) ya Dodoma, Morogoro, Singida, Tanga na Geita ambapo jumla ya vijana balehe milioni moja waliopo shuleni na nje ya shule wamefikiwa na programu hiyo. Kati ya hao, Vijana Balehe 941,000 walifikiwa na elimu ya afya ya uzazi na VVU sambamba na vifaa mbalimbali vya shule ili waweze kukamilisha mzunguko wa elimu yao. Katika hao, jumla ya wasichana balehe 426,000 waliopo nje ya mfumo rasmi wa elimu walipata elimu ya ujasiriamali ambapo, wasichana 41,000 walipewa fedha taslimu Shilingi 257,000 kila mmoja ukiwa ni mtaji wa kuanzisha shughuli za kujipatia kipato kwenye Halmashauri zote 18 za mradi.

**70**. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inaendelea kuratibu **Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto 2021/22 - 2025/26** yenye lengo la kutatua changamoto za ukuaji na maendeleo ya watoto wenye umri kati ya miaka 0 hadi 8. Katika kuimarisha uelewa na umuhimu wa kuwekeza katika huduma jumuishi za Afya, lishe, ulinzi, ujifunzaji wa awali, malezi yenye mwitikio na uchangamshi wa awali kwa watoto kwenye utekelezaji wa Programu hiyo, mwezi Novemba, 2022, Wizara iliratibu mafunzo kuhusu sayansi ya malezi na makuzi ya watoto kwa wajumbe 124 wa Kamati za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zikiwemo Kamati ya Bajeti, Kamati ya Utawala na Serikali za

Mitaa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya bunge ya Maendeleo na Huduma za Jamii.

**71**. ***Mheshimiwa Spika**,* katika kuimarisha malezi jumuishi kwa kundi la vijana balehe wenye umri wa miaka 10 hadi 17; Wizara imeanzisha programu ya malezi kwa kufanya majaribio ya programu Jumuishi ya Malezi kwenye Halmashauri ya Mbarali Mkoani Mbeya mwaka 2022. Utekelezaji wa Programu ulianza kwa kutoa mafunzo kuhusu programu kwa wawezeshaji 16 ambao walipewa jukumu la kutoa elimu ya malezi kwa Wazazi ikijumuisha na Vijana Balehe kwa pamoja. Jumla ya wazazi 104 na Vijana Balehe 83 kutoka katika Kata 8 za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambazo Ruiwa, Ubaruku, Rujewa, Utengule, Ihahi, Chimala, Lugelele na Madibira walipata mafunzo hayo. Awamu ya pili ya programu hiyo imeanza kutekelezwa katika Halmashauri tatu za mkoa wa Songwe ambazo ni Mbozi, Ileje na Tunduma. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara itatekeleza programu hiyo katika Halmashauri zote za mikoa ya Kigoma, Mtwara, Iringa, Mbeya na Njombe. Tathmini ya majaribio hayo imeonesha kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuanza kutoa elimu ya malezi na matunzo ya watoto kwa vijana ili waweze kumudu utoaji wa huduma hiyo kwa watoto wao wakati ukiwadia.
***Nitumie fursa hii, kutoa rai kwa Watanzania wote kuwa mstari wa mbele katika kutokomeza vitendo vyote vya ukatili dhidi ya watoto vinavyotokea nyumbani kwa 60%, ndani na nje ya shule kwa 40%. Hili litawezekana endapo wazazi na walezi watatimiza jukumu lao la msingi la malezi na makuzi ya watoto kwa kuhakikisha wanatenga muda wa kuwa karibu na watoto wao ili kujua changamoto zinazowakabili. Aidha, wazazi wafuatilie mienendo ya watoto wao na kutoa taarifa za viashiria vya ukatili na vitendo vya ukatili vinavyowapata watoto mapema ili mamlaka husika kuchukua hatua kwa wakati. Watoto ni tunu muhimu kwa Taifa letu, tuwalinde ili wakue na kufikia utimilifu wao.***

**ENEO LA 4: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutoa huduma za ustawi wa jamii hapa nchini zikiwemo haki, matunzo na ulinzi kwa wazee, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, watoto walio katika mkinzano na sheria, huduma kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu, huduma za msaada wa kisaikolojia katika jamii, uratibu wa huduma za afya kwa makundi maalum, huduma kwa familia duni, usajili na usimamizi wa makao na vituo na makao ya kulelea watoto nchini, uratibu wa huduma za malezi ya kambo na kuasili na utatuzi wa migogoro ya familia na ndoa. Majukumu haya yanatekelezwa na wataalam wa ustawi wa jamii kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mahsusi inayoongoza utoaji wa huduma za ustawi wa jamii nchini.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia utoaji wa huduma katika Mahabusu 5 za watoto zilizopo mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Mahabusu hizo zinatoa huduma za msingi ikiwa ni pamoja na huduma za sheria kwa watoto walio katika mkinzano na sheria. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, watoto 267 (Ke 23 na Me 244) walio katika mkinzano na sheria waliwezeshwa kupata huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu. Aidha, jumla ya watoto 482 (Me 459, Ke 23) waliokinzana na sheria walipatiwa huduma za ustawi wa jamii katika mashauri yao mahakamani katika Halmashauri zote nchini.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka mpya ujao wa fedha, Wizara itazindua mahabusu mkoani Mtwara yenye uwezo wa kuhudumia watoto 60 kwa wakati mmoja. Mahabusu hii itahudumia mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma ambayo haikuwa na mahabusu ya watoto. Aidha, Wizara inasimamia

shule ya maadilisho Irambo Mbeya yenye watoto 41 (Me 40 na Ke 1) waliohukumiwa na mahakama baada ya kutenda makosa mbalimbali. Kati ya Julai 2022 na Aprili 2023, watoto 12 (Me 11, Ke 1) waliokuwa wanatumikia hukumu ya marekebisho ya tabia wamekamilisha hukumu zao na kuunganishwa na familia zao. Shule hii inatoa marekebisho ya tabia na elimu kwa watoto waliothibitishwa kutenda makosa ya jinai ili wanapokamilisha hukumu zao waweze kuwa raia wema.

***Natoa wito kwa jamii kuendelea kuwatumia wataalamu wa Ustawi wa Jamii katika ngazi zote pale wanapobaini mienendo mibaya ya tabia ya watoto katika maeneo wanayoishi ili wafanye ufuatiliaji kabla ya watoto hao kuingia katika hatari za kukinzana na sheria.***

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na utambuzi wa Watoto walio katika mazingira hatarishi kupitia Serikali za Mitaa katika Halmashauri zote ambao unawezesha kuwasajili na kuwapa huduma watoto hao pamoja na kaya zao. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya watoto 335,971 (Me 168,634, Ke 167,337) walio katika mazingira hatarishi wametambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali ikijumuisha chakula, malazi, mavazi, elimu, matibabu na lishe. Kati ya hao, watoto 26,000 waliotelekezwa, manusura wa vitendo vya ukatili, wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu na wanaoishi kwenye makao ya watoto wameunganishwa na familia zao ili kuwahakikishia malezi, matunzo na ulinzi. Wizara itaongeza kasi ya kuwatambua watoto wa kundi hili na kaya zao ili kufikisha huduma za ustawi na kwa kushirikiana na jamii kudhibiti utoro wa watoto kwenda mitaani kwa kuchukua hatua stahiki kulingana na tathmini ya mazingira hayo.

**76.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani limepungua kwa asilimia 38. Hata hivyo tatizo hilo bado

linaendelea kuwepo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo umaskini, vitendo vya ukatili ndani ya familia, migogoro ya ndoa na familia, mila na desturi zisizofaa na malezi duni.
Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 jumla ya watoto 2,185 (Me 1,324, Ke 861) wameunganishwa na familia zao na wengine kupatiwa stadi za maisha katika vyuo vya ufundi stadi nchini. Hii ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na Wizara yangu.

***Nitoe rai kwa wazazi, walezi na jamii kuwajibika katika malezi, makuzi, matunzo na ulinzi wa watoto ili kuwezesha familia kuwa sehemu salama kwa watoto kuishi na kufurahia haki zao. Hatua kali za kisheria zitaendelea kuchukuliwa kwa mzazi au mlezi yoyote atakayebainika kusababisha mtoto kuingia mtaani ikiwemo kifungo kama ilivyo katika Kifungu cha 16 na 17 cha Sheria ya Mtoto Sura ya 13.***

***Aidha, iwapo mzazi anaona mtoto wake ana changamoto ambazo yeye ameshindwa kukabiliana nazo, badala ya kumwacha akimbilie mtaani atoe taarifa mapema ili tathmini ifanyike na hatua stahiki zichukuliwe. Vinginevyo, mtoto akitoweka nyumbani vema wazazi na walezi watoe taarifa kwenye kituo cha Polisi na Viongozi wa Serikali za Mitaa badala ya kukaa kimya. Hatua zitachukuliwa dhidi yao kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Sura ya 13.***

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, huduma za malezi ya kambo na Kuasili zimeendelea kutolewa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Malezi ya kambo ni malezi mbadala ya kisheria yanayoruhusiwa kwa mlezi mbadala kwa muda maalum. Aidha, kuasili ni kumchukua mtoto kisheria na kumfanya kuwa wako ili kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika ngazi ya familia kulingana na Sheria ya Mtoto Sura ya 13. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya watoto 75 miongoni mwao watoto 41 (Ke 19 na Me 22) walipata huduma ya malezi

ya kambo na watoto 34 (Ke 18 na Me 16) walipata huduma ya kuasili ili kuwawezesha kupata malezi katika ngazi ya familia. ***Natoa wito kwa jamii na watu wenye moyo wa kutoa huduma ya malezi ya kambo na kuasili watoto kujitokeza ili watoto waliokosa malezi ya familia waweze kulelewa katika ngazi ya familia.***

**78.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kusajili, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwenye makao ya Watoto ikiwemo malazi, chakula, malezi mbadala, huduma za kiroho, matunzo, ulinzi, afya na elimu kwa watoto walio katika mazingira hatarishi nchini. Malezi katika Makao ya Watoto ni huduma ya muda mfupi wakati mashauri ya watoto husika yakifanyiwa kazi ili waunganishwe na familia zao au kupatiwa huduma za malezi mbadala. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili, 2023, leseni 28 za usajili wa Makao yenye watoto 736 (Me 337, Ke 399) zilitolewa katika mikoa ya Dar es Salaam (7), Njombe (2), Arusha (3), Tabora (2), Manyara (1), Iringa (2), Pwani (3), Dodoma (1), Mara (1), Simiyu (1), Tanga (3) na Morogoro (2). Hivyo, kufikia jumla ya Makao 333 yaliyosajiliwa nchini yanayohudumia watoto 12,077 (Me 6,050, Ke 6,027).

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, imeanza kuratibu utoaji wa mafunzo ya Taaluma za Ustawi wa Jamii na Malezi ya Watoto Wadogo kwa vyuo binafsi kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa kutumia mitaala ya Wizara. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya vyuo 93 vimetambuliwa ambapo 45 vinatoa mafunzo ya taaluma ya ustawi wa jamii na 48 vinatoa mafunzo kwa walezi wa watoto. Uratibu wa vyuo unalenga kuimarisha umahiri na weledi wa wataalam wanaotoa huduma za ustawi wa jamii na malezi ya watoto nchini.

***Nitoe rai kwa wamiliki na waendeshaji wa mafunzo ya taaluma ya ustawi wa jamii na mafunzo kwa walezi wa watoto wadogo kuendelea kufuata sheria, kanuni na miongozo ya uendeshaji***

***na utoaji wa mafunzo ili kupata wahitimu wenye umahiri na weledi wa kuhudumia jamii.***

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, inaendelea kuratibu huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Ofisi za Ustawi wa Jamii ngazi za Halmashauri nchini. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya mashauri 28,773 yalipokelewa ambapo mashauri 22,844 yalifanyiwa usuluhishi katika Mabaraza ya Usuluhishi na Ofisi za Ustawi wa Jamii, kati ya hayo, mashauri 5,929 yalipewa rufaa kwenda mahamakani. Katika kipindi hicho Migogoro hiyo imeshuka kwa 27% ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita kutokana na jitihada zinazoendelea kufanywa na Wizara, Maafisa Ustawi wa Jamii, wadau, Mabaraza ya Usuluhuhishi wa migogoro ya ndoa na vyombo vya Habari, kutoa elimu ya athari ya Migogoro ya ndoa katika familia na jamii kwa ujumla.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** vyanzo vikuu vya migogoro ya ndoa vilivyobainishwa ni pamoja na mawasiliano hafifu ya wanandoa, umaskini, wanandoa kutokujua wajibu wao, mila na desturi zisizofaa, ndoa za utotoni na mmomonyoko wa maadili yanayosababisha mifarakano kwenye ndoa, malezi duni na kutowajibika kwenye matunzo ya watoto. Hivyo, huduma ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia huzingatia malezi, matunzo na ulinzi wa watoto ili kuepusha madhara ya ukosefu wa haki za watoto katika jamii. Aidha, watoto 18,922 waliobainika kuathiriwa na migogoro ya ndoa baada ya mashauri kukamilika, walipatiwa matunzo kutoka kwa wazazi wao. Naipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuongoza mchakato wa mapitio ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 yatakayosaidia kulinda ustawi wa watoto na familia.

***Nitoe rai kwa wanandoa kutafuta suluhu ya mapema kufika katika vyombo vya usuluhishi na upatanishi ikiwemo ofisi za***

***Ustawi wa Jamii pale ambapo kuna dalili za mifarakano ili kuzuia migogoro au kuvunjika kwa familia*.**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, inaendelea kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa makundi yenye mahitaji maalum ikijumuisha wazee, wahanga wa ukatili na jamii zinazoathiriwa na majanga mbalimbali ili kuwarejesha katika hali njema ya kisaikolojia waweze kutekeleza shughuli za ujenzi wa Taifa. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili 2023 huduma imetolewa kupitia Ofisi za Ustawi wa Jamii katika Halmashauri zote kwa wahanga wa vitendo vya ukatili 13,926 ambapo wanawake walikuwa 7,142 na watoto 6,784. Pia, wahanga wa vitendo vya ukatili na usafirishaji haramu wa binadamu walikuwa 452 (Me 05, Ke 447). Vilevile, ili kuhakikisha watoa huduma za Ustawi wa Jamii nchini wanazingatia weledi na miiko ya kazi zao, Wizara inaratibu kutungwa kwa Sheria ya Wataalam Wanaotoa Huduma za Ustawi wa Jamii (Social Welfare Services Practitioners Act).

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia wataalamu wa ustawi wa jamii ilitoa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa manusura 26 wa ajali ya ndege ya *Precision Air* iliyotokea tarehe 06 Novemba, 2022 na waathiriwa 1,208 wa ugonjwa wa *Marburg* katika Mkoa wa Kagera ambapo watu wazima walikuwa 321 (Me 104, Ke 217) na watoto 887 (Me 387, Ke 500). Huduma hiyo ililenga kuondoa hofu kwa manusura na waathiriwa wa majanga ili waweze kurejea katika hali njema kisaikolojia. Vilevile, kuzuia unyanyapaa kwa familia na jamii na kuwajengea uwezo wa kuwasaidia kupona ili waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji mali sambamba na kujikinga dhidi ya maambukizi mapya.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, Wizara ilifanikiwa kutoa elimu kwa Wadau 1,050 kuhusu huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii na maeneo

zinakopatikana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani yaliyofanyika Mwezi Oktoba, 2022. Vilevile, Jumla ya Wataalam 1,850 kutoka Halmashauri 73, wamejengewa uwezo kuhusu utoaji wa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii katika maeneo yao.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, inaendelea kutoa na kuratibu utoaji wa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza na wasiokuwa na mtu wa kuwahudumia katika makazi 14 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali na makazi 15 yanayomilikiwa na Taasisi na watu binafsi. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili 2023, wazee wasiojiweza 259 (Ke 102, Me 157) wanahudumiwa katika makazi ya Wazee ya Serikali na Wazee 268 (Ke 150 na Me 118) wanahudumiwa katika makazi ya wazee yanayosimamiwa na Taasisi na watu binafsi kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Wahudumiwa katika Makazi ya Wazee yanayomilikiwa na Serikali katika kipindi cha Julai 2022 - Aprili, 2023.**

| Na. | Makazi | Mkoa | Idadi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | |
| 1 | Kibirizi | Kigoma | 14 | 9 | 23 |
| 2 | Njoro | Kilimanjaro | 11 | 5 | 16 |
| 3 | Kolandoto | Shinyanga | 13 | 4 | 17 |
| 4 | Bukumbi | Mwanza | 9 | 18 | 27 |
| 5 | Ipuli | Tabora | 15 | 11 | 26 |
| 6 | Fungafunga | Morogoro | 17 | 6 | 23 |
| 7 | Mwanzange | Tanga | 12 | 4 | 16 |
| **Na.** | **Makazi** | **Mkoa** | **Idadi** | | **Jumla** |

| | | | Me | Ke | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Nunge | DSM | 13 | 10 | 23 |
| 9 | Magugu | Manyara | 4 | 2 | 6 |
| 10 | Misufini | Tanga | 11 | 4 | 15 |
| 11 | Nyabange | Mara | 7 | 10 | 17 |
| 12 | Kilima | Kagera | 09 | 4 | 13 |
| 13 | Sukamahela | Singida | 12 | 3 | 15 |
| 14 | Nandanga | Lindi | 10 | 12 | 22 |
| | **JUMLA** | | **157** | **102** | **259** |

***Chanzo: WMJJWM, 2023***

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya imeendelea kuhakikisha wazee wanapata huduma za afya kwa wakati, kwa kufanya utambuzi na tathmini ya wazee wasiojiweza ambapo wazee 585,672 (Me 255,496 na Ke 330,176) wamepatiwa vitambulisho maalum na kukatiwa bima za afya kwa ajili ya matibabu. Vilevile, ili kuhakikisha wazee wanapewa kipaumbele cha matibabu katika vituo vya kutolea huduma za afya, Serikali imeendelea kuimarisha utaratibu wa utoaji huduma za matibabu kwa wazee kupitia kampeni kabambe ya "MPISHE MZEE KWANZA" kutoa kipaumbele kwa wazee ngazi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa, kanda na taifa. Aidha, Wizara inakamilisha Mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 ili kuendana na mahitaji ya wazee kwa kipindi hiki.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kushirikiana na Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee, Taasisi na asasi za kiraia zinazoshughulika na wazee katika kutatua changamoto na kuleta ustawi na maendeleo ya Wazee nchini. Asasi za kiraia zinazoshughulika na Wazee ni pamoja na Chama cha Wazee

Wanaume Tanzania, Umoja wa Wastaafu Tanzania (REAT), *Help Age* Tanzania, REDESO, *TOP Elderly* Tanzania, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Mashirika ya Hifadhi ya Jamii.

**88.** ***Mheshimiwa Spika**,* pamoja na juhudi za Serikali za utoaji wa huduma za ustawi wa jamii zinazofanywa na Maafisa wa Ustawi wa Jamii nchini, bado tunakabiliana na changamoto ya upungufu wa Maafisa 20,057 ambayo ni sawa na asilimia 95.3 ya Maafisa wanaotakiwa kuanzia ngazi ya mkoa mpaka ngazi ya Kijiji/Mtaa kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3: Idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika Ngazi Mbalimbali**

| Na. | Ngazi | Maafisa Wanaohitajika | Maafisa Waliopo | | Upungufu | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % | Idadi | % |
| 1. | Mkoa | 26 | 26 | 100 | 0 | - |
| 2. | Hospitali za Rufaa za Mikoa | 157 | 42 | 26.8 | 115 | 73.2 |
| 3. | Halmashauri | 1,454 | 535 | 36.8 | 919 | 63.2 |
| 4. | Hospitali za Wilaya | 384 | 156 | 40.6 | 228 | 59.4 |
| 5. | Kata/Vituo vya Afya | 4,461 | 225 | 5.0 | 4,236 | 95.0 |
| 6. | Mtaa/Kijiji / Zahanati | 14,600 | 1 | 0.01 | 14,559 | 99.99 |
| | **Jumla** | **21,082** | **996** | **4.7** | **20,057** | **95.3** |

***Chanzo: WMJJWM, 2023***

89. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za ajira inaendelea kushughulikia changamoto ya upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii. Aidha, Wizara inahimiza taasisi binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, taasisi za elimu, makampuni, viwanda, migodi na waajiri wengine kuona umuhimu wa kuajiri na kuwatumia Maafisa Ustawi wa Jamii katika kutatua changomoto za kijamii kwenye maeneo ya kazi.

## ENEO LA 5: MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kukuza usawa na uwezeshaji wanawake, inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi chenye Usawa 2021/22 – 2025/26 (Generation Equality Forum Commitments) ambalo Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Kinara wa utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa Kiuchumi kwa Wanawake.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa programu hiyo unajumuisha afua za kuanzisha na kuendeleza vituo vya malezi na makuzi ya watoto; kuongeza uwekezaji katika usambazaji wa maji, umeme na nishati mbadala yenye kutunza mazingira na matumizi ya teknolojia yenye gharama nafuu na inayofaa katika kutatua changamoto za majukumu mengi kwa wanawake katika maeneo ya vijijini na mijini; kuongeza kazi zenye staha kwa kuendeleza biashara na urasimishaji wa biashara za wanawake; na kuboresha upatikanaji na matumizi ya teknolojia nafuu na zinazofaa ili kuongeza uwezo wa wanawake wa kuzalisha bidhaa zenye ushindani wa soko la ndani na nje.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** afua nyingine za programu hii ni pamoja na kuongeza uwekezaji katika programu za elimu kwa wasichana; kuimarisha afua zinazoongeza ushiriki wa

wanawake na wasichana katika kumiliki, kusimamia na kufaidika na ardhi na rasilimali nyingine za uzalishaji; kuongeza huduma jumuishi za fedha; kuongeza matumizi ya teknolojia ya kidijitali ili kuongeza ushindani katika uzalishaji na biashara kwa wanawake; na kuongeza wigo wa utoaji wa huduma kwa familia kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa unafanyika sambamba na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000 inayofanyiwa mapitio, Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22 - 2025/26) na Mfumo Jumuishi wa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi (2017). Programu na mfumo huo vinalenga kuleta usawa wa kijinsia, kuongeza fursa za kiuchumi kwa wanawake na kuimarisha malezi na makuzi ya watoto kwa ustawi na maendeleo ya familia na Taifa kwa ujumla.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa programu hii unahusisha Wizara za Kisekta, Taasisi za Umma na Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Wadau wengine. Aidha, **Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Masuala ya** K**izazi chenye Usawa** chini ya Uenyekiti wa **Mhe. Angellah Kairuki (Mb)** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kushauri utekelezaji wa Programu hii kwa tija na ufanisi. Vilevile, katika kuratibu utekelezaji wa Programu hii, **wameteuliwa Maafisa Dawati wabobezi 24** kutoka Wizara za Kisekta na wengine sita (6) kutoka katika Taasisi na Mamlaka za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Vilevile, umeandaliwa Mkakati wa Mawasiliano wa Programu ambao utawezesha kuongeza uelewa na ushiriki wa jamii na wadau katika utekelezaji wa Programu. Sambamba na mkakati

huu wa mawasiliano, umeandaliwa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Matokeo ya Utekelezaji wa Programu (Monitoring and Evaluation Result Framework) utakaowezesha katika ufuatiliaji wa karibu wa afua zilizoainishwa na programu.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto kwa ustawi wa watoto na familia, Wizara kupitia Programu ya Kizazi Chenye Usawa imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vituo vya malezi na makuzi ya awali ya mtoto ambavyo vinasaidia kutoa huduma ya uchangamshi wa awali inayowasaidia watoto kukua kimwili, kiakili, kiafya, kihisia na kimaadili. Aidha, vituo hivi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha ulinzi wa watoto wakati wazazi na walezi wao wakijihusisha na shughuli za kiuchumi. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 jumla ya vituo 148 vya kulelea watoto mchana vimeanzishwa na kufikia jumla ya vituo 2,833 vyenye watoto 175,039 (Ke 91,842 na Me 83,197). Vilevile, Wizara imeratibu uanzishwaji wa vituo 200 vya kijamii vya malezi na makuzi ya watoto na kufanya jumla ya vituo kuwa 3,033.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika vituo vya malezi na makuzi ya watoto vya kijamii, wazazi na walezi wa watoto waliopo katika vituo hivyo wamewezeshwa kuunda vikundi katika kila kituo kwa malengo mawili; kwanza kikundi kama jukwaa la kutoa elimu sahihi ya makuzi ya watoto ikijumuisha afya ya msingi, lishe bora, uchangamfu na ujifunzaji wa awali, malezi yenye kumwitikia mtoto anapoendelea kukua na ulinzi na usalama wa mtoto; na pili kikundi kuwezeshwa kuzalisha mali ili wazazi au walezi kupata kipato cha kuendesha vituo hivyo vya kijamii. Hali hiyo inafanikisha uendelevu wa vituo hivyo.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara inashirikiana na Wizara ya Kilimo kutekeleza Programu ijulikanayo kama *Building a Better Tomorrow (BBT*) mahsusi kwa ajili ya vijana wa kike na kiume ambayo ni afua mojawapo ya kutekeleza Programu ya

Kizazi Chenye Usawa. Programu hiyo itazalisha ajira kwa vijana wa kike na kiume milioni nane (8) nchini ifikapo mwaka 2025. Kupitia Programu hii wasichana 282 sawa na asilimia 34.73 waliochaguliwa kati ya vijana 812 wanaendelea na mafunzo ya miezi minne katika vituo vya mafunzo 15. Utekelezaji wa programu hii utawezesha wasichana kuwa na mashamba makubwa ya pamoja (Block farms) na hivyo kudhihirisha mikakati madhubuti ya Serikali ya awamu ya sita (6) katika kuwezesha wanawake kiuchumi kupitia sekta ya kilimo.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa haki za wanawake na hasa wajane zinapatikana hapa nchini, Wizara inashirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza **Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia** ambayo ni mojawapo ya afua za Programu ya Kizazi Chenye Usawa yenye lengo la kulinda na kukuza haki ya upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria nchini. Kupitia Kampeni hiyo jumla ya Wanawake 1,896,012 na wanaume ya 1,369,910 walifikiwa na kupatiwa elimu ya masuala ya sheria na haki za binadamu katika mikoa yote ya Tanzania bara. Aidha, wanawake 24,856 na wanaume 17,068 walipatiwa huduma ya msaada wa kisheria kupitia wasaidizi wa kisheria 4790 ambao kati yao 1,073 wamesajiliwa, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau yakiwemo Mashirika ya Legal Service Facility (LSF), Legal and Human Rights Centre (LHRC), Women in Law and Development in Africa (WiLDAF), Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA) na Women's Legal Aid Centre (WLAC) katika kuhakikisha huduma za msaada wa kisheria zinawafikia wananchi wengi zaidi.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ushiriki wa wanawake katika kumiliki ardhi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, nyumba na Maendeleo ya Makazi zimeendelea kutekeleza Programu ya kizazi chenye Usawa kwa kuhakikisha wanawake wanapata haki sawa ya kumiliki ardhi. Hadi Aprili, 2023, jumla ya

Hatimiliki ya kimila 39,023 zilitolewa ambapo kati ya hizo Hatimiliki za kimila 13,008 sawa na asilimia 33.3 zilizotolewa kwa wanawake na 26,015 zilitolewa kwa wanaume. Aidha, wanawake 15,102 walipatiwa Hatimiliki kati ya Hatimiliki 45,306 zilizotolewa.

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza programu zinazotoa fursa za elimu kwa wasichana katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM). Serikali inaendelea na ujenzi wa shule 10 za wasichana za masomo ya sayansi kidato cha tano na sita katika Mikoa na nyingine 16 zitajengwa ikiwa lengo la kujenga shule moja kwa kila Mkoa. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya wanafunzi 1,338,884 walihitimu masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati katika ngazi ya Sekondari ambapo kati yao 664,105 sawa na asilimia 41.8 ni wanafunzi wa kike ikilinganishwa na asilimia 48.2 ya wanafunzi wa kiume 674,779 waliohitimu masomo hayo. Vilevile wasichana 244 wenye ufaulu wa juu wamefadhiliwa kusoma masomo ya Utabibu, Uhandisi, Sayansi na Teknolojia na Hisabati kupitia **Samia *Scholarship***. Hii inadhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Dkt Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwawezesha watoto wa kike kuingia katika ushindani wa soko la ajira kwenye ulimwengu wa kidigitali na kuongeza wigo wa kuteuliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi na maamuzi.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kumwezesha mwanamke kiuchumi na kumuongezea muda wa uzalishaji mali, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini chini ya kampeni ya **''Mtue Mama Ndoo Kichwani''** ambapo hadi kufikia Aprili, 2023, upatikanaji wa maji vijijini umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 74.5 mwezi Desemba, 2021 hadi kufikia wastani wa asilimia 77 mwezi Desemba, 2022. Kiwango hicho kimeongeza idadi ya wananchi 3,575,919 wanaopata

huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini na kufanya jumla ya wananchi wanaopata huduma kufikia 30,209,409. Kwa upande wa mijini, hali ya huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 86.5 mwezi Desemba, 2021 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Desemba, 2022, hivyo, kumpunguzia mzigo mwanamke wa kutafuta huduma ya maji sambamba na kumwezesha kuwa na muda wa kushiriki shughuli za uzalishaji mali ili kujiongezea kipato na halikadhalika kupata muda wa kuimarisha malezi na makuzi ya watoto.

**102.** ***Mheshimiwa spika,*** vilevile, Dira na Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha ifikapo 2032 asilimia 80 watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ili **'Kumtua Mama Kuni Kichwani''**. Progamu hii ya Kizazi chenye Usawa inachochea utekelezaji wa mkakati huu wa Serikali ambapo kupitia Wizara ya Nishati mitungi ya gesi 1,900 imetolewa kwa wanawake katika mikoa yote 26 ili kuchochea uhamasishaji wa nishati safi. Vilevile majiko ya gesi 120 na, mitungi ya gesi 120 vilitolewa kwa wanawake mama lishe wa Mkoa wa Dar es Salaam ili kuwachochea wanawake wanaotoa huduma ya Mama lishe kutumia nishati safi. Aidha, hadi Aprili, 2023, asilimia 76.7 ya vijiji vya Tanzania Bara vimeuganishwa na huduma ya umeme kupitia Programu ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA). Hivyo, imesaidia kuwezesha wanawake wajasiriamali kuendelea na uzalishaji wa shughuli zao za kiuchumi kwa kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha na kuongeza uchumi wa kaya na pato la Taifa.

**103.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika kutekeleza programu hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI inaratibu uwezeshaji wa wanawake kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza ujasiriamali ili kujikwamua kiuchumi na kuchangia Pato la Taifa. Kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Halmashauri wameratibu upatikanaji wa mikopo yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 30.9** kwa vikundi 5,120 vya wanawake inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotengwa

na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 nchini ikijumuisha fedha za marejesho inayotokana na mikopo iliyotolewa kabla. Vilevile, Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Nchini (NEDF) ulio chini ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) umetoa mikopo kwa wanawake 1,026 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 2.35**.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mifuko na Programu za Uwezeshaji wananchi kiuchumi zimeendelea kuwezesha wananchi kupata mikopo ya kuanzisha na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi. Mifuko hiyo katika kutekeleza kipaumbele cha Programu ya Kizazi Chenye Usawa imetoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 713.8** kwa wajasiriamali 2,203,838, kati yao wanawake ni 1,234,149 sawa na asilimia 56 na wanaume 969,689 sawa na asilimia 44. Kupitia mikopo hiyo, jumla ya ajira 3,122,104 zilizalishwa, kati ya ajira hizo, wanawake ni 1,623,494 sawa na asilimia 52 na wanaume ni 1,498,610 sawa na asilimia 48. Mikopo hiyo imekuwa chachu kwa wananchi hususan wanawake kujishughulisha na ujasiriamali na uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali, hivyo kuchangia pato la Taifa.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara inaendelea kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, mikopo yenye thamani ya **Shilingi Milioni 664.5** ilitolewa kwa wanawake wajasiriamali 104. Kati ya hao, wanawake 90 walipewa mikopo kupitia vikundi na wanawake wajasiriamali 14 walinufaika kupitia mkopo wa mtu mmoja mmoja katika Mikoa ya Dodoma, Pwani, Singida na Dar es Salaam. Kwa kipindi cha Oktoba 2022 hadi Aprili, 2023 kiasi cha **Shilingi Milioni 78.18** zimerejeshwa na urejeshaji unaendelea. Kulingana na maelekezo ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 29 Machi, 2023 kuhusu utoaji wa mikopo kupitia Taasisi za Kifedha, Wizara imeanza maandalizi ya utoaji wa mikopo hiyo kupitia mfumo wa Benki. Kupitia mikopo hiyo, wanawake wamenufaika na mitaji, fursa za masoko na

kuongeza kipato katika familia zao hivyo, kusaidia kupunguza hali ya utegemezi.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi za fedha ni Wadau muhimu katika utekelezaji wa programu ya Kizazi Chenye Usawa ambapo hadi Aprili, 2023, Taasisi za Fedha (Mabenki) zimeendelea kuanzisha madirisha mahsusi ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Madirisha hayo ni pamoja na Tabasamu (TCB), Wewe ni Jasiri (Azania), Jasiri *Bond* (NMB), Malkia (CRDB), Johari (NBC) na Fanikisha (Equity Bank). Mfano NMB kupitia Jasiri *Bond* imewezesha kiasi cha **Shilingi Bilioni 288.33** kwa wanawake **10,565**.

***Nitoe rai kwa taasisi za kifedha kuweza kupitia upya suala la riba na dhamana ya mikopo ili iwe na masharti nafuu zaidi kwa wanawake hao kupata mikopo ikizingatia kuwa ndio wahanga wa mila na desturi zenye madhara hususan kwenye umiliki wa rasilimali***.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuhakikisha inaratibu, kuelimisha na kuhamasisha Wadau kubainisha fursa za kiuchumi na kuhakikisha zinawafikia wanawake wengi walio vijijini. Uratibu huu utaenda sambamba na kutekeleza kampeni endelevu ya kutangaza shughuli za Serikali na Wadau pamoja na fursa za maendeleo ya kiuchumi. Wizara na baadhi ya wadau kwa sasa inatekeleza Kampeni hii chini ya Kaulimbiu ya "Zijue Fursa, Imarisha Uchumi, Kataa Ukatili, Kazi Iendelee (ZIFIUKUKI)" ambapo wasanii wa kizazi kipya 40 wameteuliwa kuwa mabalozi wa kupinga vitendo vya ukatili na kuchangamkia fursa za kiuchumi *(Ambassadors of Gender Development Initiatives)* kama njia ya kukuza ustawi na maendeleo ya jamii.

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Programu hii, Wizara kwa kushirikiana na OR- TAMISEMI kupitia Maafisa Maendeleo

ya Jamii imeendelea kutekeleza Mwongozo wa Uhamasishaji wa Wanawake Kujiunga na Kuanzisha Vikundi vya Kiuchumi katika Ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kupitia Mwongozo huo, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wameendelea kuhamasisha wanawake kujiunga katika vikundi vya kiuchumi ili waweze kukopesheka ambapo hadi Aprili, 2023 jumla ya vikundi 10,276 vimeanzishwa. Aidha, vikundi 5,120 vya wanawake vyenye wanachama 136,489 vimewezeshwa kupata mafunzo ya ujasiriamali katika shughuli wanazoziendesha. Vilevile, vikundi 34,127 vya kijamii ikijumuisha vikundi vya wanawake vya huduma ndogo za fedha vimetambuliwa kwa lengo la kuviimarisha ili viweze kuwa endelevu, kuongeza huduma jumuishi za kifedha na kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, Wizara imeratibu ushiriki wa wanawake wajasiriamali 7,574 katika maonesho ya ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, wanawake 5,988 walishiriki maonesho ya Sabasaba, 1,300 maonesho ya Nanenane, 60 maonesho ya Utamaduni na Sanaa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) yaliyofanyika nchini Burundi, wanne (4) maonesho ya biashara Italia na 222 maonesho ya Wajasiriamali wadogo na Kati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kupitia maonesho hayo, wanawake wamepata fursa ya kujengewa uwezo kwa kupatiwa elimu ya kodi, urasimishaji wa biashara, hifadhi ya jamii, viwango na ubora wa bidhaa, mbinu za kukuza mitaji na upatikanaji wa masoko ya uhakika. Elimu hiyo ilitolewa kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Taasisi za Fedha na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Wizara katika kukuza ushiriki wa wanawake kwenye biashara, imeratibu wanawake wajasiriamali ili wafikie fursa za masoko ambazo Serikali imezibainisha kupitia nchi za China (maharage ya soya, korosho, mihogo na parachichi); Qatar (nyama); Kenya (mchele), Uturuki (karanga), India (soya

na parachichi), Umoja wa Falme za Kiarabu (pilipili mbuzi na nyama); na Denmark (asali na pilipili kavu).

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inashirikiana na Kampuni ya Global System of Standard (GS1) katika kuhakikisha bidhaa za wajasiriamali wanawake zinazalishwa katika ubora unaokubalika kwa soko la ndani na nje, ambapo jumla ya viwanda 5,500 vimesajiliwa na kupata Msimbomilia (Barcode) inayowezesha bidhaa za wajasiriamali kukidhi viwango vya kimataifa. Katika viwanda hivyo asilimia 80 ni vya wanawake wajasiliamali waliojikita kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo cha viungo (spices) asali, matunda, maziwa, mchele, karanga, ulezi, unga wa mahindi, nyama, samaki, mafuta ya kula na mvinyo.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Programu ya Nchi ya Kizazi chenye Usawa, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wa mwaka 2022 na kupitia Mwongozo huo, jumla ya majukwaa 3,091 yameanzishwa hadi kufikia Aprili 2023. Majukwaa haya yameanzishwa katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, Halmashauri 140, kata 1,149 na vijiji/mitaa 1,776. Aidha, Majukwaa ya Mikoa ya Kilimanjaro, Dar es salaam, Dodoma pamoja na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na wa Halmashauri zote nchini wamejengewa uwezo. Umuhimu wa majukwaa haya umeanza kujidhihirisha kwa baadhi ya Mikoa na Halmashauri ambapo Jukwaa la Mkoa wa Dodoma limeanzisha SACCOs ya wanawake yenye wanachama 322, na Jukwaa la Halmashauri ya Ushetu limeanzisha Mradi wa Kampuni ya Usafi wa Mazingira na usindikaji wa mboga za majani maarufu kwa jina la Nsansa.

**112.** ***Mheshimiwa Spika*****,** utekelezaji wa haya yote niliyozumgumza kuhusu kizazi chenye usawa ni maono ya **Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa ambalo Tanzania imeendelea kung'ara na kuheshimika kutokana na mafanikio yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wake imara. Vilevile, kupitia Jukwaa hili Tanzania imechaguliwa kuwa kiongozi wa kundi la kimataifa linalojumuisha nchi saba (7) zinazotoa mwongozo wa utekelezaji wa maeneo yote ya Kizazi Chenye Usawa. Nchi hizo ni pamoja na **Marekani, Ufaransa, Mexico, Sweden, Afrika ya Kusini na Georgia**. Tanzania ikiwa mojawapo ya Nchi za Kusini mwa Afrika imepewa heshima ya kuwa mwenyeji Mwenza wa Mkutano wa mapitio ya nusu ya kipindi (Mid Point Review) cha utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa. Mkutano huo utafanyika Septemba, 2023. Heshima hii imetokana na kudhihirika umahiri wa ukinara wa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza maono ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na Wadau kuhamasisha na kuwajengea uwezo wanawake kushiriki katika nafasi za uongozi na maamuzi ili kuhakikisha changamoto na vipaumbele vyao vinasikika katika ngazi zote. Kutokana na jitihada hizi, kufikia Aprili, 2023, idadi ya Wanawake Mawaziri imeongezeka kutoka asilimia 21 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 37.5. Idadi ya Madiwani wanawake imeongezeka kutoka asilimia 30.1 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 34.2 Aprili, 2023. Kwa upande wa Makatibu Wakuu, idadi wanawake imeongezeka kutoka asilimia 13.8 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 24.0 Aprili, 2023. Vile vile, kwa nafasi za Wakuu wa Mikoa imefikia asilimia 30.8, Wakuu wa Wilaya asilimia 33.1, Majaji wa Mahakama Kuu ni asilimia 38.1 na Mabalozi asilimia 24.5. Katika kuwajengea wanawake uwezo wa kushiriki nafasi mbalimbali za uongozi, Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Waajiri Tanzania (Association of Tanzania Employers – ATE) imefanikiwa kuwajengea uwezo Wanawake 274 kutoka Kampuni 79 wakiwemo Waheshimiwa

Wabunge na Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar 150. Namshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaamini na kuendelea kuteua wanawake kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara katika kuhakikisha upatikanaji wa wasifu wa Wanawake, imeendelea kuwahamasisha Wanawake kujisajili katika Kanzidata ya Wanawake na Uongozi. Kanzidata hii inatumika kuhifadhi wasifu wa wanawake mbalimbali ili waweze kupata fursa ya kutambulika na hivyo kuwezesha Serikali kuwa na taarifa ya taaluma na ujuzi wa wanawake wa rika tofauti hapa nchini. Hadi mwezi Aprili, 2023 Wizara kwa kushirikiana na Mtandao wa Jinsia Tanzania (Tanzania Gender Network Programme - TGNP) imewajengea uwezo Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa TEHAMA 30 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Mara, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mbeya, Morogoro, Pwani, Iringa, Dodoma, Katavi na Shinyanga. Hadi kufikia kipindi cha Aprili, 2023 jumla ya Wanawake 1,359 wamesajili taarifa zao ikilinganishwa na wanawake 978 waliojisajili mwaka 2022.

***Nitoe wito kwa wanawake wenye ujuzi na taaluma mbalimbali kujisajili katika Kanzidata hii kupitia https://twl.jamii.go.tz ili taarifa/wasifu wao uweze kufahamika pale zinapohitajika.***

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya Manunuzi Sura ya 410 ya Sheria za Tanzania, inaelekeza kutengwa kwa asilimia 30 ya manunuzi Serikalini kwa ajili ya makundi maalum wakiwemo wanawake, vijana na wenye ulemavu. Kupitia sheria hii jumla ya vikundi vya wanawake 117 vimesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), ambapo vikundi 25 vilinufaika na utekelezaji wa Sheria hii. Aidha, Wizara inaendelea kuhimiza Wizara na Taasisi za Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha kundi hili maalum kupata zabuni zenye

vigezo nafuu. ***Nitoe rai kwa Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinatekeleza Sheria hiyo ili makundi maalum yaliyoainishwa yaweze kunufaika na zabuni mbalimbali zinazotangazwa na Serikali yao.***

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO),* Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* Jumuiya ya Ulaya *(EU)* na Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia Masuala ya Wanawake na Jinsia *(UNWomen)* imewezesha uanzishwaji na uimarishwaji wa Madawati ya Jinsia 260 kati ya madawati 612 yanayotakiwa kuanzishwa. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 jumla ya madawati 255 yameanzishwa sawa na asilimia 41.6 ukilinganisha na kipindi cha mwaka 2021/2022 ambapo madawati matano (5) sawa na asilimia 0.8 ya madawati yalianzishwa, hivyo kwa ujumla wake uwepo wa madawati umefikia asilimia 42. Pia Wizara imewajengea uwezo Waratibu wa Madawati ya Jinsia 220 kwenye Vyuo kuhusu wajibu na majukumu ya kupokea taarifa za matukio ya ukatili yanayotokea vyuoni na kuyapatia ufumbuzi unaofaa au kutoa rufaa kwa ajili ya kupata huduma za msingi.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshwaji wa Dawati la Kutokomeza Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Maeneo ya Umma wa Mwaka 2023. Hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara imetoa mafunzo kwa waratibu wa Dawati 216 kati yao 84 ni viongozi wa masoko makuu, 42 kutoka Mikoa sita (6) ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mwanza, Shinyanga na Geita. Mafunzo hayo yalilenga namna bora ya utekelezaji wa mwongozo ambao utawezesha wananchi katika maeneo ya umma kutoa taarifa za vitendo vya ukatili katika dawati linaloratibiwa na Maafisa Maendeleo

ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Biashara, Maafisa Polisi Kata, Watendaji wa Vijiji/Mitaa na Viongozi wa Masoko.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa masuala ya Jinsia yanazingatiwa katika Sera, Miongozo, Mikakati na Bajeti za Serikali, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha uandaaji wa nyaraka za uingizaji wa masuala ya Jinsia katika Ofisi hiyo. Nyaraka hizo ni Mwongozo, Mkakati na Mpango Kazi ambazo zitawezesha ofisi hiyo kujumuisha masuala ya jinsia katika utekelezaji wake. Aidha, kukamilika kwa nyaraka hizo kutaiwezesha pia ofisi hiyo kuangalia kama masuala ya Jinsia yamezingatiwa katika Wizara za Kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala za Serikali na Taasisi zinazojitegemea wakati wanapofanya ukaguzi katika ofisi hizo. Kwa kutekeleza hili, Wizara itafahamu kwa kina utekelezaji wa bajeti ya Serikali inavyozingatia masuala ya Jinsia, hivyo kuiwezesha Wizara kuandaa na kutekeleza mikakati ya ufumbuzi kwa maeneo yenye upungufu kwa Sekta husika.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8 Machi, 2023 ambayo yalifanyika kimkoa. Maadhimisho haya hufanyika kila mwaka ambapo mwaka huu wa 2023 kauli mbiu ilikuwa "**Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia: Chachu Katika Kuleta Usawa wa Kijinsia**". Kaulimbiu hiyo ilisisitiza umuhimu wa mawazo ya ubunifu yenye kuleta mabadiliko, teknolojia jumuishi na elimu inayoweza kutumika katika kupambana na ubaguzi na kutengwa kwa wanawake duniani kote. Aidha katika maadhimisho hayo vazi la Batiki lilitumika kama sare ya Taifa. Kutumika kwa vazi hilo ililenga kukuza soko la ndani la wajasiriamali wazalishaji wa batiki. Hivyo, wanawake walipata fursa, uzoefu na ujuzi wa kutengeneza batiki, kuongeza mitaji na kupanua wigo wa masoko.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki kwenye Mkutano wa 67 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani uliofanyika New York, Marekani mwezi Machi, 2023. Kaulimbiu ya Mkutano huo ilikuwa ni ''**Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia na Elimu Katika Ulimwengu wa Kidijitali Katika Kufikia Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake na Watoto wa Kike**". Mkutano huo ulijadili hatua za utekelezaji wa Sera, Mikakati na Mipango iliyopo kwa nchi wanachama ili kufikia usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kupata ajira na kuongeza kipato. Hivyo, kupitia mkutano huo, ilikubaliwa kuwa nchi wanachama kuhakikisha suala la usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake linafikiwa kwa kuwapatia elimu, stadi, mafunzo ya ubunifu na teknolojia sahihi ili kuwawezesha kuongeza wigo wa kupata ajira na kuongeza kipato.

**ENEO LA 6: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI.**

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura Na. 56. Uratibu huu unalengo la kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika hayo kuendelea kutoa michango yao katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,106 yamesajiliwa yakiwemo Mashirika ya Kimataifa 49, Kitaifa 1,014, Mkoa 24 na Wilaya Mashirika 19.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, Mashirika hayo yamekuwa yakiomba usajili ili kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo afya, maji, mazingira, elimu, kilimo na masuala ya haki za binadamu. Hata hivyo, katika ufuatiliaji ambao umekuwa ukifanyika imebainika kuwa, yapo baadhi ya Mashirika ambayo yamekuwa yakikiuka Sheria, Kanuni na Miongozo. Wizara ilifanya uchambuzi wa uzingatiaji wa Sheria na Miongozo ambapo ilibainika kuwa, hadi kufikia Aprili, 2023 kati ya Mashirika 14,059 yaliyokuwa na usajili,

Mashirika 4,898 yalibainika kutozingatia Sheria ambapo tarehe 19 Januari, 2023 Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliyafutia usajili hivyo kubakia na Mashirika hai 9,161.

**123.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara katika mwaka 2022/23 inaendelea na ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Ufuatiliaji wa utendaji kazi wa mara kwa mara kwa Mashirika hayo hufanywa na Wasajili Wasaidizi waliopo katika kila Halmashauri na Mikoa. Katika ufuatiliaji huo, Wizara imeyafikia Mashirika 2,644 yaliyopo katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, ufuatiliaji huo ulihusisha kupitia mikataba (321), kufanya mikutano (2,270), kufanya ufuatiliaji maalum (17) na ufuatiliaji wa ana kwa ana wa mashirika (26). Mashirika yaliyohusika na ufuatiliaji huo yanatekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa madarasa, vyoo, vituo vya afya na wodi za wazazi; ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa na vifaa tiba; uwezeshaji katika miradi ya kilimo cha chai, mbogamboga, matunda na korosho; uwezeshaji wa wananchi kiuchumi; kutoa mafunzo na elimu ya afya, ulinzi na usalama wa mtoto; uchimbaji wa visima vya maji shuleni na katika vituo vya afya; kutoa huduma katika kambi za wakimbizi, kuwezesha kaya maskini na watoto yatima; usambazaji wa miche ya miti na kugawa madawati shule za msingi; kutoa bima ya afya (iCHF) kwa watoto; kusambaza magodoro gerezani; ujenzi wa vituo vya malezi na makuzi ya watoto na kutoa elimu ya masuala ya fedha. Ufuatiliaji huo ulifanyika katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe, Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Tabora, Mwanza na Kigoma.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, ufuatiliaji ulifanyika kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango, ORTAMISEMI na Wizara za Kisekta, ili kuangalia matumizi ya fedha za miradi zilizotolewa na Washirika wa Maendeleo. Ufuatiliaji huo, ulifanyika katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Morogoro, Pwani, Tanga, Dar es Salaam,

Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Geita, Lindi, Mtwara, Tabora na Shinyanga ambapo ilibaini kuwa miradi mingi ya Mashirika hayo hushirikisha kikamilifu Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, katika ufuatiliaji unaofanyika, Mashirika yanayobainika kwenda kinyume na sheria na taratibu zilizopo yanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Hii ni pamoja na mashirika yale yanayobainika kujihusisha na vitendo vinavyoenda kinyume na maadili, mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania. Aidha, nachukua fursa hii kuyapongeza mashirika yote yanayofanya kazi kwa kuzingatia sheria za nchi pamoja na nyaraka za usajili wao. Naendelea kuyakumbusha Mashirika yote Yasiyo ya Kiserikali kufuata misingi ya Sheria na kuzingatia Mila, Desturi na Tamaduni za kitanzania katika utekelezaji wa majukumu yao kama inavyoelekezwa kwenye Sheria inayosajili na kuratibu Mashirika hayo nchini. Aidha, naendelea kuiasa jamii kuendelea kufichua vitendo vilivyo kinyume na maadili vinavyofanywa na baadhi ya Mashirika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**126.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2022/23 Wizara imepitia na kutoa vibali kwa Mashirika 210 yaliyowasilisha jumla ya mikataba 306 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 206** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo afya, elimu, mazingira, kilimo, maji, haki za binadamu na utawala bora, uboreshaji wa miundo mbinu, uwezeshaji wa jamii na ulinzi wa jamii. Lengo ni kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha kabla ya kutekeleza miradi ikiwa ni pamoja na kufahamu jina la mfadhili, kiasi kinachotolewa na malengo ya ufadhili huo.

**127.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 955 yaliyowasilisha taarifa zao yalipokea **Shilingi Trilioni 1.2** na kutumia **Shilingi Trilioni 1.1** katika maendeleo ya Taifa kupitia utekelezaji wa miradi ya afya, elimu, hifadhi ya jamii, uwezeshaji

kiuchumi, utawala bora, mazingira, maji, jinsia na haki za binadamu. Aidha, ajira 14,121 zilitolewa, ambapo kati ya hizo ajira 8,344 zilitolewa kwa watanzania sawa na asilimia 59.8 ya ajira zote na ajira 5,777 zilizotolewa kwa wasio watanzania sawa na asilimia 40.2 ya ajira zote.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu majukwaa ya Mwaka ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa ambayo yalianza kufanyika kuanzia Septemba hadi Oktoba, 2022 kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Jumla ya Mikoa 20 ilifanya majukwaa na kuwasilisha mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto zilizoibuliwa katika Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ngazi ya kitaifa lililofanyika tarehe 03 - 04 Oktoba, 2022 ambapo ufafanuzi kuhusu mapendekezo yaliyotolewa ulifanyika na kuweka maazimio ya pamoja ya kufanyia kazi changamoto na mapendekezo yaliyoibuliwa.

***Naipongeza Mikoa yote iliyojitokeza kuratibu majukwaa katika ngazi zao kwani inaimarisha uratibu wa pamoja na ushirikiano wa Mashirika hayo kuanzia ngazi za msingi hadi Taifa. Aidha, natoa rai kwa Mikoa kuendelea kuratibu mikutano hiyo muhimu kwa maendeleo ya sekta.***

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 - 2026/27) na kuzinduliwa rasmi na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali tarehe 4 Oktoba, 2022. Mkakati huo utawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupunguza utegemezi wa ufadhili kwa kuwa na vyanzo vingi vya mapato.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara ilianzisha Madawati 19 ya Uratibu wa

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara za Kisekta ambapo yalizinduliwa rasmi na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 04 Oktoba, 2022. Madawati hayo yanalenga kuboresha utendaji kazi kwa kuwa na uratibu wa pamoja wa Mashirika ikiwemo kubadilishana taarifa mbalimbali kwa kuzingatia miongozo iliyowekwa na vigezo vya kitaalam vya Wizara husika wakati wa kutekeleza vipaumbele vyake na utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na Mashirika.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Shirika la *Foundation for Civil Society* imetoa mafunzo kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 638 katika mikoa ya Dodoma (45), Singida (51), Tabora (38), Shinyanga (53), Geita (35), Njombe (50), Ruvuma (64), Rukwa (56), Lindi (32), Mtwara (54), Iringa (62), Mbeya (60) na Tanga (38) na Wasajili Wasaidizi 110 kutoka katika mikoa iliyotajwa hapo juu ukijumuisha mkoa wa Songwe. Mafunzo hayo yamewajengea uwezo na kuboresha utendaji kazi katika kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo.

**132.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini kumekuwa na ushirikiano wa karibu kiutendaji baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Ushirikiano huu hufanyika kwa kubadilishana taarifa, uzoefu na utaalam unaohusisha mikutano ya mara kwa mara baina ya watendaji wa Wizara katika pande zote mbili za Muungano zinazohusika na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, tarehe 22 Desemba, 2022 kilifanyika kikao cha kujadili uboreshaji wa uratibu na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa pande zote mbili za Muungano. Kupitia kikao hicho, uratibu umeendelea kuboreshwa hususan katika masuala ya usajili ambapo hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya Mashirika 36 yalitambulishwa kusajiliwa Zanzibar. Azma ya Serikali ni

kuhakikisha kuwa Mashirika yanakuwa na mazingira mazuri ya kuchangia katika maendeleo ya nchi.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kujenga mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao, Wizara imeendelea kuimarisha mahusiano ya Asasi za Kiraia katika ngazi ya kimataifa kupitia utengamano wa Asasi za Afrika Mashariki ambapo kwa mara ya kwanza Tanzania imekuwa mwenyeji wa mkutano wa Asasi za Kiraia za Afrika Mashariki ambao ulifanyika mkoani Arusha kuanzia tarehe 3 hadi 5 Mei, 2023. Katika Mkutano huo, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alialikwa kuwa mgeni rasmi na aliniagiza nimuwakilishe. Kupitia mkutano huo, Nchi wanachama za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan ya Kusini zilishiriki na hivyo kupata fursa ya kuimarisha mahusiano na nchi nyingine, kubadilishana uzoefu na kuweza kutambua fursa mbalimbali zilizopo ndani ya Afrika Mashariki.

**ENEO LA 7: URATIBU WA UTEKELEZAJI WA MTAKUWWA.**

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikitekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kwa kipindi cha miaka mitano (2017/18 - 2021/22) ambapo ukomo wake ulifikia Juni, 2022. Agenda ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni endelevu, hivyo pamoja na utekelezaji wa MTAKUWWA awamu ya kwanza kukamilika Juni 2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za MTAKUWWA zikiwemo ukamilishaji wa maandalizi ya MTAKUWWA awamu ya pili, uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya mkono kwa mkono na ujenzi wa nyumba salama. Aidha, Wizara imekubaliana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ajenda hii kuwa ya kudumu kwenye vikao vyote vya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatunga sheria ndogo za kupinga ukatili katika maeneo yao.

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeratibu tathmini ya utekelezaji wa MTAKUWWA ambapo baadhi ya matokeo ya tathmini hiyo ni pamoja na: Jumla ya wananchi 5,180,684 (Wanawake 56% na Wanaume 44%) walinufaika na Programu ya TASAF awamu ya Tatu inayolenga kunusuru kaya maskini; kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya Madhara ya Ukatili kupitia Kampeni mbalimbali zilizofanywa kwa kushirikiana na wadau na vyombo vya habari ambapo kutokana na Taarifa za Jeshi la Polisi jumla ya matukio ya ukatili wa kijinsia 226,621 (Wanawake 70,312 na Wanaume 156,309) yameripotiwa katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2022; Kupungua kwa vitendo vya ukeketaji ambapo kutokana na Utafiti wa *Social Institution and Gender Index - SIGI* unaonesha kuwa kiwango cha ukeketaji Tanzania ni 12% ikilinganishwa na kiwango cha ukeketaji kwa ukanda wa Afrika Mashariki ambapo ni 38%; Kuanzishwa kwa Mahakama za Watoto 133; kuimarika kwa mazingira salama shuleni ikiwemo kutungwa kwa Waraka wa Elimu No.2 wa mwaka 2021 kuhusu urejeshwaji shuleni wa wanafunzi waliokatiza masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali; kuwepo kwa dawati la Jinsia na Watoto 420 katika vituo vya Polisi; na kuanzishwa kwa Kamati za Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto 18,186. Mafanikio mengine ni pamoja na kuwepo kwa Mazingira ya Kisera ya Uratibu wa MTAKUWWA ambapo Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali zimetungwa.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya tathmini yamewezesha maandalizi ya MTAKUWWA kwa awamu ya pili ambapo pamoja na masuala mengine, tathmini ilipendekeza kwamba ili kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa MTAKUWWA II, muundo wa Uratibu uhusishe Mawaziri ambao ni wasimamizi wa Sera, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Rasimu ya Mpango wa Pili wa MTAKUWWA kwa miaka mitano (2023/24 – 2027/28) inayotarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023 na kuanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2023/24. Maeneo

yatakayowekewa mkazo katika Mpango wa Pili ni pamoja na:- kuimarisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika ngazi zote ili ziweze kutekeleza majukumu yake; kushirikiana na vyombo vya habari kutoa elimu kwa jamii juu ya masuala yote ya MTAKUWWA; na kuimarisha mifumo ya kijamii ya kutunza mila na desturi chanya ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu mila na desturi zenye madhara kwa taifa la Tanzania.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu utoaji wa huduma kwa manusura wa ukatili wa kijinsia kwa kuanzisha vituo vya Mkono kwa Mkono katika maeneo mbalimbali. Mpaka sasa kuna vituo 22 ambavyo viko katika hospitali mbalimbali nchini. Katika mwaka 2022/23 kimeanzishwa kituo katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma. Aidha, kupitia vituo hivyo jumla ya manusura wa vitendo vya ukatili 1,857 walipatiwa huduma jumuishi ikiwemo huduma za kitabibu, msaada wa kisheria na huduma za unasihi na ushauri. Lengo ni kuwezesha utoaji wa huduma hizo katika eneo moja ili kuepusha usumbufu, ucheleweshaji wa huduma na kuharibu au kupoteza ushahidi.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Nyumba Salama zimeongezeka kutoka 10 hadi 11 kati ya 26 zinazohitajika, ambapo nyumba moja (Wote Sawa) imejengwa katika Mkoa wa Mwanza. Aidha, Nyumba Salama nyingine zipo katika Mikoa ya Arusha (3), Iringa (1), Kigoma (1), Mara (2), Morogoro (1) na Kilimanjaro (2). Nyumba hizi zinatumika kutoa huduma za msingi na hifadhi ya dharura kwa manusura wa ukatili nchini. Katika kipindi cha Julai hadi Aprili, 2023 jumla ya manusura 482 walihudumiwa kupitia Nyumba hizo. Wizara kwa kushirikiana na Wadau itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Nyumba Salama katika maeneo mbalimbali kulingana na uhitaji wake.

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeendelea kutoa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Vilevile, Taasisi imeendelea kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika nyanja zinazo shabihiana na taaluma ya Maendeleo ya Jamii. Aidha, kumekuwepo na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Taasisi hii ili kuimarisha mifumo ya utoaji wa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi kwa lengo kuongeza ukusanyaji wa mapato.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwa na ongezeko la udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 2,800 katika ngazi zote (Ke 1,857 na Me 943) waliodahiliwa katika mwaka 2021/22 hadi kufika wanafunzi **2,918** katika ngazi zote (Ke 1,935 na Me 983) kwa mwaka wa masomo 2022/23 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 4.2. Aidha, kwa mwaka 2022/23, jumla ya wanafunzi 1,619 (Ke 1,121 na Me 498) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,464 (Ke 1,006 na Me 458) waliohitimu mwaka 2021/22.

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kupitia Kituo cha Kitaifa cha utafiti na uhifadhi wa machapisho yanayohusu wanawake iliandaa Kongamano kubwa la wanawake tarehe 7 Machi, 2023 kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani na jumla ya wadau 250 kutoka makundi mbalimbali walishiriki. Lengo la kongamano hili ilikuwa ni kupata taarifa za tafiti mbalimbali kuhusu hali halisi ya masuala ya

usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake, pamoja na kubadilishana uzoefu wa afua mbalimbali zinazofanywa na wadau katika maeneo hayo.

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, aidha, kituo kimefanya midahalo ya masuala ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake kwenye Taasisi za Elimu 20 kwenye Mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa lengo la kuwezesha wasichana kutambua wajibu na haki zao pamoja na fursa mbalimbali za kujiendeleza kielimu na kibiashara ambapo jumla ya wanafunzi 3,000 kutoka Taasisi za elimu wameshiriki na kunufaika na midahalo hiyo.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Taasisi ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 5,470,132,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali ambapo hadi mwezi Aprili 2023, Taasisi imefanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 3,246,855,420.00** sawa na asilimia 60 ya makadirio. Aidha, ufuatiliaji wa madeni ya ada za wanafunzi na huduma ya hosteli inaendelea ili kuhakikisha chuo kinafikia malengo ya makusanyo.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Taasisi ilifanikiwa kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ambapo shughuli mbalimbali zilifanyika ikiwemo mijadala kuhusu migogoro ya kifamilia inavyochangia unyanyasaji wa kijinsia miongoni mwa wanandoa na ilibainika kuwa wanaume pia ni waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia. Aidha, mafunzo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na hatua za kukabiliana nayo yaliendeshwa kwa wanawake 500 kutoka Kata za Akheri, Kikwe na Kiutu Wilayani Arumeru pamoja na wanafunzi 200 wa shule za msingi na wanafunzi 300 wa sekondari walipatiwa mafunzo hayo.

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imechapisha tafiti 24 kupitia Jarida *(Journal)* la Taasisi lijulikanalo *Tengeru Community Development Journal - (TCDJ)*. Pia, Taasisi imefanya tafiti kuhusu viashiria vya ushirikishwaji wa Jamii

*Community Participation Indicators* katika mikoa 11 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**147.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2022/23 baadhi ya huduma za ushauri elekezi zilizotolewa na Taasisi zilijikita katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto uliofanyika katika Kata 18 za Mkoa wa Shinyanga;

(ii) Mtazamo wa Haki za Binadamu katika Kilimo cha Tumbaku kwa mikoa ya Kigoma na Tabora;

(iii) Usimamizi wa Maliasili katika ukuaji wa utalii;
(iv) Kuanzishwa na Kuendeleza Usimamizi wa Vihatarishi ndani ya Halmashauriza Jiji la Arusha na Manispaa ya Lindi na;

(v) Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko na Ukatili wa Kijinsia/Unyanyasaji wa kingono kwa Viongozi wa Hifadhi za Mbuga za Wanyama, Viongozi wa Serikali za Tarafa, Kata na Vijiji kwenye maeneo yanayoshiriki kusimamia mradi wa maliasili na kuendeleza utalii kusini mwa Tanzania (REGROW). Mradi huo unasimamiwa na TANAPA chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

**148.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Taasisi imeendelea kutekeleza programu ya kuchochea na kuendeleza ubunifu (innovation) miongoni mwa wanafunzi kupitia Kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidijitali (Jamii Outreach Digital Innovation Center – JODIC). Kituo hiki kinatumika kuratibu utekelezaji wa programu za ubunifu wa kidijitali, ushirikishaji jamii na uanagenzi katika kazi pana za Taasisi. Kupitia kituo hicho, Taasisi imetekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Taasisi imewajengea uwezo wanafunzi kwa kuwabadilisha mtazamo **(mindset change**) pamoja na kuwajengea ujuzi na stadi za kazi kwa kupitia wadau mbalimbali kama vile Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO). Kupitia eneo hili wanafunzi 120 wameweza kujiajiri baada ya kupatiwa mafunzo ya uzalishaji bidhaa kama vile mafuta ya kupaka, bidhaa za kufanyia usafi (sabuni mbalimbali), mabegi/mikoba, bidhaa za chakula kama asali, ubuyu, karanga na unga lishe; na

(ii) Jumla ya wanafunzi 1,145 (wanaume 407 na wanawake 738) walifanya uanagenzi kwa muda wa miezi miwili katika mwaka 2022/23 na hivyo kupata ujuzi mbalimbali katika maeneo ya utatuzi wa changamoto za jamii, uandaaji na usimamizi wa vikao, ukusanyaji wa kodi, utoaji wa elimu ya vikundi vya kuweka na kukopa fedha (vicoba), utengenezaji wa sabuni za maji, utengenezaji wa unga wa lishe, utengenezaji wa mapambo kutokana na taka ngumu, uandishi wa maandiko ya miradi na tafiti mbalimbali na usimamizi wa miradi.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, kwa upande wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili katika fani ambazo zinalenga Ustawi wa Jamii. Ili kufikia malengo iliyojiwekea, Taasisi imeendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vyake ambavyo ni: - ada za wanafunzi, tafiti, ushauri elekezi na vyanzo vinginevyo. Katika mwaka 2022/23, Taasisi ilitarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 7,651,467,000.00** Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Taasisi imekusanya **Shilingi 3,762,313,349.00** sawa na asilimia 50 ya makadirio. 150. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2022/23, Taasisi imedahili wanafunzi 2,966 (Ke 1,864 na Me 1,102) ikilinganishwa na wanafunzi 3,234 (Ke 2,104 na Me 1,130) waliodahiliwa

mwaka 2021/22. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2022/23, wanafunzi 1,036 walidahiliwa katika ngazi za Astashahada, wanafunzi 890 ngazi ya Stashahada, wanafunzi 947 ngazi ya Shahada, wanafunzi 7 ngazi ya Stashahada ya uzamili na wanafunzi 86 ngazi ya Shahada ya Uzamili. Katika mwaka wa masomo 2022/23, Taasisi ilikuwa na wanafunzi 5,341 (Ke 3,523 na Me 1,818) ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.6 ikilinganishwa na wanafunzi 4,784 waliokuwepo mwaka 2021/22.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kutoa msaada wa kisaikolojia kwa wanafunzi na Jamii kupitia kituo chake cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia. Kituo hiki kinatumika na Taasisi kufanya programu za kushirikisha Jamii (Community engagement), uanagenzi (Apprenticeship) na ubunifu (innovation). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Taasisi ilifanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Imetoa huduma za elimu ya afya ya akili na namna bora ya kukabiliana na msongo wa mawazo, huduma ya awali ya msaada wa kisaikolojia, elimu rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana pamoja na elimu ya mahusiano na ndoa. Huduma hizi zimetolewa kwa jumla ya watu 4,713 kati yao 2,648 ni watumishi wa Taasisi binafsi na za Umma na 2,065 ni wanajamii wenye mahitaji mbali mbali ya huduma zinazotolewa na Taasisi. Huduma hizi hutolewa kwa lengo la kuimarisha utulivu wa afya ya akili, ubunifu, kuwa na mtazamo chanya na kuona fursa zilizopo katika jamii na kuzitumia ili kuleta ustawi na maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

(ii) Katika kutekeleza programu ya uanagenzi, Taasisi imepeleka jumla ya wahitimu 79 wa kada ya Ustawi wa Jamii katika maeneo mbali mbali nchini. Kati ya wanagenzi 79, 12 wapo Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni –Tanga na 67 katika Halmashauri – Idara mbalimbali za serikali pamoja na Mashirika Binafsi. Wanagenzi 12 waliopo kijiji cha Msomera

wanatoa huduma mbalimbali za Ustawi wa Jamii kwa kipindi cha miezi 6 kwa wananchi waliohama kutoka Ngorongoro na wenyeji wa eneo hilo kulingana na uhitaji.

(iii) Kupitia programu ya kuwawezesha wanawake na vijana kiuchumi Taasisi ilishirikiana na ***Kampuni ya Coca Cola Kwanza*** kutoa elimu ya afya ya akili, jinsi ya kukabiliana na msongo wa mawazo na namna bora ya kufanya biashara pamoja na uhifadhi wa kumbukumbu za kibiashara kwa mama lishe 948 na vijana wanaojishughulisha na ukaangaji wa chipsi 913 katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

(iv) Taasisi imeendesha semina elekezi ya Malezi na Makuzi ya Watoto kwa Wadada - Wasaidizi wa kazi za nyumbani 110. Lengo ni kuwajengea uelewa wa pamoja wa namna bora ya kutoa huduma ya malezi na makuzi kwa watoto pamoja na namna bora ya kukabiliana na changamoto za malezi. Programu hii ni endelevu na inatarajiwa kutolewa katika mikoa yote nchini. Kwa awamu ya kwanza imefanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam.

(v) Taasisi imeendesha Programu ya kuwajengea uelewa vijana waendesha bodaboda juu ya ukatili wa kijinsia, viashiria, madhara, sehemu sahihi ya kutolea Taarifa, na namna ya kukabiliana na vitendo vya ukatili. Mafunzo haya yamehusisha vijana 47 Kwa awamu ya kwanza kutoka "vijiwe" mbali mbali katika Wilaya ya Kinondoni – Dar es Salaam ambao watakuwa mabalozi katika sehemu zao za kazi. Programu hii ni endelevu na inatarajiwa kufanyika katika mikoa mbali mbali nchini.

(vi) Taasisi ilitoa mafunzo ya namna ya kukabiliana na ukatili, kujiendeleza kitaaluma na kupigania haki kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 700 kati yao Wanawake 500 na Wanaume 200 katika Kata ya Kijitonyama.

(vii) Taasisi iliandaa kongamano la wanandoa lililohudhuriwa na watu 317 ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na migogoro katika mahusiano na ndoa. Washiriki 67 walijitokeza kwa ajili ya kupata huduma ya msaada wa kisaikolojia na mashauri ya ndoa.

**152. *Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ilitoa matokeo ya tafiti mbili zinazohusu Unyanyasaji wa Kijinsia katika Elimu ya Juu (*Eradicating Sexual Violence among Higher Learning Students in Tanzania: The Role of Social Media*) na nyingine inayohusu Umuhimu wa Kazi za Staha katika Kuboresha Makampuni (*Realization of Decent Work Objectives in Small and Medium Enterprises (SMEs) in Tanzania*). Lengo kuu la Tafiti hizi ni kutambua namna ambavyo mitandao ya kijamii inaweza kutumika kutoa elimu na kuzuia ukatili wa kijinsia huku tafiti ya pili ikiwa na lengo la kuangalia namna ambavyo viwanda vidogo vidogo na vya kati vinaweza kufikia vigezo vya kazi za staha. Katika tafiti hizo matokeo yalionesha kuwa mitandao ya kijamii ikitumika vizuri ina mchango mkubwa katika kukomesha na kuzuia ukatili, kwa kuwa inawapa wananchi fursa ya kupata Taarifa mbalimbali pamoja na nafasi ya kushiriki katika midahalo inayozungumzia namna bora ya kutokomeza ukatili. Katika utafiti wa pili iligundulika kuwa viwanda vidogo vidogo vinakidhi vigezo vya kazi za staha kwa kati ya asilimia 25 na 75 kutegemea na ukubwa pamoja na jukumu la kiwanda.

**153. *Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea na tafiti nyingine tatu zinazohusu kupunguza unyanyasaji na unyonge wa wafanyakazi wa sekta zisizo rasmi (*Buffering Deprivation and Vulnerability among Informal Workers in The Covid-19 Context: The Case of the Tourism Sector in Kilimanjaro and Arusha Regions*), Namna ya kuzuia unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake (*Protecting Women in Tanzania: Prevention of GBV Through Indigenous Approaches in Tanga and Mara Regions - ProWomen-TZ*) nyingine inahusu changamoto wanazopitia

watoto wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia katika kupata msaada (*Barriers to Help Seeking Behavior among Children Who Experience Sexual Violence in Tanzania: The Case of Dar es Salaam, Tanga and Coast Regions*). Lengo kuu la tafiti hizi ni kuweza kuibua njia za kuzuia na kupambana na ukatili kwa wanawake na watoto.

**E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**154. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi na Vyuo vilivyo chini yake. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, Wizara iliweza kupokea fedha za ndani za maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.97** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii (**Shilingi Bilioni 3.97)** na Mradi wa Huduma za Ustawi wa Jamii (**Shilingi Bilioni moja)**.

**155.** *Mheshimiwa Spika,* kati ya fedha za ndani zilizopokelewa Shilingi Bilioni 3.97 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (Shilingi Bilioni 1.6) na Vyuo vya Maendeleo ya jamii Rungemba (Shilingi Milioni 70), Ruaha (Shilingi Milioni 500), Monduli (**Shilingi Milioni 500**), Buhare (**Shilingi Milioni 500)** pamoja na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi vya Misungwi (**Shilingi Milioni 300)** na Mabughai **(Shilingi Milioni 500)**.

**156. *Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizotekelezwa kutokana na fedha hizo ni: kutengeneza na kufunga milango na madirisha na kuweka samani katika kumbi pacha za mihadhara na bweni la wasichana katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Kwa upande wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba fedha zilitumika kuanza ujenzi wa Maabara ya Kompyuta yenye

uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kwa wakati mmoja, ujenzi huo unaendelea. Aidha, katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mabughai fedha zilizopokelewa zimetumika kununua Lori na gari aina ya *pick up double cabin*, fedha nyingine zilitumika kukarabati nyumba moja ya mtumishi, kufunga mifumo ya TEHAMA, kununua mashine ya tofali (Poker Machines), *mobile block machines*. Vilevile, katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, fedha zilitumika kujenga bwalo la Chakula lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi huo bado unaendelea. Kwa upande wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli, fedha zilizopokelewa zimetumika katika ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 kwa wakati mmoja, ujenzi huo bado unaendelea.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi fedha zilipokelewa zimetumika katika ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 352 kwa wakati mmoja, ambapo kazi hii inaendelea na katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare fedha zilizopokelewa zimetumika katika ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 450 kwa wakati mmoja, ambapo kazi ya ujenzi inaendelea.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha za ndani zilizopokelewa **Shilingi Bilioni moja** imeelekezwa kwa ajili ya kukarabati makazi ya wazee Ipuli – Tabora na Njoro – Kilimanjaro **(Shilingi Milioni 400)**, Mahabusu ya Watoto Mbeya na Arusha **(Shilingi Milioni 300).** Vilevile kazi ingine ni ujenzi wa hosteli katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Kampasi ya Kisangara **(Shilingi Milioni 300)**.

## F. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/24

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele kumi

(10) ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Vipaumbele hivyo ni:-

(i) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF);

(ii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA);

(iii) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up);

(iv) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo;

(v) Kutambua na kuratibu Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo ili kuboresha mazingira ya biashara zao;

(vi) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii;

(vii) Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

(viii) Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki za watoto na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee;

(ix) Kuimarisha mifumo ya malezi, ulinzi na maendeleo ya watoto na familia; na

(x) Kuimarisha utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili mchango na ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa uweze kutambulika na kuwa na tija kwa jamii.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara kwa mwaka 2023/24 imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 74.2** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuwezesha uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na: -

(i) Katika eneo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF), kiasi cha **shillingi Bilioni 4.9** zimetengwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi;

(ii) Katika eneo la kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.3** kimetengwa;

(iii) Katika eneo la kutambua na kuratibu shughuli za kiuchumi za Makundi Maalum hususan wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo machinga, mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji, kiasi cha **Shilingi Bilioni 18.5** kimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza mitaji na kuboresha shughuli zao za kiuchumi;

(iv) Kwenye eneo la watoto, kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.6** kimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria,

kufuatilia utoaji wa huduma katika Makao ya Watoto, Nyumba Salama na Vituo vya Kulelea Watoto wadogo Mchana na Watoto Wachanga; Kukarabati Shule ya Maadilisho ya Irambo; Kukarabati Mahabusu za Watoto Upanga, Arusha, Mbeya, Moshi na Tanga; na Kukamilisha ujenzi wa Mahabusu ya Watoto Mwanza;

(v) Katika eneo la Wazee, **Shilingi Bilioni 1.8** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi kwa wazee wasiojiweza katika Makazi ya Wazee 14 na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Makazi ya Misufini, Mwanzange, Ipuli na Bukumbi;

(vi) Kwenye eneo la Taasisi na Vyuo, kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.1** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, na Vyuo vitatu (3) vya Maendeleo ya Jamii vya Uyole, Monduli na Misungwi;

(vii) Eneo la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali limetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.6** kwa ajili ya ufuatiliaji wa Mashirika 1,000 katika Kanda Tano, kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yapatayo 1,000, kuandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2022, kuwezesha Mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS), kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/2023 - 2025/2026), kuratibu Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuratibu Vikao vya Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(viii) Eneo la maendeleo ya jamii limetengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 283.6** kwa ajili ya kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kuamsha Ari ya Jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi na kutekeleza

Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up) katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara; na

(ix) Katika eneo la ufuatiliaji na tathmini, kiasi cha **Shilingi Milioni 200** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi wa Jamii vilivyo chini ya Wizara.

## G. SHUKRANI

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta mbalimbali zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki zikiwemo Marekani, Ufalme wa Uingereza, Ufalme wa Sweden, Ufalme wa Norway, Falme za Nchi za Kiarabu, Japan, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Canada, Ufalme wa Denmark, Ireland, Jamhuri ya Uswisi, Italia, Bangladesh na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na:- Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UN-Women, UNDP,UNICEF, UNFPA, WHO, ILO, IOM, FAO, WFP, UNHCR na UNESCO. Vilevile, ninashukuru Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU). Pia nayashukuru Mashirika ya Kimataifa ambayo ni:- Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund (for HIV,TB and Malaria)* na *Hilton*

*Condrad Foundation*. Aidha, nazishukuru Taasisi za Kifedha za hapa nchini zinazoshirikiana na Wizara ambapo ni pamoja na Benki za NMB, CRDB, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), NBC, Stanbic, Azania, Equity, Benki ya Mkombozi, Akiba Commercial Bank (ACB) na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

**164. *Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi na Mashirika ya Dini kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na; *Foundation for Civil Society*, WiLDAF, ICS, TAWLA, TAYOA, LSF, *SOS Children's Village Tanzania*, *Railway Children Tanzania*, BRAC Maendeleo Tanzania, *Plan International - Tanzania*, Kivulini, FSDT, WFT, TANLAP, *The Aga Khan Foundation*, *HelpAge International*, *Save the Children, World Vision, PACT Tanzania, Equality for Growth (EfG)*, Landesa, AMFED, CSEMA; REPPSI, *Amani Girls Home*, Pelum Tanzania, LHRC, Haki Elimu, TWCC, *Compassion International, Care International Tanzania*, TECDEN, EGPAF, *Responsible Organization Tanzania*, FAGDI, *Safe Society Platform Tanzania*, *Both Ends Believing* (BEB), MEWATA na *Children in Crossfire*.

**165. *Mheshimiwa Spika,*** nitoe pia shukrani zangu kwa Jumuiya za makundi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Wizara. Jumuiya hizo ni pamoja na:- Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jukwaa la ULINGO, Jumuiya ya Wazazi CCM, Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Baraza la Wazee Tanzania, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TAWIA, Chama cha Wazee Wanaume Tanzania, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA), Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA) na Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT). Pia naomba nizishukuru Klabu za Mpira wa Miguu Tanzania hususan Yanga na AZAM na vyombo vyote vya habari.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe shukrani zangu pia kwa viongozi na taasisi zetu za dini zikiwemo Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA).

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Naomba kumshukuru **Dkt. John A. K. Jingu,** Katibu Mkuu na **Bw. Amon A. Mpanju,** Naibu Katibu Mkuu kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wasajili, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mahiri uliowezesha kukamilisha maandalizi ya Hotuba yangu kwa wakati muafaka.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru Bodi na Menejimenti za Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mzuri unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendelee kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya Taifa letu.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, kupitia OR – TAMISEMI nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote na Wataalam wote chini ya Ofisi zao na pia Wadau wote wa sekta mbalimbali wanaohudumia katika maeneo yao pamoja na

wananchi mmoja mmoja na mitandao yote ya habari za kijamii ambao wamekuwa wakifuatilia na kutoa ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu hasa kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia na kwa watoto.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, hususan mume wangu **Wakili Methusela Gwajima** na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa usawa wa jinsia huku wakitumia **Simu Namba 116** bila malipo kwa ajili ya kuripoti matukio au viashiria vya ukatili saa 24 kila siku. Aidha, nawahimiza kuendelea kutumia simu zote kama tulivyotangaza kwenye vyombo vya habari na kuziweka kwenye tovuti yetu ya Wizara ambayo ni ***www.jamii.go.tz***.

**H. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2023/24 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2023/24**

**171**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara imekadiria kukusanya **hilingi 8,500,000,000.00** kutokana na ada katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na mapato mengine.

**Matumizi ya Kawaida**

**172**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 43,664,963,000.00** kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,577,510,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 17,087,453,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

**Miradi ya Maendeleo**

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 30,558,230,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,800,000,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 3,758,230,000.00** ni Fedha za Nje.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) inaomba jumla ya **Shilingi 74,223,193,000.00** ili kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum www.jamii.go.tz

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa baada ya wasilisho hilo la Waziri nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa niaba yake Mheshimiwa Katani Katani aje awasilishe maoni ya Bunge.

**MHE. KATANI A. KATANI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii yote iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. kwa mujibu wa kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengwa fedha wa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaa wa kukagua Mradi wa Ujenzi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara, ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Makazi ya Wazee Njoro na Mahabusu ya watoto Moshi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi katika taasisi ya jamii tengeru. kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 Taasisi ilipokea kiasi cha shilingi 1,600,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa samani, malipo ya mshauri elekezi na vibarua vifaa vya TEHAMA. Katika ziara hii Kamati pia ilibaini kuwa taasisi inaendesha miradi ya kujifunzia na uzalishaji ikiwa na lengo la kuongeza mapato na kutoa mafunzo kwa wanafunzi. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kutengeneza *paving block,* mradi wa ufugaji samaki na mradi wa uchapishaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza utekelezaji mzuri wa ujenzi wa miradi hii ya maendeleo na pia kwa kuwa wabunifu wa miradi ambayo itongeza pato la ndani la chuo pia kwa kupatia ujuzi wanafunzi. Pamoja na pongezi hizo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika chuo hiki zikiweomo zifuatazo: -

(i) Uchakavu wa miundombinu ya chuo. Katika ziara hii kamati ilishududia jinsi majengo ya chuo yalivyochakavu kutokana na kuwa ya muda mrefu sana;

(ii) Ukosefu wa bweni la wavulana. Kutokana na chuo kuwa umbali mrefu toka mjini kamati inashauri kuwa Serikali ione umuhimu wa kuanza ujenzi wa mabweni ili kupunguza adha ya malazi.

(iii) Upungufu wa Nyumba za Watumishi. Katika kutatua changamoto hii, Kamati ilishauri kuwa Taasisi kwa kutumia mapato ya ndani itenge fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba hizi.

(iv) Chuo kutokuwa na Hatimiliki ya eneo lake jambo linaloweza kuwavutia wanachi kuvamia na kusababisha migogoro ya umiliki wa ardhi. Ni rai ya

Kamati kuwa Chuo kiharakishe kupima maeneo yake na kupata Hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa ujenzi katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 chuo kilitengewa kiasi cha shilingi 300,000,000 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 104. Hata hivyo, hadi Kamati inatembelea mradi huu hakuna fedha iliyokuwa imepelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakipongeza chuo kwa kuaanda Mtaala wa Elimu ya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto katika ngazi ya Stashahada na tayari umeshaidhinishwa kwa matumizi na mamlaka ya ufundi na ufundi stadi. Mpango huu una mchango mkubwa katika hatua za kudhibiti mmomonyoko wa maadili kupitia utekelezaji wa vituo vya malezi na makuzi ambavyo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa Taifa wa *Generation Equality Programme*.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande mwingine, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi 400,000,000 kilipokelewa na taasisi. Hadi Kamati inatembelea mradi huu, kiasi cha shilingi 235,821,079.70 kilikuwa kimetumika, ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa msingi, kuta, kuezeka miundombinu ya maji safi na umeme.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao umegharimu kiasi cha shilingi 235,821,079.70 na haionekani kulingana na thamani ya fedha iliyotumika, na utekelezaji umechukua muda mrefu licha ya kupatiwa fedha zote kwa wakati. Ni rai ya Kamati kuwa miradi hii ikamilike kwa wakati ili kuongeza thamani ya mradi na kuwasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilibaini kuwa Chuo hakina Hatimiliki ya maeneo yake, jambo linalohatarisha maeneo hayo kuvamiwa na wananchi. Ukosefu wa jengo la utawala na maktaba, upungufu mkubwa wa watumishi katika kada mbalimbali, ukosefu wa maji, na upungufu wa hosteli. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kutenga fedha za Bajeti ili kuweza kujenga miundombinu ya chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Makazi ya Wazee Njoro na Mahabusu ya Watoto Moshi. Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha shilingi 200,000,000 zilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa Makazi ya Wazee Njoro, lakini hadi Kamati inatembelea makazi haya, hakuna fedha iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, katika ziara yake Kamati ilishuhudia uchakavu wa majengo ya Mahabusu ya Watoto na ufinyu wa majengo, ukosefu wa nyumba za watumishi, ukosefu wa eneo la michezo kwa watoto na ukosefu wa gari la kuhudumia vituo hivi. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuboresha Mahabusu ya Watoto na Makazi ya Wazee ili waweze kuishi katika mazingira mazuri na kununua magari kwa ajili ya kutoa huduma kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaishauri Wizara kuanzisha miradi ya ufugaji ng'ombe wa maziwa, kuku, bustani katika eneo la makazi ya wazee kwa kuwa wana eneo lenye ukumbwa wa mita za mraba 5,226 kwa ajili ya kuwawezesha wazee kujishughulisha na kazi ndogo ndogo, na kuboresha lishe kwa wazee na kuongeza kipato katika makazi ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha

2022/2023; kwa upande wa uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 8,500,000,000. Hadi kufikia Februari, 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya shilingi 2,712,157,233, sawa na asilimia 32 ya makusanyo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekena katika Jedwali Na. 1. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa ni asilimia 32 tu ya makusanyo yote, Wizara hii ilikusanya katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara hii siyo ya kuridhisha. Kamati ilitaka kujua sababu za makusanyo madogo kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato ambapo ilielezwa kuwa imetokana na wanafunzi wengi kutoripoti kama ilivyokadiriwa na Vyuo. Kufutwa kwa usajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali 4,898 kutokana na ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo inayosimamia shughuli za mashirika haya ambapo imeathiri makusanyo ya Mapato kutoka kwenye ada za usajili na ada za mwaka za mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua ya kufuta Mashirika yasiyo ya Kiserikali 4,898 ambayo yalikiuka sheria, kanuni na miongozo inayosimamia shughuli za mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande mwingine, Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato, yanaweza kutafsiriwa kwamba ama malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi; au jitihada za ukusanyaji zilikuwa hafifu, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ipange bajeti yake kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 32,310,981,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo, shilingi 18,169,057,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi 14,141,924,000 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara ilihamishiwa kiasi cha shilingi 6,729,892,250 kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya uratibu wa kitengo cha makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi 19,175,644,557 sawa na asilimia 59 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 9,667,294,223 sawa na asilimia 68 ni fedha kwa ajili ya mishahara na shilingi 9,508,350,333.56 sawa na asilimia 52 ni fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* na hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa ajili ya uratibu wa Machinga. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ya Wizara pamoja na Taasisi zake ni wa kuridhisha kwani imepokea asilimia 59 ya fedha iliyoidhinishwa. Aidha, Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 hakuna Fedha iliyopokelewa kwa ajili ya uratibu wa wafanyabiashara ndogo ndogo, maarufu kama Machinga.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati, na kwa ufanisi, upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa wakati na kwa kadri inavyostahili ni jambo muhimu kufanikisha. Hivyo ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha hizo kwa wakati na kwa ukamilifu ili kutoathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 11,092,080,000 kwa ajili ya utekelezaji

wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,900,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 4,192,080,000 ni fedha za nje. Wizara ilihamishiwa kiasi cha shilingi 16,196,000,000 kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo, maarufu Machinga.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 6,831,334,941 sawa na asilimia 62. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,940,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 891,334,941 ni fedha za nje na hakuna fedha yoyote ya Machinga iliyotolewa. Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa katika Jedwali Na. 3.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kama ifuatavyo:-

(a) Kwa jumla mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichopangwa kupokelewa ambapo ilipokelewa asilimia 21 tu ya makadirio jambo lililoathiri utekelezaji wa miradi.

(b) Mapokezi ya fedha za ndani ni ya kuridhisha ambapo Wizara imepokea asilimia 86 ya makadirio.

(c) Kamati imebaini kuwa Wizara ilihamishiwa kiasi cha shilingi 16,196,000,000 kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuwezesha shughuli za wafanyabiashara ndogo ndogo (Machinga), zikiwemo kuwapatia mikopo nafuu na kujenga miundombinu. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2023 hakuna fedha yoyote iliyopokelewa na Wizara kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kutokutolewa kwa fedha za Machinga kwa wakati, kwa kiasi kikubwa kumeathiri utekelezaji wa mradi huu na hivyo kufifisha nia njema ya Serikali ya kuwawezesha

Machinga kwa kuwapa mikopo ya bei nafuu na kuwawekea mazingira bora ya kufanya biashara. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizi kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha mwezi Juni kwa kuwa fedha hizi ni za mkopo kutoka *ECF*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa wakati fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani kwa kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje za ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Hata hivyo, kuna baadhi ya maoni na ushauri ambayo hayakuzingatiwa ambapo ni pamoja na uhaba wa watumishi wa ustawi na maendeleo ya jamii na uchakavu wa miundombinu ya vyuo na taasisi za maendeleo pamoja na ustawi wa jamii. Kamati itaendelea kusisitiza tena masuala hayo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwa eneo la Maduhuli, Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 8,500,000,000 ikilinganishwa na shilingi 8,500,000,000 katika mwaka wa fedha 2022/2023. Hakuna ongezeko wala punguzo ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha. Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 53 unaonekana katika Jedwali Na. 4.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imeweka lengo la kukusanya kutoka kwenye vyanzo sita vya mapato.

Aidha, lengo la makusanyo lililowekwa ni sawa na lengo la mwaka wa fedha 2022/2023, hivyo lengo hilo halijaongezeka wala kupungua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kufikia asilimia 32 tu, Kamati haioni uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo ililowekwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa ni vema Serikali izingatie changamoto zinazosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na kuzingatia uhalisia katika kupanga makisio hayo. Aidha, Wizara iweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya shilingi 43,664,963,000 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 26,577,510,000 ni matumizi mengineyo na kiasi cha shilingi 17,087,453,000 fedha za mishahara. Kiasi hicho ni ongezeko la shilingi 11,353,982,000 sawa na asilimia 35 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 32,310,981,000 kama ilivyochanganuliwa katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko la bajeti ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi na pia kwa kuongezeka kwa kitengo kipya cha kuratibu makundi maalumu. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza bajeti kwenye Kitengo cha Uratibu wa Mashirika ya Kiserikali kiasi cha shilingi 1,500,000,000 ili kuimarisha ufuatiliaji wa mashirika haya. Hata hivyo, Kamati inaishauri

Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatolewa kwa wakati na kutumika vizuri kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara, imetengewa jumla ya shilingi 30,558,230,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 26,800,000,000 ni fedha za ndani, na shilingi 3,758,230,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa takribani shilingi 19,466,150,000 sawa na asilimia 175 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia kama inavyochanganuliwa katika jedwali Na. 6.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo:-

(a) Ongezeko la asilimia 175 la bajeti lipo hasa kwenye fedha kwa ajili ya kuwezesha shughuli za wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu Machinga. Kamati pia ilielezwa kuwa sababu nyingine ya kuongezeka kwa bajeti ni uandaaji wa programu ya kizazi chenye usawa Tanzania ambayo ni utekelezaji wa ahadi ya nchi iliyotoa wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa uliofanyika nchini Ufaransa.

(b) Bajeti ya fedha ya nje imepungua kwa asilimia 10. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa Wizara hii. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itatoa fedha za maendeleo kwa wakati ili kutekeleza mpango kazi wake.

Aidha, Kamati inatoa rai kwa Serikali kutotegemea fedha kutoka nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo

zimekuwa hazina uhakika wa kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

(i) Kukadiria matumizi ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo bila kuwa na mikakati madhubuti ya upatikanaji wa fedha hizo, unaathiri utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Wizara iweke mikakati ya ufuatiliaji wa mtitiriko wa fedha za maendeleo na utekelezaji wa miradi hiyo.

(ii) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni jambo linaloathiri tija iliyokusudiwa na mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo. Serikali izingatie umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kusaidia utekelezaji wa miradi hiyo na kupatikana kwa tija ya mradi iliyokusudiwa. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

(iii) Kukosekana kwa Hatimiliki za maeneo yanayomilikiwa na Vyuo na Taasisi za Maendeleo na Ustawi wa Jamii ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo na baadaye kusababisha migogoro ya umiliki. Wizara iandae mkakati maalum wa kupima na kupata hati za maeneo yote ya vyuo na taasisi zake zote za ustawi na maendeleo ya jamii.

(iv) Kutotolewa kwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Uyole na

Mlale kumekwamisha utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inashauri kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi hiyo zitolewe kabla ya kwisha kwa Mwaka huu wa fedha ili kuboresha mazingira ya vyuo hivi na kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia.

(v) Serikali iweke mkakati wa muda mrefu kuhusu namna ya kutekeleza miradi yake yote ya maendeleo ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati. Mkakati huo uainishe kila mradi na kipindi ambacho kinatarajiwa kukamilisha miradi hiyo. Aidha, katika mkakati huo, Serikali iainishe namna ambavyo miradi iliyokamilika itatunzwa na kufanyiwa ukarabati wa mara kwa mara ili kuitunza miradi hiyo.

(vi) Upungufu wa Watumishi katika Taasisi za Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa kiasi kikubwa unaathiri utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo. Kamati inashauri Serikali iweke mkakati wa dhati wa kuongeza bajeti ili kutoa ajira za kutosha katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ili kuimarisha utendaji kazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri mahsusi, kwa upande wa makundi maalumu. Kamati inapongeza Serikali kwa kuanzisha Kifungu 3003 na kukitengea kiasi cha shilingi 18,500,000,000 kwa ajili ya kusimamia na kuratibu masuala ya Makundi Maalumu wakiwemo wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu Machinga.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa pamoja na kutengwa kwa kiasi hicho cha fedha, hakuna mwongozo wa uratibu na usimamizi wa wafanyabiashara ndogo ndogo, jambo linalotaharisha matumizi ya fedha hizi. Ni vema Serikali ikaandaa kwa haraka mwongozo wa namna fedha hizo zitakavyotumika katika kuratibu, kuimarisha na kusimamia uboreshaji wa mazingira ya wafanyabiashara hao.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa moja ya changamoto kubwa katika Wizara hii ni uhaba wa watumishi. Kwa mujibu wa taarifa za Wizara kuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii 2,293 sawa na asilimia 56.7 na Maafisa Ustawi wa Jamii 20,057 sawa na asilimia 95.3 katika ngazi mbalimbali hususan kata. Maafisa hawa ni muhimu katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii kama vile huduma za unasihi na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini pia kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile usafiri kwa Maafisa kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya jamii. Kutokana na changamoto hizo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iwe na mkakati wa dhati wa kutoa ajira hususan katika Wizara hii ili kuongeza nguvukazi katika ufuatialiaji wa masuala mbalimbali ya jamii.

(ii) Serikali itenge Bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya watumishi wa Wizara, kama vile vyombo vya usafiri, kompyuta ili kuwarahisishia usafiri na kuifikia jamii kiurahisi na kutatua changamoto zao.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa nyumba za Watumishi na uchakavu wa miundombinu. Katika ziara zake za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya taasisi zilizo chini ya Wizara hii, Kamati ilibaini uchakavu wa miundombinu kama vile, majengo ya madarasa, ofisi, mabweni, uchakavu wa miundombinu katika makazi ya Wazee ya Njoro, Mahabusu ya Watoto Moshi, na upungufu wa nyumba za Watumishi. Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Serikali ihakikishe inaongeza Bajeti ya Ujenzi wa Miundombinu hiyo katika Taasisi zilizo chini ya Wizara

hii na kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge;

(ii) Kamati inashauri Wizara ihakikishe inajenga nyumba za Watumishi ili kuwaondolea adha ya makazi watumishi wanaofanya kazi katika Taasisi za Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kuongeza Bajeti ya Usimamizi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuongeza kiasi cha shilingi 1,500,000,000 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwenye kitengo cha uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, kamati ina maoni yafuatayo: -

(i) Serikali ikaongeze bajeti katika kifungu ili kufatilia kwa kina mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yapo takribani 9,025 Tanzania Bara ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yake kwa manufaa ya jamii na maslahi mapana ya Tanzania na kudhibiti changamoto kubwa ya mashirika hayo kujihusisha na kuamasisha mmong'onyoko wa maadili kinyume na mila na desturi za kitanzania na vilevile kudhibiti mienendo yote ya fedha zinazoingia katika mashirika hayo ili kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu;

(ii) Kumekuwa na mashirika yanayojiusisha na kuhamasisha mmong'onyoko wa maadili kinyume na mila na desturi za kitanzania, utakatishaji fedha haramu na baadhi ya mashirika kujihusisha na siasa wakati wa uchaguzi na kuizingatia Tanzania inaelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024. Kamati inaishauri wizara kuyachukulia hatua za haraka ikiwemo kuyafuta mashirika yote yanayobainika kujihusisha na mambo tajwa hapo juu;

(iii) Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kuendelea kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, hitimisho napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Naibu Waziri Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, Mbunge kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. John Athony Jingu na Naibu Katibu Mkuu Amon Anastaz Mpanju.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Rehema Lazarus Kipera na Ndg. Aziza Waziri Kheir wakisaidiwa na Bi. Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilisha kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizaya ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

**1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (5)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inapaswa kabla ya kuchambua Bajeti, kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.

Kanuni ya 117 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lako tukufu lijadili hoja ya Wizara ya

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Malaam pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua (**Fungu 53)** pamoja na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa wizara hii. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara za kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya fungu lililotajwa hapo juu. Uchambuzi wa Kamati ulikuwa kama ifuatavyo;-

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata wasaa wa kukagua mradi wa Ujenzi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Kisangara, Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Makazi ya Wazee Njoro na Mahabusu ya Watoto Moshi.

### 2.1 Mradi wa ujenzi katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Taasisi ilipokea kiasi cha **Shilingi 1.600,000,000** ambapo fedha hiyo ilitumika kununua na kufunga viti 1,118 katika kumbi pacha za mihadhara, ununuzi wa vitanda 292 na

makabati katika bweni la wasichana, ununuzi wa magodoro 584, ununuzi wa viti vya kusomea 584 katika bweni la wasichana, ununuzi wa podium na screen ya kufundishia na malipo ya fundi mkuu na vibarua. Aidha kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 98.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hii Kamati pia ilibaini kuwa Taasisi inaendesha miradi ya kujifunzia na uzalishaji ikiwa na lengo la kuongeza mapato na kutoa mafunzo kwa wanafunzi. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kutengeneza "Paving Blocks" mradi wa ufugaji samaki na mradi wa uchapishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza utekelezaji mzuri wa ujenzi wa miradi hii ya maendeleo na pia kwa kuwa wabunifu wa miradi ambayo itaongeza pato la ndani la chuo pia kuwapatia ujuzi wanafunzi.

Pamoja na pongezi hizo kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika chuo hiki zikiwemo zifuatazo;

i) Uchakavu wa miundombinu ya chuo; Katika ziara hii kamati ilishuhudia jinsi majengo ya chuo yalivyo chakavu kutokana na kuwa ya muda mrefu sana.

ii) Ukosefu wa bweni la Wavulana. Kutokana na chuo kuwa umbali mrefu toka mjini, kamati inashauri kuwa Serikali ione umuhimu wa kuanza ujenzi wa mabweni mapema ili kupunguza adha ya malazi.

iii) Upungufu wa Nyumba za Watumishi. Katika kutatua changamoto hii Kamati ilishauri kuwa Taasisi kwa kutumia mapato ya ndani itenge fedha kwaajili ya kuanza ujenzi wa nyumba hizi.

iv) Chuo kutokuwa na Hati Miliki ya eneo lake jambo linaloweza kuwavutia wanachi kuvamia na kusababisha migogoro ya umiliki wa ardhi. Ni rai ya Kamati kuwa Chuo kiharakishe kupima maeneo yake na kupata hati ya umiliki.

**2.2 Mradi wa ujenzi katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kisangara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 chuo kilitengewa kiasi cha **Shilingi 300,000,000** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 104 hata hivyo hadi Kamati inatembelea mradi huu hakuna fedha iliyokuwa imepelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakipongeza Chuo kwa kuaanda Mtaala wa Elimu ya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto katika ngazi ya Stashahada na tayari umeshaidhinishwa kwa Matumizi na Mamlaka ya Ufundi na Ufundi Stadi. Mpango huu unamchango mkubwa katika hatua za kudhibiti mmomonyoko wa maadili kupitia utekelezaji wa vituo vya malezi na makuzi ambavyo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa taifa wa *Generation Eguality Program*.

Aidha kwa upande mwingine Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kiasi cha **Shilingi 400,000,000** kilipokelewa na Taasisi. Hadi Kamati inatembelea mradi huu kiasi cha **Shilingi 235,821,079.70** kilikuwa kimetumika, ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa msingi, kuta, kuezeka miundombinu ya maji safi na umeme.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao umegharimu kiasi cha **Shilingi 235,821,079.70** na haionekani kulingana na thamani ya fedha iliyotumika na utekelezaji umechukua muda mrefu licha ya kupatiwa fedha zote kwa wakati. Ni rai ya Kamati kuwa miradi hii ikamilike kwa

wakati ili kuongeza thamani ya mradi na kuwasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu.

Aidha Kamati ilibaini kuwa Chuo hakina Hati Miliki ya maeneo yake jambo linalohatarisha maeneo hayo kuvamiwa na wananchi, ukosefu wa jengo la utawala na Maktaba, upungufu mkubwa wa watumishi katika kada mbalimbali, ukosefu wa maji, na upungufu wa hostel. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kutenga fedha za Bajeti ili kuweza kujenga miundombinu ya chuo hiki.

**2.3 Ukarabati wa Makazi ya Wazee Njoro na Mahabusu ya Watoto ya Moshi.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Makazi ya Wazee Njoro na Mahabusu ya Watoto Moshi. Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kiasi cha **Shilingi 200,000,000** zilitengwa kwaajili ya ukarabati wa Makazi ya Wazee Njoro lakini hadi Kamati inatembelea makazi haya hakuna fedha iliyokuwa imetolewa kwaajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara yake Kamati ilishuhudia uchakavu wa Majengo ya Mahabusu ya Watoto na Ufinyu wa Majengo, ukosefu wa Nyumba za Watumishi, ukosefu wa Eneo la Michezo kwa Watoto na Ukosefu wa Gari la kuhudumia vituo hivi. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuboresha Mahabusu ya Watoto na Makazi ya Wazee ili waweze kuishi katika mazingira mazuri na kununua Magari kwa ajili ya kutoa huduma katika maeneo hayo.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuanzisha miradi ya ufugaji ng’ombe wa maziwa, kuku, bustan katika eneo la makazi ya Wazee kwa kuwa wana eneo lenye ukumbwa wa Mita za Mraba 5226 kwaajili ya kuwawezesha wazee kujishughulisha na

kazi ndogondogo, kuboresha lishe kwa wazee na kuongeza kipato katika makazi ili kupunguza gharama za uendeshaji.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 3.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika mambo makuu manne yafuatayo;-

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

### 3.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi. 8,500,000,000** kutoka vyanzo mbalimbali kama vile Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 7,084,497,000,** uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 40,000,000**; Ada ya Malazi kwa wanafunzi wa vyuo vya maendeleo ya jamii **Shilingi 720,000,000** usajili na ada za mwaka za NGOs **Shilingi 638,500,000** na uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 15,000,000** na Mapato mengineyo **Shilingi 2,003,000 .**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 2,712,157,233** sawa na **asilimia 32** ya makusanyo yaliyokusudiwa. Makusanyo hayo yapo katika

mchanganuo ufuatao**: -** ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 1,936,671,238** sawa na **asilimia 27,** Uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 10,500,000** sawa na **asilimia 26** Ada ya malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, **Shilingi 427,784,126** sawa na **asilimia 59** Usajili na ada za mwaka za NGOs **Shilingi 318,145,869** sawa na **asilimia 50** uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 12,000,000** sawa na **asilimia 80** Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekena katika **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1: Fungu 53 Makadirio na Makusanyo halisi katika Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| MAELEZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ada za vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 7,084,497,000 | 1,936,671,238 | 27 |
| Uuzaji wa Mitaala ya Maendeleo ya Jamii | 40,000,000 | 10,500,000 | 26 |
| Ada za Malazi ya Wanafunzi wa vyuo vya Maendeleo | 638,500,000 | 318,145,869 | 50 |
| Usajili na Ada za Mwaka za NGOs | 720,000,000 | 427,784,126 | 59 |
| Uuzaji wa Mitaala vya Vyuo vya Ustawi | 15,000,000 | 12,000,000 | 80 |
| Mapato mengineyo | 2,003,000 | 7,056,000 | 352.27 |
| **JUMLA** | **8,500,000,000** | **2,712,157,233** | **32** |

**Chanzo: Randama ya Bajeti ya 2022/23 Fungu 53**

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(a) Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 2,712,157,233** sawa na **asilimia 32** ya makusanyo yote ya Wizara hii yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Wizara hii imekusanya **aslimia 32** tu ya lengo; ingawa kwa kipindi hicho ilitarajiwa angalau wawe wamefikia asilimia 65 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara hii sio ya kuridhisha kwani hadi kufika februari 2023 ni **asilimia 32** tu ya lengo imekusanywa. Kamati ilitaka kujua sabababu za makusanyo madogo kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato ambapo ilielezwa kuwa imetokana na wanafunzi wengi kutoripoti kama ilivyokadiriwa na Vyuo mathalani katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 vyuo vilikadiria kudahili wanafunzi 8,191, lakini vilifanikiwa kudahili wanafunzi 5,255; kufutwa kwa usajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali 4,898 kutokana na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za mashirika haya ambapo imeathiri makusanyo ya Mapato kutoka kwenye ada za usajili na ada za mwaka za Mashirika haya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua ya kufuta Mashirika yasisyo ya Kiserikali 4,898 ambayo yalikiuka Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za mashirika haya.

Aidha, kwa upande mwingine Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato, yanaweza kutafsiriwa kwamba au malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi; au jitihada za ukusanyaji zilikuwa

hafifu, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ipange bajeti yake kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vya mapato.

**3.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 32,310,981,000** kwa matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 18,169,057,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na **Shilingi 14,141,924,000** kwaajili ya mishahara**.** Aidha Kamati ilijulishwa kuwa Wizara ilihamishiwa kiasi cha **Shilingi 6,729,892,250** kutoka Wizara ya Fedha kwaajili ya uratibu wa Kitengo cha Makundi Maalum.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 19,175,644,557** sawa na **asilimia 59** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida**,** ambapo **Shilingi 9,667,294,223** sawa na **asilimia 68** ni fedha kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 9,508,350,333.56** sawa na **asilimia 52** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa ajili ya uratibu wa Machinga. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Fungu 53 - Mapokezi ya Fedha Matumizi ya Kawaida 2022/2023**

| **MAPOKEZI YA FEDHA MATUMIZI YA KAWAIDA 2022/2023** | | | |
|---|---|---|---|
| Matumizi | Fedha iliyotengwa 2022/2023 | Fedha zilizopokelewa | Asilimia ya mapokezi |
| Mishahara | **14,141,924,000** | 9,667,294,223 | 68 |
| Oc | 18,169,057,000 | 9,508,350,333.56 | 52 |
| Jumla | **32,310,981,000** | 19,175,644,557 | 59 |

***Chanzo: Randama ya Bajeti 2022/2023 Fungu 53***

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwaajili ya mishahara na matumizi mengineyo ya Wizara pamoja na Taasisi zake ni wa kuridhisha kwani imepokea **asilimia 59** ya fedha iliyoidhinishwa. Aidha, Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Februari 2023 hakuna Fedha iliyopokelewa kwa ajili ya uratibu wa Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga).

**Mheshimiwa Spika,** Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi, upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa wakati na kwa kadri inavyostahili ni jambo muhimu kufanikisha. Hivyo ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha hizo kwa wakati na kwa ukamirifu ili kutoathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

**3.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ilitengewa jumla ya **Shilingi 11,092,080,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,900,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 4,192,080,000** ni fedha za nje. Wizara ilihamishiwa kiasi cha **Shilingi 16,196,000,000** kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya Wafanyabiashara ndogondogo (Machinga).
Hadi kufikia Februari 2023 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 6,831,334,941** sawa na **asilimia 62.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,940,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 891,334,941** ni fedha za Nje na hakuna fedha yoyote ya Machinga iliyotolewa. Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa katika **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3: Fungu 53- Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha 2022/2023**

| **MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2022/2023** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Bajeti iliyotengwa 2022/2023** | | **Mapokezi ya fedha hadi kufikia marchi 2023** | |
| | Fedha za ndani | Fedha za nje | Fedha za ndani | Fedha za nje |
| **Na. 6290:** *Kuprogramu Mfumo wa Kompyuta na kuchakata Data* | 200,000,000 | 273,270,000 | **200,000,000** | **0** |
| **Na. 6330:** Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 5,300,000,000 | 0.00 | **4,170,000,000** | **0** |
| **Na. 6259:**Mpango wa Rasilimali kwa Program za Jinsia | | 1,833,210,000 | 1,680,000,000 | **390,651,941** |
| **Na. 5414**: Uhai na Maendeleo ya Mtoto | 0.00 | 1,574,000,000 | | **500,683,000** |
| **Na.5451:** Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii | 1,400,000,000 | 511,600,000 | **90,000,000** | **0** |
| **Jumla Kuu** | **6,900,000,000** | **4,192,080,000** | **5,940,000,000** | **891,334,942** |

***Chanzo. Randama ya Bajeti 2022/2023 Fungu 53***

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo;

(a) Kwa jumla mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichopangwa kupokelewa ambapo ilipokelewa **asilimia 21** tu ya makadirio jambo lililoathiri utekelezaji wa miradi.

(b) Mapokezi ya fedha za ndani ni ya kuridhisha ambapo Wizara imepokea **asilimia 86** ya makadirio.

(c) Kamati imebaini kuwa Wizara ilihamishiwa kiasi cha **Shilingi 16,196,000,000** kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuwezesha shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga) zikiwemo kuwapatia mikopo nafuu na kujenga miundombinu. Hata hivyo hadi kufikia Februari 2023 hakuna fedha yoyote iliyopokelewa na Wizara kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, kutokutolewa kwa fedha za Machinga kwa wakati, kwa kiasi kikubwa kumeathiri utekelezaji wa mradi huu na hivyo kufifisha nia njema ya Serikali ya kuwawezesha Machinga kwa kuwapa mikopo ya bei nafuu na kuwawekea mazingira bora ya kufanya biashara. **Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizi kabla ya Mwaka huu wa Fedha kuisha Mwezi Juni kwa kuwa fedha hizi ni za mkopo kutoka ECF.**

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa mapokezi wa fedha za nje za kutekeleza miradi ya maendeleo uko chini ukilinganisha na fedha za ndani. Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa wakati fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani kwakuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua.

### 3.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Hata hivyo, kuna baadhi ya maoni na ushauri ambayo hayakuzingatiwa ambayo ni pamoja na Uhaba wa Watumishi wa Ustawi na Maendeleo ya Jamii na uchakavu wa miundombinu ya Vyuo na Taasisi za Maendeleo pamoja na Ustawi wa Jamii. Kamati itaendelea kusisitiza tena masuala hayo kwenye taarifa hii.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 4.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 8,500,000,000** ikilinganishwa na **Shilingi 8,500,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Hakuna ongezeko wala punguzo ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo ni pamoja na**:** Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 7,084,497,000,** uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 40,000,000**; Ada ya Malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 720,000,000** usajili na ada za mwaka za NGOs **Shilingi 638,500,000** na uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 15,000,000** na Mapato mengineyo **Shilingi 2,003,000.** Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 53 unaonekana katika **Jedwali Na.4** hapa chini.

**Jedwali Na. 4: Fungu 53- Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli**

| CHANZO | 2022/2023 (Tsh.) | 2023/2024 (Tsh.) | Nyongeza/ Pungufu (Tsh.) | Nyongeza/ Pungufu (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ada za vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 7,084,497,000 | 7,084,497,000 | 0 | 0 |
| Uuzaji wa Mitc Maendeleo ya Jamii | 40,000,000 | 40,000,000 | 0 | 0 |
| Ada ya Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 720,000,000 | 720,000,000 | 0 | 0 |
| Usajili wa ada za mwaka za NGOs | 638,500,000 | 638,500,000 | 0 | 0 |
| Uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Ustawi | 15,000,000 | 15,000,000 | 0 | 0 |
| Mapato Mengineyo | 2,003,000 | 2,003,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **8,500,000,000** | **8,500,000,000** | **0** | **0** |

***Chanzo. Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 53***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati unaonyesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara imeweka lengo la kukusanya kutoka kwenye vyanzo vyake 6 vya mapato. Aidha, lengo la makusanyo lililowekwa ni sawa na lengo la Mwaka wa Fedha 2022/2023 hivyo lengo hilo halijaongezeka wala kupungua.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kufikia **asilimia 32** tu hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya muda wa lengo. Kamati haioni uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo ililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa ni vema Serikali izingatie changamoto zilizosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na kuzingatia uhalisia katika kupanga makisio hayo. Aidha Wizara iweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato.

**4.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 43,664,963,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shlingi 26,577,510,00** ni matumizi mengineyo na kiasi cha **Shilingi 17,087,453,000** fedha za Mishahara. Kiasi hicho ni ongezeko la **Shilingi 11,353,982,000** sawa na **asilimia 35** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 32,310,981,000.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 18,169,057,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 14,141,924,000** kwa ajili ya mishahara kama ilivyochanganuliwa katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**

| ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 65 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **2022/2023 (tsh.)** | **2023/2024 (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (%.)** |
| Mishahara | 14,141,924,000 | 17,087,453,000 | 2,945,529,000 | 21 |
| OC | 18,169,057,000 | 26,577,510,000 | 8,408,453,000 | 46 |
| **Jumla** | **32,310,981,000** | **43,664,963,000** | **11,353,982,000** | **35** |

***Chanzo. Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 53***

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imeongezeka kwa **asilimia 35** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Shilingi 32,310,981,000**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi na pia kwa kuongezeka kwa Kitengo kipya cha kuratibu Makundi Maalumu.

Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza bajeti kwenye Kitengo cha Uratibu wa Mashirika ya Kiserikali kiasi cha **Shilingi 1,500,000.000** ili kuimarisha ufuatiliaji wa mashirika haya.

Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatolewa kwa wakati na kutumika vizuri kwa manufaa ya Nchi.

**4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwaajili ya Miradi ya Maendeleo.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara, imetengewa jumla ya **Shilingi 30,558,230,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,800,000,000** ni fedha za ndani, na **Shilingi 3,758,230,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa takribani **Shilingi 19,466,150,000** sawa na **asilimia 175** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha kama ilivyochanganuliwa katika **Jedwali Na. 6**.

**Jedwali Na. 6: Fungu Na. 53 Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**

| **ULINGANISHO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2022/2023 NA 2023/2024** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Makadirio kwa mwaka 2022/2023** | | **Makadirio kwa mwaka 2023/2024** | |
| | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Fedha za Ndani | Fedha za Nje |
| **Na. 6290:** Kuprogramu Mfumo wa Kompyuta na kuchakata Data | 200,000,000 | 273,270,000 | 200,000,000 | 200,000,000 |
| **Na. 6330:** Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 5,300,000,000 | 0.00 | 2,100,000,000 | **00** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na. 6259:**Mpango wa Rasilimali kwa Program za Jinsia | 00 | 1,833,210,000 | 4,000,000,000 | **1,257,993,831** |
| **Na. 4952**: Uhai na Maendeleo ya Mtoto | 0.00 | 1,574,000,000 | | **1,253,236,169** |
| **Na. 6280:** Uratibu wa Makundi Maalum | 16,196,000,000 | 0 | **18,500,000,000** | **0** |
| **Na.5451:** Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii | 1,400,000,000 | 0 | **1,000,000,000** | **1,047,000,000** |
| **Jumla Kuu** | **6,900,000,000** | **4,192,080,000** | **26,800,000,000** | **3,758,230,000** |

***Chanzo. Randama ya Bajeti 2022/2023 Fungu 53***

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo;-

(a) Bajeti ya Maendeleo imeongezeka wa **asilimia 175** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Ongezeko hilo lipo hasa kwenye Fedha za kwa ajili ya kuwezesha shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga). Kamati pia ilielezwa kuwa sababu nyingine ya kuongezeka kwa Bajeti ni uandaaji wa programu ya kizazi chenye usawa Tanzania ambayo ni utekelezaji wa ahadi ya nchi iliyotoa wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa uliofanyika nchini Ufaransa.

(b) Bajeti ya Fedha ya Nje imepungua kwa **asilimia 10,** ambapo kwa Mwaka 2022/2023 ilitengwa kiasi cha **Shilingi 4,192,080,000** na katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imetengwa kiasi cha **Shilingi 3,758,230,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa Wizara hii. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itatoa fedha za maendeleo kwa wakati ili kutekeleza mpango kazi wake.
Aidha kamati inatoa rai kwa Serikali kutotegemea fedha kutoka Nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo hazina uhakika wa kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo: -

i) Kukadiria matumizi ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo bila kuwa na mikakati madhubuti ya upatikanaji wa fedha hizo unaathiri utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Wizara iweke mikakati ya ufuatiliaji wa mtitiriko wa fedha za maendeleo na utekelezaji wa miradi hiyo.

ii) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni jambo linaloathiri tija iliyokusudiwa na mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo. Serikali izingatie umuhimu wa

kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kusaidia utekelezaji wa miradi hiyo na kupatikana kwa tija ya mradi iliyokusudiwa. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo nchini.

iii) Kukosekana kwa Hati Miliki za maeneo yanayomilikiwa na Vyuo na Taasisi za Maendeleo na Ustawi wa Jamii ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo na baadae kusababisha migogoro ya umiliki. Wizara iandae mkakati maalumu wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Vyuo na Taasisi zake zote za Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

iv) Kutotolewa kwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Uyole na Mlale kumekwamisha utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inashauri kuwa fedha zilizotengwa kwaajili ya miradi hiyo zitolewe kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa fedha ili kuboresha mazingira ya vyuo hivi na kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia.

v) Serikali iweke mkakati wa muda mrefu kuhusu namna ya kutekeleza miradi yake yote ya maendeleo ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati. Mkakati huo uainishe kila mradi na kipindi ambacho kinatarajiwa kukamilisha miradi hiyo. Aidha, katika mkakati huo, Serikali iainishe namna ambavyo miradi iliyokamilika itatunzwa na kufanyiwa ukarabati wa mara kwa mara ili kuitunza miradi hiyo.

vi) Upungufu wa Watumishi katika Taasisi za Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa kiasi kikubwa unaathiri utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo. Kamati inashauri Serikali iweke mkakati wa dhati wa kuongeza bajeti ili kutoa ajira za

kutosha katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ili kuimarisha utendaji kazi wa Wizara hii.

## 5.2 Maoni na Ushauri Mahsusi

### 5.2.1 MAKUNDI MAALUMU

Kamati inapongeza Serikali kwa kuanzisha Kifungu 3003 na kukitengea kiasi cha **Shilingi 18,500,000,000** kwa ajili ya kusimamia na kuratibu masuala ya Makundi Maalumu wakiwemo Wafanyabiashara ndogondogo (Machinga). Hata hivyo Kamati imebaini kuwa pamoja na kutengewa kiasi hicho cha Fedha, hakuna mwongozo wa uratibu na usimamizi wa Wafanyabiashara ndogondogo jambo linalotaharisha matumizi ya fedha hizi. Ni vema Serikali ikaandaa kwa haraka mwongozo wa namna Fedha hizo zitakavyotumika katika kuratibu, kuimarisha na kusimamia uboreshaji wa mazingira ya wafanyabiashara hao.

### 5.2.2 UHABA WA WATUMISHI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa moja ya Changamoto kubwa katika Wizara hii ni Uhaba wa watumishi. Kwa mujibu wa taarifa za Wizara kuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii **2,293** sawa na **asilimia 56.7** na Maafisa Ustawi wa Jamii **20,057** sawa na **asilimia 95.3** katika ngazi mbalimbali hususan Kata. Maafisa hawa ni muhimu katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii kama vile huduma za unasihi na ustawi wa jamii.

Kamati imebaini pia kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile usafiri kwa Maafisa kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ya jamii. Kutokana na changamoto hizo kamati inatoa ushauri ufuatao: -

i. Serikali iwe na mkakati wa dhati wa kutoa ajira hususani katika Wizara hii ili kuongeza nguvukazi katika ufuatialiaji wa masuala mbalimbali ya jamii.

ii. Serikali itenge Bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya watumishi wa wizara, kama vile vyombo vya usafiri, kompyuta nk ili kuwarahisihia usafiri na kuifikia jamii kiurahisi na kutatua changamoto zao.

### 5.2.3 UHABA WA NYUMBA ZA WATUMISHI NA UCHAKAVU WA MIUNDOMBINU

Katika ziara zake za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kamati ilibaini uchakavu wa miundombinu kama vile, majengo ya madarasa, ofisi mabweni; Uchakavu wa miundombinu katika Makazi ya Wazee ya Njoro, Mahabusu ya Watoto Moshi, na Upungufu wa Nyumba za Watumishi. Kamati inatoa maoni Na ushauri ufuatao: -

i. Serikali ihakikishe inaongeza Bajeti ya Ujenzi wa Miundo mbinu hiyo katika Taaisis zilizochini ya Wizara hii na kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyiidhinshwa na Bunge.

ii. Kamati inashauri Wizara ihakikishe inajenga nyumba za Watumishi ili kuwaondolea adha ya makazi watumishi wanaofanya kazi katika Taasisi za Wizara hii.

### 5.2.4 KUONGEZA BAJETI YA USIMAMIZI WA MASHIRIKA YASIYO YA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuongeza kiasi cha **Shilingi 1,500,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwenye kitengo cha uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Kamati ina maoni yafuatayo;-

i. Serikali kuongeza Bajeti katika Kifungu hiki ili kufuatilia kwa kina Mashirika yasisyo ya Kiserikali ambayo yapo takribani

9,025 Tanzania Bara ili kuhakikisha yanatekeleza majukumu yake kwa manufaa ya jamii na maslahi mapana ya Tanzania na kudhibiti changamoto kubwa ya Mashirika haya kujihusisha na kuhamasisha mmomonyoko wa maadili kinyume na mila na desturi za kitanzania na vilevile kudhibiti mienendo yote ya fedha zinazoingia katika mashirika haya ili kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu.

ii. Kumekuwa na Mashirika yanayojihusisha na kuhamasisha mmomonyoko wa Maadili kinyume na mila na Desturi za Kitanzania; Utakatishaji Fedha haramu na Baadhi ya Mashirika kujihusisha na siasa wakati wa uchaguzi na ukizingatia Tanzania inaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2024. Kamati inashauri Wizara kuyachukulia hatua za haraka ikiwemo kuyafuta Mashirika yote yanakayobainika kujihusisha na mambo tajwa hapo juu.

iii. Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kuendelea kufanya marekebisho.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe.Fatma Hassan Toufiq, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe.Riziki Said Lulida, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe.Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe.Tecla Mohammed Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Maimuna Salum Mtanda, Mb.
8. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
9. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
10. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
11. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
12. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb.
13. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
14. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
15. Mhe. Alli Hassan Omar King, Mb.
16. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
17. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
18. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
19. Mhe. Toufiq Salim Hassan Turky , Mb.
20. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
21. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mhe. Mwanaidi Ali Khamis, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiaono walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. John Antony Jingu na Naibu Katibu Mkuu Amon Anastaz Mpanju.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Rehema Lazarus Kipera na Ndg.Aziza Waziri Kheir wakisaidiwa na Bi. Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Riziki Said Lulida, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
18 Mei, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumeisha sikia maoni ya kamati kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri na sasa tunaanza uchangiaji. Ninayo majina hapa ya wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii tutaanza na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji atafuatia na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi kwa jitihada zao wanazozichukua katika Wizara hii wanafanya kazi sana usiku na mchana kutokana na shughuli zetu hasa hizi za wanawake na watoto pamoja na maendeleo mengine yaliyokuwemo humu nchini, nakushukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kwanza nizungumzie kuhusu suala la mgogoro wa ndoa. Mgogoro wa ndoa hapa nchini, wamefanya jitihada katika taarifa yao humu nimeisoma wamefikia malengo makubwa lakini bado, bado katika kazi ya hii inaendelea mgogoro huu wa ndoa, bado wanawake wananyanyasika ndani ya ndoa zao. Kwa sababu kama mnavyojua hii nchi yetu ni kubwa ina mambo mengi mengi tu kuhusu wanawake na hasa masuala ya ndoa bado nazidi kuzungumzia kwamba wanawake wanajitihada kubwa, ndoa zao na wanajitahidi kwamba wakae na ndoa zao ndani ya majumba yao ili wakae na waume zao ndani ya majumba yao na watoto wao.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake wananyanyasika kutokana na hizi ndoa ndani ya nyumba. Wanajitahidi na wanahangaika huku na kule, wanachukua mpaka mitaji yao ili ndoa zao zidumu lakini bado, bado kabisa. Mheshimiwa Waziri hili suala litizame kwa kina juu ya Serikali yetu lizidi kuchukua fursa hii ya kuweza kukaa na hawa wanawake wetu wa ndoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuhusu wanawake, wanawake wamepatiwa fursa ya kujengewa uwezo wa kupatiwa elimu ya kodi, urasilimishaji wa biashara, hifadhi. Lakini kutokana na biashara hizo wanazozifanya waliyopatiwa kweli hii

fursa ya kujengewa uwezo lakini na wao pia tasema bado fursa ingali ndogo.

Mheshimiwa Spika biashara zao wanapokuwa wanazifanya hawana masoko ya uhakika japokuwa humu mmeandika kwamba yapo masoko wafanye mpaka China imefika kusema humu lakini wengine hawana uwezo huo wa kufanyia biashara zao wakafikia malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, wanawake bado vilevile tunanyanyasika humu nchini kutoka na biashara zetu tunazozifanya ni biashara ndogo, ndogo hazikidhi kufikia malengo mpaka wakafikia hatua ya kupata masoko ya uhakika ili kufanya biashara zao wakaendelea kufanya vizuri kwenye biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazunguzia kuhusu udhalilishaji sasa, kuhusu udhalilishaji Mheshimiwa Waziri pia umeuzungumzia humu kweli mmechukua hatua kubwa za udhalilishaji lakini bado udhalilishaji umeongezeka kama watu waliyoambiwa kafanyeni makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanawanyanyasa watoto wetu, wanawanyanyasa wanawake kijinsia bila tatizo hata kama mtu kapata ule uthibitisho kwamba huyu kweli kanyanyasika. Hili sasa hivi ndiyo linalonishughulisha, anakwenda kunyanyaswa mwanamke au wananyanyasa Watoto wetu kijinsia lakini akienda zake Mahakamani anachukuliwa dhamana yule mfanyaji wa kile kitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli hapa siye tutafika mahali? Hatufiki mahali kwa sababu tayari kaishachukuliwa hatua yule mwanaume atoke aende zake akakae nje, sijui kama aende akabake tena? au sijui akajitetee kivipi? Lakini hili suala bado halijawa zuri hapa nchini kwetu ingali lina nyanyasa watoto

wetu na wanawake na anapochukuliwa dhamana huyu anakwenda zake, anakwenda kufanya vitendo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri bado hili suala halijafikia malengo kabisa, halijafikia malengo na nasema hapa Mheshimiwa Condester, alisema hapa juzi kuna pombe hizi watu wa humu wanapokunywa wanakuwa hawana nguvu za kiume. Kwa nini hawapewi ili wakatoka hizi nguvu za kiume? Tukatokana na hili suala lililokuwa tunalo hapa nchini, wapewe wanywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana kuhasiwa hawataki, kuhasiwi lakini wapewe hizi pombe wanywe ili wakatike nguvu za kiume labda tunaweza kupata suluhisho la hawa watoto wetu kunyanyasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba chonde chonde hili suala bado kabisaa halijafanyiwa kazi na huko nje bado watoto wetu wananyanyasika hizi pombe hizi wapewe ili waweze kuvunjika nguvu za kiume na watoto wetu waweze kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naunga mkono hoja, asilimia mia moja Wizara hii ya Wanawake na Watoto hapa tulipo hivi sasa hivi tunaipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kabla atujaendelea na uchangiaji kuna wageni ambao wako hapa Bungeni na hawakupata nafasi ya kutangazwa asubuhi.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Chemba, hawa ni Madiwani, nimeambiwa tulitangaza

kwamba wanatoka Dodoma, lakini hawa wanatoka Chemba. Madiwani kutoka Chemba, haya pengine wameishatoka.

Pia nimeletewa ujumbe hapa wageni wa Mheshimiwa Neema Mwandabila, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni wengine ambao nimeletewa taarifa zao hapa, wageni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ambao ni Mabalozi wa Kupinga na Kutokomeza Ukatili nadhani hawa niliwatangaza, lakini hawa wengine hawakuwepo. Hawa ambao wameingia sasa ni kutoka Taasisi ya *FAGDI* wakiongozwa na Mkurugenzi wao Ndugu Saimon J. Kobu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni sita kutoka Dawati la Jinsia la *Mwanza City College*, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 29 wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Makete, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, viongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru iliyopo Arusha karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 70 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE) Campus* ya Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo yaliyokuja, lakini kuna jambo lingine la muhimu kabla hatujaendelea na michango yetu nitumie fursa hii kuwapongeza sana Yanga kwa ushindi wa jana wameliwakilisha vizuri Taifa letu, wamepeperusha bendera vizuri

na tunawatakia kila la kheri kwenye fainali zilizo mbele yao. Tunaamini wataleta kombe safari hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya pongezi hizo. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila na Mheshimiwa Ali Hassan King ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nianze kwa kupongeza Wizara na hasa Waziri Gwajima na Naibu wake angalau tunaanza kusikia wizara wanasema inawaka waka, kuna amsha amsha ndani ya wizara, hata hivyo ni bado muendelee.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia hili suala sasa hivi limeota mizizi na hasa kwa wazazi ambao ni baba na walimu. Hawa walimu tuna wakabidhi watoto lakini sasa hivi limeibuka kweli hili wimbi walimu wakabidhiwa watoto ili wakawafundishe lakini imetokea walimu hao ndiyo wanawabaka watoto, walimu wana wabaka wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi wa tatu mpaka wa nne kuna kesi sita za walimu wanawabaka wanafunzi, sasa wazazi wanajiwaza hivi hao watoto tunawapeleka wapi? Ukienda makanisani shida, misikitini shida hata shuleni. Kwa hiyo, suala la wazazi na hasa baba, baba mzazi wa mtoto kujiusisha kumbaka mtoto mpaka anampa mimba hili suala limekuwa ni zito sasa nini nataka kusema hapo?

Mheshimiwa Spika, ifikie wakati sasa na ndiyo maana Waziri wa Katiba alijibu hapa ilifikie wakati kama alivyosema Mheshimiwa Mwantumu, suala hili la ubakaji na ulawiti hawa watu wasipewe kabisa dhamana, hawa watu wasipewe dhamana waendelee kukaa ndani hata kama hizo kesi zinakaa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Hakimu wa Kilolo aliyemfunga yule mwanamme aliye mbaka mtoto wa dada yake kifungo cha Maisha. Lakini kifungo cha maisha hakitoshi yule alitakiwa anapoingia gerezani atandikwe viboko kumi na mbili halafu ndiyo aingie huko lakini kule bado mwili wake haujajeruhiwa ndiyo maana tunasema hawa watu wapewe adhabu kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwauliza baadhi ya Wabunge mistari kama mitatu hivi hapa nyuma nikasema hebu chagueni adhabu kati ya kunyongwa au kuasiwa? Wakasema afadhali kunyongwa sasa inamaana hao wanapenda sana waendelee kubaka au kulawiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, chakufanya hapa bora hawa wahasiwe ile wanayoikataa ndiyo tuiweke huko, wakihasiwa hili janga litapungua na wale wa sheria hao mnapoenda kujadili mmeniahidi kwamba mtaleta mswada. Tunaomba mlete muswada wa sheria kali, sisi tunaogopa nini? Mbona wenzetu wanawanyonga kabisa ni aibu, ni aibu sana maana yake tunalisema, tunalisema lakini watu wanaendelea tu, kila siku unapata hizi kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo nimelisema kwa uchungu na tuanze na hawa walimu wanao lawiti watoto. Hawa ndiyo wawe mfano kwenye hizi adhabu kali, ni mwalimu lakini kwa hilo nasema tuanze na walimu na baba wazazi wanaofanya hicho kitendo leteni huo mswada haraka sana ili turekebishe hayo mambo, dhamana isiwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana wakitoka nje kama wamepewa dhamana wanaenda kushirikiana na ndugu hata wazazi wanakaa pamoja, kesi ile inafutika, tume ziwe zinaundwa kucheki…

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kuna taarifa, sijajua ni wapi?

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN. RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, inatoka hapa kwa Mheshimiwa Ramadhan.

**SPIKA:** Ahaa jirani yako. Mheshimiwa, haya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan.

**TAARIFA**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN. RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa kwa ruska yako mzungumzaji kabla ya mwaka 2018 Zanzibar kwenye Sheria yake ya *Penal Code* (Kanuni za Adhabu) makosa ambayo yalikuwa na dhamana yalikuwa matano tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya 2018 tukafanya marekebisho ya sheria yakaongezwa kutoka matano mpaka kumi na moja kwenye Sheria za Mwenendo wa Adhabu *(Criminal Procedure)* za Zanzibar. Miongoni mwa makosa ambayo yaliwekwa yasiwe na dhamani ni makosa ambayo mchangiaji anayasema. Kwa kiasi kikubwa hii taarifa imsadie kwa kiasi kikubwa tumepunguza wimbi la makosa haya kwa sababu ya ukali wa washeria zetu zilizoko Zanzibar. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, naipokea ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Ramadhan. Sasa nilikuwa nasema kuna ndugu akienda kuambiwa huyo mtoto

wako, tukae chini tulimalize hili wanakubali. Ndugu na wale watumishi na polisi wanaohusika katika kuhakikisha kwamba kesi hizi zinaishia huko mitaani nao waingizwe kwenye hiyo adhabu wafungwe maisha na wao wahasiwe pia tukifanya hivyo watajua hee sasa hivi hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye hili suala la elimu ya jamii, kwa kingereza wanaita *sociology of education*. Mambo yanayofundishwa au niseme haya mambo yanayaofundishwa kwenye *sociology of education* vyanzo vyake ili mtoto aelewe, apate hiyo elimu ya jamii, anaipata kwenye familia, anapata shuleni, anapata kwenye rika, anapata kwenye *media,* anapata kwenye *NGO,* anapata kwenye vyombo vya dini.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi, vyombo hivi, hivi vyanzo hivi vikitoa elimu potofu au vikitoa elimu mbaya inamuathiri mtoto kwenye jamii wakitoa elimu nzuri inamsadia mtoto kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sasa hivi, katika hivi nilivyovitaja hivi vyanzo, *media* ikitoa kitu kibaya mnasikia hata Bunge tunakemea. Lakini leo hii naomba niliseme kwa faida ya watoto wetu. Kuna wakati mwingine elimu inayotolewa kwenye hizi dini zetu ni elimu ya uongo tunasika, vyombo vya dola wapo, Wizara ya elimu ipo, maendeleo ya jamii wapo. Watu wanafundishwa kwamba mtu unaenda mbinguni unaoana na Mungu. Watu wanafundishwa kwenye madhehebu kwamba humu ndani kuna mtu alikufa sasa hivi amefufuka yuko kwenye hiki chumba, kwa nini polisi wasiende kumtoa huyo mtu aliyekufa kwenye hicho chumba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunafundishwa vitu vya uongo watu wanavichukua na wakati mwingine mimi naona kama ni ujambazi na kupora fedha za watu. Suala hili tuliangalie; kutangaza elimu za uongo kwa kutumia madhehebu ya dini lazima Serikali tukae macho.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani? haya yanayotokea nchi za jirani tukae chonjo, yanayotokea nchi za jirani yanaweza yakatokea hata Tanzania. Nasema tujipange, Wizara zinazohusika zihakikishe elimu zinazotolewa kwenye hivi vyanzo ziwe elimu za ukweli.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalize dakika mbili tu, *please!*

**SPIKA:** Dakika moja malizia.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, dakika moja. Niwaombe Wizara hebu angalieni sheria ya jamii inasemaje kuhusu watoto wadogo wanaoajiriwa majumbani. Inasemaje sheria? Wanapataje haki zao au wanastahili kweli kuajiriwa wakiwa watoto wadogo? Na sheria za wafanyakazi wa majumbani bado. Ongea na Wizara ya Kazi na Ajira, mjipange muone kwamba hakuna unyanyasaji kwa watoto wanaoajiriwa wakiwa wadogo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Hassan Omar King, Mheshimiwa Mwatatu Mbarak Khamis ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi leo hii asubuhi na mimi niweze kuchangia katika Wizara yetu hii ya msingi kabisa na ya muhimu.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa Wizara hii ni Wizara kwa kweli ambayo imebeba dhamana kubwa ya Taifa letu katika kuhakikisha usalama wa nchi yetu kimaadili, kiuchumi na kuweza kusaidia mambo mbalimbali ya Taifa hili yaweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa-*support* Wizara hii, na amekuwa akiendela kuwapa *support;* nadhani ni vile kwa sababu na yeye ni mtaalamu wa maendeleo ya jamii; kiukweli angalau tunaona Wizara hii inaendelea kuonekana machoni pa Watanzania. Na pia Mheshimiwa Waziri Gwajima na Naibu wake na timu nzima yake ya uendeshaji wamekuwa wakiendela kupambana kuhakikisha angalau afua za maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii zinakuwa zinajulikana katika makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaongelea nitapenda nijikite sana kwenye masual ala *NGO;* na niseme tu, uwepo wa *NGO* katika nchi yetu umetusaidia katika meneo mbalimbali. Niseme, kwamba tunafahamu kama Taifa tunakabiliwa na changamoto mbalimbali hususani za kimaadili. Tunaona kiwamba kuna masuala ya ushoga ambayo sasa hivi ndio yana-*hit,* na yamekuwa yakitupa *stress* Watanzania wengi, kuona kwamba jambo hili ni kitu kisichokubalika, ni kitu ambacho kinatweza utu wetu na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona kuna changamoto ya dawa za kulevya, kitu ambacho kipo. Kiko *underground* lakini ukiweza kufuatilia wataalamu wanaoshughulika na masuala ya dawa za kulevya utagundua kwamba ni kitu kiko kikubwa lakini bado watanzania kama watanzania hatujakipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna biashara ya ngono. Ni kitu ambacho kimendelea kushamiri; na biashara yoyote haiwezi kushamiri kama hakuna wateja. Lakini pia kuna suala la ubakaji na ualawiti ambalo limekuwa likiendelea katika jamii yetu.Hili suala limeenda mbali, kwenye shule zetu tumekuwa tukipata tarifa mbalimbali ambazo wataalamu wa ustawi wa jamii wamekuwa wakiendelea kufuatilia na kubaini kwamba zipo shule ambazo watoto wengi wameweza kuharibiwa na wameweza kushirikishwa katika matendo haya ya ngono ambayo ni ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu, na nitoe masikitikop yangu hapa, niliweza kupata taarifa kutoka kwenye shule moja inaitwa Haloli Mbozi, kwamba watoto 30 kati ya watoto wa darasa la tatu na la nne walibainika kuwa wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono; wengine wamelawitiwa na wengine wamebakwa. Na wale wanaobainika wamefanya matendo haya mpaka leo sijasikia kauli wamefanyiwa nini?

Mheshimiwa Spika, niseme tu, kulingana na changamoto hizi tumekuwa na *NGO* ambazo zinafanya kazi nzuri na zinahitaji kupongezwa. Wamekuwa wakiendelea kuwabaini na kuwatambua waathirika wa matendo haya yote ya ukatili au matendo haya ya hovyo ambayo yamekuwa yakiendelea. Wametengeneza afua ambazo wanaendelea kuwabadili kitabia na kuwasaidia kiuchumi, na hawa watu wanakuwa wanafanya wanabadilika kitabia na kuweza kusimama binafsi na kuachana na matendo ambayo yanakuwa hayana maadili mema kwa nchi yetu. Kwa taasisi hizi nazipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kumekuwepo na *NGO* ambazo Mheshimiwa Mwakyembe aliweza kuongea kwa huzuni sana. Alisema kwamba tuna *NGO* nyingi ambazo zimeeendelea kuwafundisha Watanzania ushiriki wa ngono za jinsia moja. Sasa, ninapata hofu kwamba kama Taifa tunakuwa

na *NGO* ambazo zimeingia mpaka zimefika *site* zimefanya kazi, zimewafundisha watu ushoga na kama Taifa hatuna habari; mpaka wanakuja wanaharakati ndio wanaenda kuibua. Ninapata shaka na usalama wa nchi yetu kwamba kama hii ni ushoga tu taasisi nyingi zimeshapewa fedha na zimeshafanya kazi nzito na hakuna kilichokuwa kinaeleweka mpaka wanaharakati, ninapata hofu kubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kama huu ni ushoga umefanya hivi, je, mambo mengine yanayohatarisha hali ya usalama wa nchi yetu hali ikoje? Na hii inaonesha kuna ulegevu wa ufatiliaji wa *NGO* hizi. Kwa hiyo nilitamani Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja atuambie, baada ya kauli zile nzito za Mheshimiwa Mwakyembe kwenye lile kongamano na yule mwanaharakati ambaye alikuwepo pale, Catherine Kahabi, wamefanya nini kuhakikisha kwamba kauli zile kama zina uhalisia au hazina uhalisia, au ijoke? Kwa hiyo kwenye hili nitamtaka Mheshimiwa Waziri aje na kauli atuambie ilikuwaje na imekuwaje mpaka leo tunakuwa na miongozo ambayo inaelekeza namna ya watu kuwasiliana wanaume wa jinsia moja, yaani jinsi ya kufanya mapenzi na *practical* zao? kwa sababu zile tuhuma ni nzito sana kwa nchi yetu. Kwa hiyo nilitamani Mheshimia Waziri aje atuambie.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine ambacho nataka nikiongelee nataka niongelee dhamana ya maadili ya Taifa letu. Kwamba tunataka kuiacha dhamana ya maadili kwa watu ambao si watu wa Taifa letu. Yaani imagine *NGO's* kutoka mataifa mengine ndio wanakuja kuanza kubadili tabia za watu wetu ama kuzitengeneza tabia za watu wetu. Kwa hiyo ninatamani kada ya ustawi wa jamii ipewe kipaumbele. Ni kada ambayo inasahaulika sana. Yaani unakuta unapoongelea maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii, Wizara imejikita kwenye masuala ya maendeleo ya jamii tu. Ustawi wa jamii hausemwi. Ukiangalia ukienda ufuatilia bajeti ya ustawi wa jamii ndani ya

Wizara hii unaweza ukakuta *ceiling* ni ndogo sana; na nilitamani Waziri atakapokuwa anakuja mwishoni kuhitimisha atuambie kwenye ajira hizi 800 za maendeleo ya jamii zilizotangazwa ndani yake ustawi wa jamii ni ngapi?

Mheshimiwa Spika, haiwezekaniki ajira 800 kutoka Wizara moja ziwe za kada moja watu wa ustawi wa jamiii hawapewi hizo nafasi. Asilimia 95.3 ni upungufu. Yaani katika hali ya kawaida utaona kabisa kama nchi hatuna uelekeo kwenye suala la kulinda zile *values* za nchi yetu. Kwa hiyo kwenye hilo Waziri pia nitamtaka mwishoni atuambie ana mkakakti gani wa kuhakikisha ajira za ustawi wa jamii zinaongezwa? na ikiwezekana kama kunakuwa na sintofahamu kwenye wizara kati ya ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii ustawi wa jamii ipewe iwe *institution,* yaani inayojitegemea. Ikiwa idara maalumu inayojitegemea tunaamini itakuwa na uongozi wake na hata *management* ya masuala ya ustawi wa jamii kwa nchi hii yataenda vizuri. Tunafahamu ni kada mtambuka ustawi wa jamiii inagusa Wizara nyingi, lakini itakapokuwa kwenye idara moja ambayo inajitegemea tunaamini *management* yake itakuwa ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, *imagine* wengine wako Wizara ya ndani, wengine wako sijui wako TAMISEMI, wengine sijui wako kwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo niseme tu kwenye hili nitatamani kumsikia Waziri anatuambia nini kuhusu kuisimamisha kada ya ustawi wa jamii ili iweze kufanya kazi yake vizuri na kuwa na bajeti ya kutosha ili iweze…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili ilishagonjwa Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niseme ninashukuru sana kwa nafasi na naunga hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Shukrani. Mheshimiwa Ally Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka ajiandae.

**MHE. ALLY HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutujaalia siku ya leo uzima kuja kujadili mambo yanayohusiana na bajeti ya Wizara hii ambayo inahusika zaidi na watu.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nilikuwa niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao waliotangulia hapa kuzungumza, naona hii *group* hii ya wanaume imeandamwa sana. Maana katika *group* hii *members* wengi kwanza walishame–*left,* sasa bado inakamatwa kwamba wapewe pombe wazidi ku*leftis*hwa *(to left)* wengine watabakia wangapi? *Members* wengi walisha-*left* katika hili *group* jamani. Msiwe na wasiwasi sana kuna visukari huko mtaani.

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza niipongeze sana Serikali na nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais katika makundi maalumu, hasa kwa kuwajali kundi hili ambalo linaloitwa wamachinga. Tumeanzisha *sub vote* ya wamachinga kwa ajili ya maendeleo ya wafanya biashara ndogondogo ambao tunaamini kwamba kwenye *sub vote* hii itakwenda kuwasaidia. Lakini pamoja na pongezi hizi za kuanzisha *sub vote* hii, mwaka uliopita tumepeleka bilioni 22 kwenye msimu huu ambao tunaumaliza, na safari hii tunapeleka bilioni 20 nyingine kwa ajili ya wamachinga. Kwa hiyo hii mimi ninawapongeza sana Serikali kwa kuliona kundi hili, hapo pokeeni pongezi Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika wamachinga Mheshimiwa Waziri alieleza katika hotuba yake, anasema kwamba Wizara inakamilisha utaratibu wa kuzipokea bilioni 22. Sasa mimi najiuliza, kwa nini hapakuwa na uwazi katika fedha hizi za wamachinga, hizi bilioni 22? Mheshimiwa Waziri anajiandaa kuzipokea, fedha ambazo zilivyokuja zilikuja kama mkopo wa *ECF*. Mheshimiwa Mwigulu alituambia katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2022/2023, alisema hivi, kwenye *paragraph* ya 81, kwamba Serikali inatarajia kupokea fedha trilioni 2.5 ambayo kwa miezi 40. Lakini kwa bahati katika *paragraph* ya 85 ya Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti kuu 2022/2023 alisema kwamba bilioni 45 zitakwenda kuratibu mambo ya machinga pamoja na kupatiwa mikopo wamachinga waliojipanga vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hotuba hii moja kwa moja ilipofika tarehe 18 Julai 2022, *IMF* wame-*release* hizo fedha kuja hapa Tanzania Julai 2022. Bunge lako kupitia Kamati zake likakaa, na lilivyokaa likapokea fedha hizi Kwenda kwenye sekta tofauti tofauti. Zimekwenda kwenye umeme, kilimo, mifugo, *TASAF* na nyingine hizi bilioni 22 ndizo zilikuwa zinakuja kwa wamachinga.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni kwamba hizo zote zimeonekana katika kitabu kikubwa hiki cha bajeti katika *approved estimate,* lakini hizi za wamachinga hazijaonekana. Sasa mimi najiuliza, kwa nini fedha hizi za wamachinga peke yake zisionekane? Fedha hizi bilioni 22 ukiziwekeza katika Benki ya Azania kwenye *fixed deposit* kwa miezi 11 unapata faida ya bilioni 2.3. Fedha hizi endapo mzingelikopeshwa kwa wakati kwa wamachinga, kwa sababu zinaitwa *revolving,* kwa hiyo zingelikuwa zinarudishwa anaanza kukopeshwa wengine.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha hizi za wamachinga zingekuwa zimetolewa hiyo athari tunayoisikia huko Kariakoo kwamba kuna wamachinga wanachajiwa *(be charged)* ushuru wa *store* lengo lake ilikuwa wale wanaopewa bidhaa mkononi

ili waweze na wao kwamba ziwe zimeshalipiwa kodi. Hii ni kwa sababu wanafanyabiashara wakubwa wanatumia ujanja kuwapa wale wadogo wadogo ambao wametandika vi-busati pale mbele na wanaokamata mkononi. Kwa hiyo athari hii nayo pia ingepungua.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza fedha hizi ziliingia mapema sio bajeti inayosubiriwa kukusanywa. Na malengo yake yalikuwa ndiyo hayo. Sasa najiuliza kwa nini kwamba sasa hivi ndio unafanyaika utaratibu. Mwezi wa 11 huu ndio unafanyika utaratibu wa kupokea hizo fedha. Utaratibu huo unafanyika sasa hivi, Serikali ilikuwa wapi muda wote huo? Maana ingelikuwa mimi ningeenda kuweka kwenye *fixed deposit* nikapata faida. Tunaambiwa sasa hivi, lakini fedha hizi zilikuja tokea mwezi wa saba, na kamati zako hizi ndizo zilizohusika kuzipokea fedha hizi za wamachinga.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa naiuliza Serikali, kwa nini fedha hizi hapakuwa na uwazi? Kwa nini kwenye *REA* zimekwenda bilioni 100? Kwa nini *TANESCO* zimekwenda bilioni 100? Kwa nini kwenye kilimo zimekwenda? Kwa nini kwenye mifugo zimekwenda? Hizi zilikosa nini? Na fedha hizi zilipokelewa milioni 151.7 Dola za Kimarekani, na zilikuja mwezi wa Saba na zilifanyiwa utaratibu zikaenda kwenye *vote* hizo. Sasa mimi najiuliza hapa Serikali kwa nini wametufanyia kitu cha aina hii?

Mheshimiwa Spika, wanasema kwamba *account* haijafunguliwa kwa ajili ya kuwakopesha wamachinga, si kweli. Bilioni 6.8 zilikuwa zinahusika na *other charges* ambazo ni kuratibu, lakini milioni 680 zilikuwa zinahusika na ujenzi wa ofisi za wamachinga kwa kila mkoa ambazo zimo mule; na hizi Mheshimiwa Rais amepita akizisema anapokutana na wananchi, kwamba atajenga ofisi za wamachinga kila mkoa. Sasa huku uratibu gani unaotakiwa? Bilioni 15.5 ndizo zilikuwa ziwe *revolving fund,* na tarehe 7 Oktoba. Serikali ilileta kwenye

Bunge lako hili kwamba tarahe 7 Oktoba, 2022 kwamba imeleta mchanganuo wa fedha hizi jinsi zitakavyotumika, na hiyo barua imekwenda Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha imekuja nayo Pamoja na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na makundi maalum. Sasa nashangaa fedha hizo zinatafutiwa utaratibu sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, hapa tunachezewa. Bunge hili tulipokea *ceiling*, Bunge hili tumepitisha bajeti. Ilitakiwa kuwe kuna *media report*. *Media report* ilisemaje? Kwa nini fedha hizi zisiingizwe? *Media review* kwa nini Bunge lako lisielezwe? Yaani tusijue, tunakuja kuja sasa hivi. Hata hiyo randama ambayo iko hapa sasa hivi ni kwa sababu ya mabadiliko, kwamba Serikali inataka kuji-*defend.* Sasa hizi fedha zimetumika lazima itakuwa ziko pahala ambako zimekaa.

Mheshimiwa Spika, mimi lengo langu, endapo Serikali haitakuwa na maelezo mazuri juu ya uwazi wa fedha hizi kama Bunge linavuyotaka na sheria ya bajeti inavyosema mimi naweza nikaja nikazuia shilingi ili Serikali itueleze tu; kwa sababu Hapana uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo nilizungumze, katika makundi maalumu kuna kundi la wazee pale Zanzibar. Wazee ambao hawakuwa katika mfumo rasmi wa ajira wanapata *pension*, inayoitwa *pension* kwa wote. Kwa nini kwenye uchumi mkubwa kama huu wa Tanzania hatuwezi kuratibu hicho kitu cha *pension* kwa wote? Tuweke *pension* kwa wote. Hawa wazee ndio walioshughulika kututafutia sisi uhuru, lakini wengine kazi yao walikuwa wakulima, wengine wafugaji, lakini walizalisha. Tukumbuke kwenye vita vya Uganda vita vya mpakani vile watu walitoa mali zao ambao walikuwa si waajiriwa hawa na hii nchi imekuwa salama. Sasa niiombe Serikali au niishauri Serikali, tutengeneze huu mfumo wa *pension* kwa wote tuwasitiri wazee wetu. Hawa wazee wametulea

tusiache wakaanza kupita wakaombaomba huko. Wakianza kuomba omba ni aibu na fedheha kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nitaunga mkono hii hoja Serikali itakapotupa uwazi pamoja na sheria, kwa sababu kifungu namba 65 cha sheria ya bajeti utakapofanya uzembe kama huu kuna vitu pale vimetajwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato ajiandae.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia pumzi kwa wakati huu nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Aidha nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mkosefu wa shukrani kama sitamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama mpambanaji ambaye anatupambania sisi Watanzania kwa jitihada zake za kuhakikisha huduma muhimu zinatufikia wananchi wa Tanzania popote tulipo. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wote kwa kusimamia vema majukumu yao na leo hii tukasikia Wizara hii imeanza kuonekana, hii yote ni jitihada yao wao kwa namna ambavyo wanaisimamia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Serikali kwa kupeleka miradi ya maendeleo 691, miradi ambayo ina lengo la kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana kupitia Wizara hii. Huduma hizo ambazo zimeelezwa katika ukurasa wa 11 wa randama ni vituo vya huduma ya afya, madarasa ya shule za msingi, pamoja na shule za sekondari. Mpango huu ni mwema sana na unaleta matumaini katika kupatikana kwa huduma ambazo zinakwenda moja kwa moja kuimarisha maisha ya wananchi, lakini pia kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wetu kupitia miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza naomba nishauri. Kwa upande wa vituo vya afya; kuhakikisha wataalamu wanakuwepo, lakini pia na vifaa tiba vinapelekwa kwa lengo la kufikia malengo ya kujengwa vituo hivi, lakini kwa upande wa shule, pia, kuhakikisha Walimu na vifaa vya kufundishia vinakuwepo, lakini pamoja na kuwepo vizingatie mahitaji ya wanafunzi wote wakiwemo wanafunzi wenye ulemavu kwa sababu, wanafunzi wenye ulemavu wanapata changamoto kubwa katika kujifunza kwa kutokupatikana kwa uhakika kwa vifaa ambavyo vinaweza kuwasaidia kufikia malengo yao ya kujifunza kama walivyo watoto wengine wasio na ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa kufuatilia na kubaini Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo yanafanya shughuli zao kinyume na utaratibu uliowekwa. Kufuatiliwa kwa mashirika haya kumeleta picha ya kuona kwamba, kuna baadhi ya mashirika ambayo yanasajiliwa kwa nia nzuri, lakini matokeo yake vitendo vyake vinaleta athari kubwa katika jamii yetu. Niiombe Wizara kupitia hili kufuatilia zaidi kwa karibu mienendo ya jumuiya hizi ambazo zinasajiliwa ambazo zipo na zile ambazo zinaundwa sasa hivi, kufuatilia kwa karibu ili ihakikishe mashirika yanayosajiliwa yawe na malengo mazuri ambayo yataleta tija kwa jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema haya natambua mchango mkubwa unaotolewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, yanasaidia sana Serikali, lakini kuna baadhi wanaunda mashirika haya kwa lengo la kupotosha utamaduni na silika zetu kama wengine walivyoanza kusema. Kwa hiyo, niwapongeze sana Serikali kwa hili, lakini waendelee kufuatilia kwa karibu zaidi na hayo ambayo wameyafuatilia wazidi kuyafuatilia na wawe karibu sana katika kusimamia utekelezaji wa mashirika haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee katika kipengele cha kulinda haki ya mtoto. Serikali imeeleza kwamba, imeunda madawati ya ulinzi na usalama yapatayo 1,393 kwa baadhi ya mikoa kwa shule za msingi na sekondari, lakini pia wameunda Mabaraza ya Watoto 560. Jambo hili ni jema sana kwa sababu, kuundwa kwa madawati haya na mabaraza haya yatakwenda kuwaweka watoto pamoja na kuweza kujadili changamoto zinazowakabili kwa pamoja na italeta picha ya kuwezesha kujua watoto wanakabiliwa na nini, kuliko hivi sasa hivi mpaka mtoto limfike, ndio uchunguzi unafanywa tunajua watoto wanapatwa na yapi, lakini katika mabaraza haya wataweza kutoa fikra zao na kila mmoja ataeleza changamoto.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua mabaraza na madawati haya vipi yamemwangalia na kumshirikisha mwanafunzi mwenye ulemavu? Kwa sababu, miongoni mwa wanaopata changamoto kubwa ni wanafunzi wenye ulemavu katika familia zao, lakini pia katika jamii inayowazunguka, wanakumbana na changamoto ya kubakwa, lakini pia na kudhalilishwa kutokana na hali zao.  Mheshimiwa Waziri atakapokuja atatueleza kwamba, watu wenye ulemavu au wanafunzi wenye ulemavu wameshirikishwa vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kuishauri Serikali, mabaraza haya na madawati haya yana lengo zuri, lakini hayataweza kusimama na kuendelea bila kuyawekea bajeti ya kutosha. Mheshimiwa Waziri labda atwambie wamejipanga vipi katika kuhakikisha madawati na mabaraza haya yanafanya kazi zake vizuri na yanaendelea ili kufikia yale malengo ya kuundwa kwake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee na mchango wangu katika Program Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. Imeelezwa kuwa elimu ya uelewa imetolewa juu ya program hii, lakini elimu hiyo imetolewa kwa mikoa kumi na ndio iliyofaidika, mikoa yenyewe imetajwa katika randama. Nataka kujua tuna mikoa isiyopungua 32 kama sikosei, je, vipi Wizara imeangalia hii elimu kufikia katika mikoa mingine ambayo imebakia? Kwa sababu, maendeleo yanapokuja yaende kote na Wizara imechagua kwa mikoa kumi, hii mikoa iliyokuja hali itakuwaje, lakini vigezo gani ambavyo vinasababisha hii mikoa kumi ikachaguliwa kuanzishiwa program hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee na mchango wangu kwa program ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Tumeelezwa kuwa kupitia randama hii Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake umeweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 663.4 kuanzia Julai mpaka Aprili, 2023. Fedha hizi zilitolewa kwa vikundi 11, lakini pia kwa wajasiriamali mmoja mmoja wapatao 14 na ikajumuisha wanufaika 104 kwa mikoa minne. Hapa pia nataka kufahamu je, kwa nini hiyo mikoa minne tu? Ni kigezo gani kilichotumika hata mikopo hii ikatolewa kwa hiyo mikoa minne? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja Mheshimiwa, kengele ya pili ilishagonga.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwisho, naomba nimalizie mchango wangu katika makusanyo na mapato ya Wizara hii. Kwa mwaka 2022/2023, Wizara ilikadiriwa kukusanya bilioni 8.5, lakini hadi kufikia Aprili, 23 imekusanya 3,025,562,821. Nataka kujua ni changamoto gani iliyosababisha Wizara kushindwa kufikia malengo hayo iliyojiwekea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato na Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele ajiandae.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara muhimu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona umuhimu wa kipekee na kuamua kuiweka Wizara hii ijitegemee ili iweze kuwafikia Watanzania kwa ukaribu. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa namna wanavyofanya kazi kwa mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kuchangia kwenye maeneo kadhaa. Eneo la kwanza ni mafunzo ya mikopo ya asilimia kumi kwa wajasiriamali. Mafunzo haya muda unaotolewa ni mdogo, hautoshi. Namaanisha kwamba, Wizara hii kama ingeamua kujipanga vizuri ingeweza kutoa mafunzo haya ya kuanzia siku tatu mpaka tano na wakati huo wakiwa wanahakikisha bajeti ya mafunzo haya inakuwa imeshatengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili wakati wa utolewaji mafunzo haya naomba pia wataalam wetu washirikiane na wataalam wa benki. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wanaweza kufanya mambo yafuatayo:-

Kuandika andiko rahisi la kibiashara kulingana na mazingira yetu halisi; Kutoa mafunzo ya utunzaji kumbukumbu wa fedha; Kutoa mafunzo ya urejeshaji wa mikopo; na Kutoa mafunzo ya faida na mafunzo ya wajasiriamali kwa uhalisia kuendana na shughuli wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mama lishe anatakiwa apate elimu ya umamalishe, ushonaji pia pamoja na makundi mengine kuliko ilivyo hivi sasa elimu inayotolewa inatolewa kwa ujumla wake. Elimu inatolewa kwa siku moja, muda huo hautoshelezi. Nilikuwa napendekeza kwamba, elimu hii itolewe kwa muda wa siku tatu mpaka tano, ili wajasiriamali hawa waweze kupata elimu ya kutosha na yenye uelewa, ili waweze kufanyia kazi mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napendekeza pia, mikopo hii ingeweza kutolewa hata kwa mjasiriamali mmojammoja ambaye anaweza kuwa na dhamana isiyohamishika na ni mfanyabiashara ambayo inaendelea, ili aweze kuajiri na Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio hilo tu, napendekeza pia katika vikundi vinavyopewa mikopo waanzie watu wawili, watatu hadi watano, kuliko ilivyo hivi sasa mikopo inatolewa kuanzia watu watano na kuendelea. Watu hao mara nyingi wanakuwa hawaendani. Nasema hivi namaanisha kwamba, mikopo inapotolewa kwa watu watano ilimradi tu wanakuwa wamekidhi vigezo vya masharti yale, lakini wanapopewa mikopo ile wengi wao wanakuwa wanapotea, kati ya watu

wawili au watatu kwa sababu, hawaendani na inakuwa vigumu baadaye kwenye marejesho, wanabakia wanaofanya biashara ile watu wawili au watatu. Kwenye urejeshaji wengine wamepotea, nani atarejesha mikopo ya wale wengine ambao hawapo? Kwa hiyo, tunaona mikopo mingi inakuwa chechefu kwa sababu hii, hawaendani kiuhalisia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba niende kwenye upande wa waajiriwa hawa, wataalam wetu, Maafisa Maendeleo ya Jamii. Wataalam wetu wengi wanapoajiriwa wanakuwa hawapati mafunzo, wanakwenda moja kwa moja kazini kitu ambacho kinakuwa hawaendani na majukumu yao ambayo wanatakiwa waende wakayafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona Maafisa Maendeleo ya Jamii wengi wanapoajiriwa wanapenda kukaa ofisini. Hawa kazi zao sio za ofisini, inatakiwa waende vijijini na ndio maana tunaomba hata Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa wapatikane kwenye kila kata. Utaona kule kwenye kata kazi ya maendeleo ya jamii anafanya Afisa Mtendaji wa Kata, sio sawa. Kwa kufanya hivi maana yake tunakuwa tunapunguza ufanisi wa kazi za maendeleo ya jamii kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba pia, wakati tunapoenda kutoa mikopo hii iendane sambamba na urejeshwaji wa marejesho ya mikopo hiyo. Kwa nini? Sheria yetu haiweki wazi namna ya urejeshaji wa mikopo hii. Naomba sheria yetu iseme, iwe na meno ili mikopo hii ipatikane na iweze kurejeshwa kwa wakati, izunguke waweze kupata na wajasiriamali wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Thecla Mohamed Ungele. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ajiandae.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa afya njema tena kusimama na kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mara nyingine tena kwa kuona umuhimu wa kuwa na Wizara hii muhimu ambayo itashughulika na masuala ya maendeleo ya jamii yetu. Napenda kuwapongeza sana Mawaziri, Dkt. Gwajima pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote pamoja na wafanyakazi wote wanaofanya katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, leo naomba kuchangia katika jambo moja linalohusu wajane. Katika takwimu hapa duniani kuonesha kwamba, kuna wajane takribani milioni 259 na nusu ya wajane haw ani maskini na huishi katika mazingira ya unyanyapaa, ubaguzi sababu ya jinsia zao pamoja na umri.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zinazoendelea, hususan Tanzania, wajane wengi wanapopoteza wenza wao huchanganyikiwa kwa sababu, wajane wengi wanapoishi na wenza wao hushirikiana katika mambo mbalimbali ya kimahusiano, ya kiuchumi na kadhalika. Kwa hiyo, kifo kinapotokea, hasa kwa mwanaume, wajane hulia mara mbili, hulia kwa kupoteza wenza wao, lakini hulia muda mrefu kwa kufikiria maisha baada ya kupoteza wenza wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wajane wengi katika Nchi ya Tanzania wanapofiwa na waume zao, tafiti zinaonesha kwamba,

hupoteza hadhi zao kwa sababu, katika jamii yetu, wanawake huonekana kama ni wenza wasaidizi. Kwa hiyo, pale anapoondoka mwanaume, basi wao hujiona au huoenakana kwamba, hadhi kidogo imepungua, hata utu pia huonekana umepungua, lakini zaidi ya yote kipato hupungua baada ya kufiwa kwa sababu katika jamii zetu wanaume wengi ndio ambao huleta kipato katika familia. Vile vile wajane hupelekwa mbali, huenguliwa kwenye mambo ya urithi wa mali za familia na katika baadhi ya jamii zetu wanawake hurithiwa kutokana na ile mila iliyoko katika jamii hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, wajane ni kundi muhimu sana ambalo Serikali na jamii kwa ujumla ni vyema tukawaangalia kwa jicho la tofauti kwa sababu, wajane hawa mwisho wa siku huishia kuchanganyikiwa. Ikumbukwe kwamba, wajane ndio wanaotunza familia, wanawake hawa ambao sasa ni wajane na wanaachwa na watoto ambao ni yatima. Yatima ni mtoto ambaye amepoteza aidha, mzazi mmoja au wazazi wote, kwa hiyo, ninapoongelea wajane nawaingiza na watoto yatima ambao hulelewa na hawa wajane na mwisho wa siku hawa wajane hushindwa kulea watoto na hushindwa kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wajane mara nyingi wanapopoteza wenza wao wanakwenda Mahakamani kwenda kudai baadhi ya haki, ikiwepo mali. Hivyo, wajane hupoteza muda mwingi sana Mahakamani, wajane hupoteza muda mwingi sana katika mabaraza ya kifamilia, mabaraza yale ya usuluhishi na kadhalika na hivyo huathirika kisaikolojia na kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao katika jamii.

Mheshimiwa Spika, naongea kwa hisia kali kwa sababu, wajane ni wengi na ni kundi ambalo kwa kweli, wanahitaji sasa ifike mahali Wizara iwaangalie na waweze kuwa na nguvu kama wagane. Walie jambo moja kwamba, wamepoteza

wenza tu na sio kupoteza vitu vingine na walee watoto kama wagane wanavyolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii kuhusu hawa wajane, kwanza katika jamii yetu elimu ya kutosha itolewe kwa jamii kabla hata watu hawajawa ama wagane au wajane, kwamba kuwa mjane ni ile hali tu ya kupoteza mwenza na siyo kupoteza vitu vingine. Kwa sababu sasa hivi kuna vurugu nyingi ambapo wanawake wanajiandaa wanakuwa wakali na hivyo changamoto ni kubwa sana katika jamii zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, mimi naishauri tena Wizara hebu iunde kitengo maalum ambacho kitawaangalia wajane na kuwapa elimu ya kutosha ili waweze kuelewa haki zao na nini wafanye pale ambapo mtu atakuwa mjane kwa sababu kifo hakizuiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ninaomba Wizara iangalie kupata msaada wa kisheria jinsi ambavyo hao wajane wanapopata changamoto wanaweza kupata msaada wa kisheria wapi, sehemu gani waende ili waweze kupata msaada wa kisheria, pia waweze kupata msaada ili wasibaguliwe katika familia zao, vilevile wasipate ukatili wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Wizara sasa ifike mahali ambapo isomeshe wataalamu katika ngazi ya vijiji ambao watapata ujuzi wa kuwasaidia wajane kuzielewa haki zao, kuwafariji ili wasipate zile changamoto waweze kuendelea kulea familia zao, waweze kuchangia katika maendeleo ya jamii yetu na vilevile tusizalishe watoto ambao watakuwa wamechanganyikiwa au ambao watashindwa kusoma vizuri na mwisho wa siku hao watoto hubakia kuwa watoto wa mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, nami pia naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii nami nichangie. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Naibu wake, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii na wote kutoka kule ngazi ya Mikoa na Halmashauri kwa kazi kubwa wanayoifanya usiku na mchana. Hakika wanafanya kazi nzuri, inabidi kuwapongeza.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee nazipeleka pia kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ya kujali jamii ya Tanzania na makundi maalum hasa wamachinga, ambao tunaona kabisa hata kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kabisa kwamba Mheshimiwa Rais ametoa hizo shilingi bilioni 22.9 hivyo, ombi langu ni fedha hizi zitolewe kwa wakati sasa hivi ili zifanye kazi inayopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najikita kwenye eneo la ustawi wa jamii. Kazi ya ustawi wa jamii ni kubwa kwenye Wizara hii na tumeona kuanzia ngazi ya Taifa hadi kule kwenye Halmashauri. Kazi yake kubwa ni kuimarisha jamii zetu. Tumeona hata taarifa ya Kitaifa, imesema wimbi kubwa la watoto wa mitaani limepungua kwa asilimia 38. Pia hata migogoro ya ndoa imepungua kwa asilimia 27 hii ni jitihada kubwa kweli kwa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata pia kwa Mkoa wa Lindi tunaona pamoja na maafisa ustawi wa jamii wachache, wako 19 tu lakini bado kumefanyika kazi kubwa na wamebaini ukatili wa kijinsia umepungua kwa kiasi kikubwa sana. Mashauri kama 1,105 yamefanyika kufuatilia changamoto ya ukatili wa kijinsia. Pia wamesimamia msamaha wa matibabu kwa walengwa zaidi ya 33,000 kwa Mkoa wa Lindi na mengine yote hayo ni mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona mmomonyoko mkubwa kweli wa maadili na maadili haya yanaanzia ndani ya familia, familia ni kila kitu, naamini kabisa wote tulioko hapa tumetoka kwenye familia na tunazihudumia familia. Kwa hiyo, kila kitu katika maisha kinaanzia kwenye familia; maendeleo yoyote, familia, sasa tunaona familia zetu zimeendelea kuathirika na mmomonyoko wa maadili, hili jambo ni hatari sana. Tumeendelea kuhangaika na elimu, tumeendelea kuhangaika na afya, tumeendelea kuhangaika na *REA* hii ya umeme vijijini, vyote hivyo ni kwa ajili ya maendeleo lakini bado kama hatutazingatia maadili ndani ya familia zetu itakuwa ni bure kabisa, itakuwa ni shida kabisa, mwisho wa siku tutakuja kupata kizazi ambacho wala hata hiyo elimu yenyewe haitaonekana, wala hata afya yenyewe haitaonekana. Mimi naomba haya mambo yote yaendane sambamba, tuendelee kuyaboresha maadili ndani ya familia na miradi mingine tuendelee kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoona taarifa ya utafiti wa Serikali na *UNICEF,* walibainisha kwamba asilimia 60 ya watoto walioathirika katika ukatili wa kijinsia imetokea majumbani, pia asilimia 40 imetokea shuleni, kwa hiyo bado naendelea kusisitiza katika mchango wangu huu, nakumbuka hata mwaka jana nilichangia, bado mtoto huyu hayuko salama, kila eneo analokwenda. Hata mchangiaji mwingine alisema, hata kwenye vyombo vya habari, hata kwenye makanisa, hata

kwenye misikiti, bado huko kuna unyanyasaji wa kijinsia, mtoto huyu hayuko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunaona Wizara imekuja na mpango mkubwa huu wa malezi na makuzi ya mtoto huyu. Mimi naomba kwa kuwa vitendo hivi vya mmomonyoko wa maadili vimekithiri na mtoto huyu hana usalama wowote kila aendapo, ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba na Wabunge wenzangu tusaidiane, tuungane mkono katika hili kwa sababu vita hivi ni vyetu sote. Kuwepo kabisa na mkakati wa Kitaifa vituo hivi vijengwe kimkakati kabisa, viwe vituo vya kielelezo kwa nchi nzima. Vituo hivi ndivyo vile tulivyosikia hata Mheshimiwa Waziri alivyosema, kwamba vituo hivi ndiyo vitamlinda mtoto kiakili, kimwili, kiafya ili angalau kumlinda asogezesogeze umri ambao ataweza kujitetea mwenyewe. Kwa sababu tayari akiwa mdogo hana utetezi wowote, akiwa wapi hana utetezi wowote, wazazi wake wanakwenda kazini wanamwacha mtoto hana utetezi wowote. Tunaomba tafadhali jambo hili lizingatiwe ili angalau mtoto huyu afikie umri ambao ataweza kujitetea mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba wote tuungane katika vita hii ya kupingana na jambo hili ili angalau kwenye jamii yetu lipungue kwa namna fulani ili tuwe na Taifa lililo na maadili mazuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi na mimi kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri kama wenzangu walivyosema, pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuchangamsha Idara na Wizara ya wanawake kuonekana sasa tupo na tunaweza tukapiga kelele kwa sauti kubwa.

Mheshimiwa Spika, bado tuna changamoto nyingi sana, leo nitazungumza chache nikianza na suala la mauaji kwa kutumia mapenzi. Tumeona kwa siku za hivi karibuni kumekuwa kuna mauaji makubwa sana kisa wivu wa mapeni. Mheshimiwa Waziri, kuna haja kubwa sana sasa ya kupiga kelele. Na suala hili haliko Tanzania peke yake, watafiti wa haki za binadamu wamefanya utafiti, mwaka 2021 na 2022 kwa dunia nzima takribani wanawake 45,000 wamekufa kwa wivu wa mapenzi, kwa Afrika Mashariki peke yake, asilimia 43 wanawake wanapigwa, wasichana wanapigwa na vijana kisa wivu wa mapenzi, na wakati mwingine hawana uhakika, ni wivu tu umewatokea anaamua kutoa roho ya mtu kwa sababu ya kumuonea wivu. Mheshimiwa Waziri, kuna haja ya kupiga kelele katika eneo hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa vyuo, wanandoa, wanapigana wanauana na kuacha watoto mitaani wakizunguka kisa tu baba aliona simu au mama aliangalia simu ya mumewe na kuingia kwenye matatzizo. Labda niseme tu hili pia kwamba tuna haja sasa ya kujijenga tabia njema katika familia kwa sababu mwisho wa siku wivu umeondoa roho za wanawake wengi katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ukatili wa kisaikolojia. Kuna Mbunge mwingine amezungumza hapa, leo

hii takribani ndoa zaidi ya 700 zimeripotiwa katika kuwaumiza wanawake kwa kuwaacha. Mwanaume anamwacha mwanamke na watoto watano, watoto 10 anakwenda kuoa nyumba ndogo na kumwacha mke wake na kusababisha yule mwanamke kupata msongo wa mawazo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kuna namna nafikiri watu wanaohusika na afya za akili na ustawi wa wanawake wanasimamia suala hili. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri, leo hii tunataka kujenga Taifa la kesho, unalijengaje Taifa ambalo mtoto anaona mama yake anapigwa mbele yake? Mtoto anaona baba mtu anaingia usiku na matusi kwa sababu tu kalewa anatamka maneno yasiyofaa katika familia. Kuna haja ya kujenga Taifa bora, kuna haja ya kusema na kukaripia pale mambo mabaya kama haya yanapotokea, kuna haja ya kujenga Taifa jipya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunazungumzia mmomonyoko wa maadili. Mheshimiwa Waziri tukiwepo sisi viongozi, unatoka nyumbani asubihi unakwenda kazini, unarudi jioni kwa sababu ya foleni, hujui mtoto ameshinda na nani siku nzima, akiwa shuleni walimu wana msongamano wa wanafunzi wengi, mwalimu hawezi kuangalia tabia ya mtoto mmoja mmoja darasa lina watoto zaidi ya 50 au 60. Kwa hiyo, tunataka turudi nyuma sisi kama familia tuhakikishe tunafuatilia haki za watoto na makuzi yao ili tupate kuwa na Taifa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, leo hii msichana wa kazi ndiyo anakuwa mlinzi wa mtoto nyumbani, Mama umerudi umechoka, baba amerudi na *frustrations* zake naye amechoka, huyu mtoto anajilea mwenyewe, anajifunza mwenyewe, wanaanglia *pornographic pictures* kwa sababu hakuna uangalizi nyumbani. Kisasa ambacho tumekuwa nacho, kizungu, tunaiga mambo ya magharibi, unamnunulia mtoto ma-*toys* ya kuangalia na wanajifunza mambo yasiyofaa.

Wakati mwingine tunaona sifa tunawanunulia watoto simu, unampa simu anakuwa na uhuru nayo, anakwenda ana-*google* anaanglia picha zisizofaa na wewe mzazi unafikiri ndiyo uzungu, unafikiri labda ndiyo maendeleo, mwisho wa siku tunaharibu watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kujenga Taifa bora ambalo litafundisha watoto wetu umakini, kama inabidi, turudi zamani zile ambazo mtoto ni wa kijiji, mtoto ni wa mtaa, mtoto ni wa Taifa, anapokosea mtoto achapwe na jirani, aonywe na jirani, wala mzazi asiende kumgombeza mwalimu kwa nini umenichapia mwanangu ukome, huyu mtoto siyo wa kwako. Mtoto kwa sasa tunahitaji awe mtoto wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, rushwa ya ngono vyuoni. Tumeona mabinti wengi wakilalamikia suala la rushwa ya ngono vyuoni, wasichana wanaona bora basi kama ni hivyo hata kusoma wanashindwa wanajua mwalimu fulani ananihitaji basi nitatembea naye, naye atanipa *GPA* ya kutosha. Tunaomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe unahusika na Wizara hii, simamia nidhamu ya walimu wa vyuo.

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge hapa anayewakilisha vyuo vikuu amesema, mwalimu ni mdhamini mkuu wa mwanafunzi, lakini kama anataka ngono ili ampatie maksi anakuwa hatendei haki kazi yake na taaluma aliyosomea. Leo hii rushwa ya ngono imekuwa kilio kikubwa sana kwa wasichana na wanawake vyuoni, ninaomba wewe kama Waziri uweze kulisimamia hilo nasi tutakusaidia kupiga kelele katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ukatili wa watoto wengi wameshausema. Mtoto mdogo ukatili unaanzia nyumbani. Leo hii nyumbani watoto wanaharibika tunazungumza suala la ushoga na mambo kama hayo, lakini asilimia kubwa inaanzia

nyumbani. Leo hii tunaogopa kukaribisha mashemeji nyumbani, kaka zetu tunaogopa kuwakaribisha nyumbani kwa sababu utasema lala na *uncle* kule ndiyo uharibifu unakotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna namna kama Wizara inabidi tuzungumze, leo hii unajua unao majirani, majirani zako ni watu sahihi, lakini huyohuyo jirani yako unashangaa anatongoza binti yako na wewe uko palepale. Tunahitaji kupiga kelele kama Taifa. Ukatili wa kijinsia umekua mkubwa sana kwa sababu hata takwimu za 2022 ambazo zimezungumzwa na haki za binadamu, zaidi ya matukio 350 yamewakuta watoto wadogo. Leo tuna madawati lakini vijijini mpaka kufikia kwenye dawati la kijinsia ushahidi unakuwa umekwisha kupotea. Kuna haja ya kujitahidi sana kama Taifa kuweka ulinzi kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ninachoweza kushauri ni kwamba *TASAF* ipo kwa ajili ya kusaidia ustawi wa maisha ya watu. Mimi ninaomba *TASAF* ije katika Wizara yako, itoke kule iliko kwa sababu huku kwenye Wizara yako ndiyo sahihi ambako kuna uhitaji kusaidia watu katika ustawi wa maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekwisha kusema hayo, lakini bado niendelee kusisitiza masuala ya makuzi ya watoto, kama Taifa lazima tuyapigie kelele. Leo hii mtoto analindwa na wewe mama, analindwa na wewe baba, ukisubiri Serikali ikusaidie, Serikali itakuja baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nitoe rai kwa Watanzania wote, tunahitaji kuwalinda watoto kwenye maadili ya kidini, kila mtu ana dini yake amfundishe mtoto toka mdogo, kwa sababu tunaamini mtoto akiwa mdogo kichwa chake kinakua kinapokea vitu vipya. Kwa hiyo sisi tuseme nao,

tunapokuwa tumechoka ni kweli tukirudi tukazungumze na watoto na tuwaonye watoto, tusiogope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini katika sheria ya viboko japokuwa ipo, tuifwate hiyo sheria lakini itaweza kusaidia kubadilisha. Wengine tumefika hapa kwa sababu tulichapwa, tulionywa, tulikatazwa vitu vibaya, ndiyo maana leo tumefika mahali hapa. Tusianze kuiga mambo mengine kama Taifa tukaacha watoto wetu wanapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono hoja kabisa katika Wizara hii kwa sababu mimi ni Mwanakamati na ninaona mambo mengi magumu ambayo Wizara hii inapitia na hasa tukizungumzia watoto ambao wako jela, tukizungumzia wazee ambao wamekosa makazi na Serikali hii inaamua kuwasimamia. Mimi naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu kwa mustakabali wa makundi maalum ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Dorothy Gwajima, Naibu wake, Mheshimiwa Mwanaidi Katibu Mkuu, Dkt. Jingu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa mstari wa mbele kuyajali makudi maalum, lakini pia kwa namna ambavyo ameendelea

kuwatumikia Watanzania kwa moyo wa upendo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri ambayo unaifanya na namna ambavyo unaliendesha Bunge letu, nakupongeza sana. Paada ya pongezi hizo, nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu. Kila kukicha tunasikia vitendo vya ukatli vikishamiri katika jamii. Unasikia mtoto amebakwa huku, unasikia mtoto kalawitiwa kule, unasikia mwanafunzi ametoroshwa, unasikia mwanamke amepigwa, vitendo hivi vimezidi kushamiri katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe sana jamii yangu iweze kubadilisha mtazamo wa masuala haya, pia niiombe Serikali iweze kuangalia kwa kina na kuja na mkakati mahsusi wa mafunzo maalum kwa ajili ya jamii katika ngazi zote kuanzia Kata, Vijiji hadi Vitongoji. Wahakikishe kabisa mafunzo haya yanafika,kwa sababu vitendo hivi vya ukatili wa kijinsia vinatokea katika ngazi ya familia. Utasikia mjomba leo amembaka mtoto wa dada yake, baba mdogo kambaka mtoto wa shemeji yake. Kwa hiyo ni muhimu sana mafunzo yakafanyika katika ngazi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali, pamoja na mikakati mbalimbali ambayo wanaifanya kwa kila siku ya kuelimisha jamii, lakini bado nguvu kubwa inatakiwa kuwaelimisha jamii ili sasa waweze kuepukana na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba sana sasa kuwepo na haya madawati ya ukatili wa kijinsia katika kila sehemu, kuanzia ngazi ya kata na ngazi ya Kijiji ili yaweze kutoa miongozo mbalimbali na kuwasaidia wananchi kuweza kuepukana na vitendo hivi vya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika Mkoa wangu wa Singida kuna changamoto kubwa ya uhaba wa watumishi wa kada ya Maafisa Maendeleo ya Jamii. Hawa ndio wanaobadilisha mitazamo katika jamii, na ndio wanaoisaidia jamii kubadilisha uelekeo wa maisha yao. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii wa kutosha ili sasa kazi nzuri za Maafisa Maendeleo ya Jamii ziweze kufanyika katika kila eneo na katika kila sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mikopo. Naipongeza sana Serikali ambayo imeendelea kutoa mikopo kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu. Natambua kwamba kwa sasa wamesitisha, kwa hiyo, naomba wafanye maboresho haraka ili mikopo hii iweze kutoka kwa makundi haya ya vijana, wanawake na wenye ulemavu, kwa sababu imekuwa ni mkombozi mkubwa sana kwa wao kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa haya machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka ajiandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kipekee kabisa, nampongeza Mkurugenzi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum. Kwa kweli Mkurugenzi huyu amekuwa ni mtu anayetoa ushirikiano sana pale unapokuwa unafuatilia masuala ya wanawake, watoto na watu wenye mahitaji maalum. Ni mtu anapokea simu, anajibu

meseji na bado anafuatilia kama umefanikiwa suala lako. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye mwanzilishi wa majukwaa ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Leo hii nitazungumzia kuhusu majukwaa ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais mwaka 2016, alianzisha majukwaa haya ambapo mwaka 2022 yaliratibiwa rasmi. Lengo kubwa la majukwaa haya lilikuwa ni kuwakutanisha wanawake pamoja, kujadili masuala ya kiuchumi, masuala ya masoko, fursa mbalimbali zinazowazunguka kwenye makazi yao, na kubwa zaidi, kujadili changamoto zao mbalimbali katika shughuli zao za kiuchumi za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ambaye nie mwasisi wa majukwaa haya, aliziona changamoto za akina mama wajasiriamali wa Taifa hili, ambazo ni mitaji midogo isiyotosheleza, nyenzo duni, ujuzi mdogo, fursa za masoko, mila kandamizi na kukosa dhamana za kuweza kupata mikopo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imekuwa ikifanya vizuri na tumemsikia Mheshimiwa Waziri hapa, ameeleza vizuri kuhusu majukwaa, lakini tuiombe Wizara, elimu kwenye majukwaa haya kama ambavyo Mwongozo wa Uanzishwaji wa Majukwaa haya unavyosema, isishuke tu kwenye ngazi ya viongozi wa mkoa wa jukwaa, iende mpaka ngazi ya Halmashauri, ngazi ya Kata, ngazi ya Vijiji na Mitaa. Kule ndiko kwenye wanawake wajasiriamali wengi, na wanawake wengi bado hawana uelewa wa mwongozo huu. Kwa hiyo, naiomba Wizara ifanye taratibu, mwongozo huu uwafikie wanawake wote mpaka wa kule chini.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kushiriki majukwaa machache ya wanawake kule chini, wengi wao wamehamasika sana. Kwa mfano, Mkoa wa Dar es Salaam, vikundi vilivyo chini ya majukwaa ni vikundi 18,240, ni vikundi vingi sana na ni mwamko kwa wanawake wa Dar es Salaam kuhusu majukwaa haya. Wanawake wengi bado hawajajua lengo mahsusi la haya majukwaa. Wengi wao wamejiunga humo wakiwa tayari wanasubiri fursa za mikopo, lakini lengo mahsusi ni kutoa elimu kwa wanawake wa majukwaa haya. Hivyo naiomba Wizara, ihakikishe kweli majukwaa haya yakafanye vizuri kama ambavyo mwasisi wetu ametamani kuona anainua uchumi wa wanawake wa Tanzania kupitia majukwaa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona majukwaa haya yako katika ngazi ya Mkoa, ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji. Naiomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhakikisha majukwaa haya yanakuwa yenye tija na yanamsaidia kweli mwanamke wa kitanzania kwa kuratibu utoaji wa mafunzo, upatikanaji wa mitaji, kuwaunganisha na fursa mbalimbali, na kubwa zaidi kuendelea kutafuta wadau watakaowasaidia mitaji, maana kiu kubwa ya wanawake kwenye masuala ya ujasiriamali ni mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba zaidi Wizara, ihakikishe kwenye Mwongozo huu wa Uandaaji wa Majukwaa, na kuwasaidia akina mama hawa wajasiriamali, ihakikishe inakwenda kugusa vitu vitatu ambavyo ni muhimu sana kwa mwanamke wa kitanzania ambaye ni mjasiriamali. Vitu hivi ni elimu, mitaji na fursa. Mjasiriamali yeyote ukimgusa kwenye hivi vitu vitatu, unakuwa umemkomboa. Kumpa mtaji peke yake bila elimu wala kuzitambua fursa, bado haisaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara, inapoenda kutoa elimu kwa hawa waratibu, ihakikishe inafika ngazi ya kata

na huko kwenye kata ihakikishe Madiwani wa Viti Maalum wanahusishwa. Kwa sababu kwenye majimbo yetu tuna Madiwani wa Viti Maalum. Madiwani hawa wanasaidia vikundi vingi sana vya akina mama kutoa elimu mbalimbali na pia kuwasimamia kwenye mikopo. Kwa hiyo, hata wao wanatakiwa wajue lengo la majukwaa haya ili yakafanye vizuri. Hatutamani tena kuona majukwaa haya yameanza halafu yanakufa, hayaleti tija kwa mwanamke wa kitanzania.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara ijitahidi pia kutoa uelewa hata kwa Waheshimiwa Wabunge wanawake, kuwahamasisha katika kujua huu Mwongozo wa Majukwaa, kwa sababu pia na Waheshimiwa ni akina mama ambao wanasimamia akina mama huko chini. Mwongozo unaeleza vizuri kabisa, Wizara imeshautoa, ugawanywe kwa Waheshimiwa Wabunge, wahakikishe hata kwenye majimbo yao na mikoa huko iwafikie akina mama wapate uelewa wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, pia nawaomba Mabibi Maendeleo wote na waratibu wote wa majukwaa wawasimamie akina mama ipasavyo kwenye vikao vyao, wanapokuwa wanajadili mambo mbalimbali na mafunzo, wahakikishe wanawaunganisha na wadau mbalimbali washiriki kwenye vikao vyao. Kuna wadau kama *SIDO, TBS*, Taasisi za kifedha *BRELA,* Maafisa Biashara wa Halmashauri na wataalam wa masoko. Wasijadili fursa hizo peke yao, waletewe na wataalam wa hayo masuala.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwa kufanya hivi hata mikopo ya Halmashauri ambayo sasa hivi Serikali imeenda kujipanga vizuri ili kuhamasisha hii mikopo iweze kutoka kwa tija, lakini itakaporudi tunataka kuona watakaonufaika wa kwenye majukwaa nao wawe wamojawapo. Kwa sababu kwa muundo huo wa majukwaa na kwa tija ya majukwaa, kama kweli akina

mama wataenda kunufaika na majukwaa haya kwa kupata hii elimu, nina uhakika kabisa mikopo ya Halmashauri itakayoanza kutoka itakwenda kuwa na tija na itawasidia sana wanawake, wajasiriamali wa Taifa hili. Pia itasaidia kuwaondoa kwenye masuala manne ambayo yanawaumiza akina mama.

Mheshimiwa Spika, tumeona mikopo ya Halmashauri ilikuwa hairudi, lakini kama majukwaa haya tangu mwaka 2022 yaliporatibiwa yangekwenda kufanya kazi nzuri na kuwaelimisha akina mama hawa, wanufaika wa mikopo wangeweza kurudisha ile mikopo. Haiwezekani unamkopesha mtu, bado hujampa elimu. Mtu anapata fedha kwanza, ndiyo anaanza kuwaza kitu cha kufanya. Kwa lengo la majukwaa haya, tutaiona Halmashauri inakwenda kufanya vizuri kwenye mikopo, sababu wanufaika watakuwa wameshapata fursa za kufahamu ujasiriamali na mambo mbalimbali kupitia majukwaa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia majukwaa haya yakifanya vizuri, yatakwenda kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja. Kwa sababu mama anayeenda kujifunza kwenye majukwaa anayeenda kupata pale ujuzi, utamsaidia hata katika shughuli zake mwenyewe kama mtu mmoja mmoja. Pia tutashuhudia viwanda vidogo vidogo vya akina mama wajasiriamali kwenye Taifa hili kama tutashirikisha wadau mbalimbali katika kuwainua akina mama. Vilevile tutawakomboa akina mama na mikopo umiza. Tumeona mikopo ya Halmashauri ilikuwa haitoshi, wahitaji ni wengi, vikundi ni vingi. Kwa hiyo, mtu anatamani kufanya biashara, anakwenda kukopa, lakini hajui ile riba itamuumiza kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana Wizara izingatie kwenye hayo mambo manne ambayo yatakwenda kuwasaidia akina mama kupitia majukwaa haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho niombe Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya ajiandae.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara kwa ujumla. Tunawapongeza sana, wanafanya kazi kubwa kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya, kuifungua nchi kiuchumi. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwaamini vijana na kuweza kuwapatia ajira zaidi ya 21,000 kwa kada japo ni tofauti, ikiwepo Ualimu na Udaktari. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais na niseme, sisi vijana tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nielekeze mchango wangu kuhusu watoto waliofanya makosa, waliopo gerezani. Kiukweli watoto ambao wanahukumiwa na kupatiwa adhabu walioko

gerezani wengi wao wanafanya wakiwa na umri mdogo. Wanafanya makosa wakiwa na umri wa kuanzia miaka nane hadi 18. Wengi wao wanakuwa chini ya umri wa miaka kumi na nane.

Mheshimiwa Spika, adhabu zinazotoka kwa watoto hawa ni kali. Adhabu zao zinaanza kwa kufungwa jela kwa miaka thelathini, wengine wanahukumiwa kwa kifungo cha maisha, wengine wanahukumiwa kunyongwa. Tukumbuke mtoto huyu anafanya kosa akiwa na umri wa utoto. Mara nyingi wanafanya makosa ya mauaji, lakini kifungo wanachokitumikia ni cha muda mrefu. Je, Serikali inahakikisha vipi wanapata stahiki zao watoto hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, watoto hawa ambao wako kwenye magereza wanakosa zile haki za Watoto. Kwanza kusoma, hawasomi vizuri; kulala, mazingira yao kama watoto bado wanastahiki kulala sehemu nzuri, lakini wanakosa huduma hii ya kulala sehemu nzuri. Japo Serikali imeonesha ina nia na dhamira ya kuendelea kujenga magereza ya watoto, lakini toka bajeti iliyopita Wizara imeendelea kusema itajenga magereza ya watoto, lakini bado hawajaweka miundombinu na miundo rafiki kwa watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbuke adhabu hii kwa watoto wetu ni ngumu sana. Naiomba sana Wizara hii kupitia Bunge lako tukufu, ije na muswada wa kurekebisha sheria hizi ili kuwe na adhabu ya watoto. Kwa mfano, mtoto ameua akiwa na umri wa miaka nane, jifikirieni ninyi Waheshimiwa Wabunge nyote hapa, mkiwa na umri wa miaka nane, mlikuwa mnakumbuka nini? Sidhani kama kuna Mbunge alikuwa anajielewa akiwa ameshafanya makosa haya akiwa na umri wa miaka nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, adhabu hizi ni kali, tuangalie, kwa mfano kuna msanii mmoja anaitwa Lulu, alimuua Kanumba, lakini amepatiwa adhabu ambazo ni za kiutoto na ametoka, lakini kuna watoto wengine mpaka leo wako magerezani. Wamefanya kosa lile lile la kuua. Tuangalie, kama leo Kanumba angekuwa hai, leo hii angekuwa naye anahukumiwa kwa kosa la kubaka miaka 30 jela.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara hii iendelee kuangalia watoto ambao wako magereza, adhabu hizi siyo rafiki kwa watoto. Tuangalieni upya, tulete adhabu za watoto ambazo hata wakitoka jela wanaweza kufanya kazi zao za kiuchumi. Leo unamhukumu mtoto akiwa na miaka mitano, umemhukumu akae jela miaka 30, ametoka jela akiwa na miaka 35. Je, unafikiria umemjengea mazingira gani katika jamii yake? Kusoma hajui, biashara hawezi kufanya, atafanya kitu gani? Tunamfanya aingie tena kwenye makundi ya wizi, kwa sababu kule gerezani hakupatiwa elimu na kuweza kujisaidia yeye mwenyewe ili kipindi akitoka jela aweze kujisaidia. Naiomba sana Wizara iweze kuangalia. watoto wanafanya makosa, ni kweli hatukatai, lakini wanafanya makosa wakiwa na umri wa watoto pasipo kujielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la udhibiti wa hizi taasisi zisizokuwa za kiserikali. Hivi karibuni tumeshuhudia shughuli ambazo zinafanywa na taasisi zisizokuwa za kiserikali *(NGOs)*. Ni kweli tunazitaka *NGOs* kwenye nchi yetu ya Tanzania, lakini zipo nyingine hazina lengo zuri kwa jamii zetu. Taasisi hizi zinapotosha watoto wetu, tukae tuziangalie upya. Tuna shida gani kuzifutia leseni taasisi ambazo tunahisi zinahamasisha ushoga? Tukae, tufikirie. Naiomba Wizara iangalie kwa ukaribu na ifuatilie kwa ukaribu mashirika haya ambayo tunahisi yako kinyume na maadili ya kitanzania yafungiwe kwa haraka, kwa sababu bado yapo yanaendelea na yanaendelea ku-*support* suala la ushoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunalalamikia mashoga, lakini hatuangalii chimbuko lake ushoga unatoka wapi? Kama tungekuwa tunaangalia ushoga unatokea wapi, tunadhibiti nini, basi tusingefikia huku kwa sababu hakuna shoga ambaye anaweza kuwa mtu mzima akaibuka kuwa shoga. Ushoga unaanzia utoto. Huwezi kuwa shoga mtu una miaka 30 au 35. Ushoga lazima utaanza ukiwa mtoto na kijana, ili ukifika miaka 30 tayari umekomaa kuwa shoga. Naiomba sana Wizara iendelee kuangalia taasisi hizi ambazo haziitakii nchi yetu mema, na kuzifungia taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana katika mitaala yetu ya elimu, tunajua sasa hivi kuna marekebisho ya mitaala ya elimu, lakini tuangalie shule za msingi, watoto wetu waanze kufundishwa somo la ukatili wa kijinsia ili waweze kujitambua na kujikinga na ukatili. Kama tutawafundisha watoto wetu mapema, likiingizwa kama somo, watoto wetu wataelewa unapofanyiwa hivi ni udhalilishaji; na unapofanyiwa mambo haya uripoti wapi. Kama hatujafanya hivyo, hatuwezi kuwalinda watoto wetu. Mtoto hajijui kama hiki ninachofanyiwa ni udhalilishaji, wapi niripoti? Leo tunawaimbisha watoto sawa, ukifanya hapa *don't touch me*, ukiguswa hapa *don't touch me,* lakini bado hatujawapa uelewa zaidi. Tuendelee kwenye mashule kuweka kama *subject* ili watoto wetu waweze kujitambua.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

## TAARIFA

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, anachokiongea Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kabisa kwa sababu hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 30 wanasema wamefungua madawati 1,500 na kitu kwenye shule za msingi, na tunajua walimu wengi wana vipindi. Ni wakati sahihi sasa wa Serikali kuajiri Maafisa Ustawi Wajamii wengi kwa ajili ya kila shule kwa ajili ya kusaidia watoto wetu, kwa sababu walimu ni wachache, hawawezi kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, tukiajiri Maafisa Ustawi wa Jamii, wanaweza kusaidia hili jambo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira na muda wako umekwisha. Inapokea taarifa hiyo?

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo lakini tuzingatie zaidi kuanzisha masomo haya kwenye elimu zetu za awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Munira nilitaka umalize mchango wako kwanza. Umezungumza hapa habari za mwigizaji Kanumba, umezungumza pia kuhusu mwigizaji mwingine Elizabeth Michael. Sina nakala ya hukumu hapa, maana ninachojua yuko nje. Sasa sijui kama alihukumiwa ama aliachiwa, maana umesema aliua. Kwa hiyo, sasa ili tujue kama aliua ama hakuua, ni lazima tuwe na taarifa. Kama wewe unayo mahususi, taarifa hiyo tutaiacha kama ilivyo. Kama huna hakika na Mahakama kama ilimkuta na hatia ama Hapana, utayafuta hayo maneno.

Pia kuhusu yule marehemu sasa, na hiyo kesi yake ambayo angekuwa nayo kama angekuwa hai, kwa kuwa hiyo kesi haipo, naye mwenyewe hayupo hai, nadhani itakuwa ni kufikiri

mbali, na kwa sababu ni kesi ambayo ni nzito kwa muktadha huu, utayaondoa hayo yote mawili.

Kwa hiyo, nakupa nafasi.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba kuondoa, lakini nimeyaongea hayo kupitia yale ambayo yalikuwa yamejitokeza, kwa sababu tuliona Lulu alihukumiwa, ndiyo maana nilijaribu kuongea hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuyaondoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa sijaelewa kama hapo ndiyo umefuta, ama vipi. Alihukumiwa? Nimekupa uhuru, kama una uhakika Mahakama ilimkuta na hatia, utakuwa uko sahihi, lakini kama Mahakama haikumkuta na hatia, maana mimi sijasoma, ndiyo maana nakupa wewe mwenyewe ambaye ndio umeileta hiyo hoja. Kama una uhakika Mahakama ilimhukumu kwa sura hiyo, tuache hivyo Taarifa Rasmi za Bunge. Kama huna hakika uyaondoe.

maana mimi sijasoma ndio maana nimekupa wewe mwenyewe ambae ndo umeileta hiyo hoja. Kama una uhakika Mahakama ilimhukumu kwa sura hiyo tuache hivyo Taarifa Rasmi za Bunge. Kama huna hakika uyaondoe.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, maomba kuyaondoa.

**SPIKA:** Na ya kanumba?

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, yote nimeyaondoa.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Pfofesa Skukran Elisha Manya, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia mada iliyoko mbele yetu. nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai hadi leo. Niwashukuru Wabunge Wote, Mheshimiwa Spika na Katibu wa Bunge kwa jinsi ambavyo mliweza kuniliwaza na kunihudumia nikiwa hospitali. Ninaendelea kuwashukuru Madaktari wote walionihudumia. Leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia baada ya mwaka mmoja. Namshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza waziri kwa uwasilishaji mzuri, nimemsikiliza vizuri nampongeza yeye, Naibu wake na timu yake yote. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya nchini mwetu ambazo zimetuongezea sifa ndani ya nchi na nje ya nchi. Pia wanawake, vijana na watoto tumeona maendeleo ya wazi ambayo kila mtu bila hata ya kumuonesha anaona kwamba nchi imebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la ukatili na unyanyasaji. Wengi tumekuwa tukizungumzia watoto,wanawake na wazee. Leo hii ninaomba nizungumzie ukatili na unyanyasaji unaofanyika kwa wafanyakazi wa ndani, wengi huwa hatulioni. Wafanyakazi wa ndani wanaendelea kunyanyaswa na kufanyiwa ukatili. Wafanyakazi wa ndani hawana likizo, wafanyakazi wa ndani hawaumwi, wafanyakzi wa ndani ndio madakatari, wafanyakazi wa ndani ndio ma–*nurse,* wafanyakazi wa ndani ndio kila kitu lakini bado wanalipwa mshahara mdogo. Nilikuwa naomba Wizara iwapitie na kuangalia jinsi gani wanaweza kulisaidia kundi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala pia la watumishi wa kada hii ya Wizara ya maendeleo ya jamii. Kada hii asilimia kubwa imesahaulika. Ukifika hata ndani ya halmashauri au kwenye ofisi yoyote, ofisi ambayo utaona haina gari itakuwa ni hiyo ya Maendeleo ya jamii, ofisi ambayo haina *furniture* nzuri ni hiyo ya maendeleo ya jamii, Ofisi ambayo watu wake wanachelewa kwenda kusomeshwa nje ya nchi ni hiyo ya maendeleo ya jamii. Ofisi ambayo yale mambo ya hovyo hovyo yanayotakiwa yawepo pale basi watapewa Wizara ya maendeleo ya jamii. Nilikuwa naomba Mheshimiwa waziri, alifuatilie suala hili na wale pia awatoe. Wale nao wapo kwenye ajira kama walivyo wengine. Wapewe mshahara mzuri, wapewe posjho nzuri na wao pia wasomeshwe ili waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika hiyo hiyo maendeleo ya jamii, Vyuo vyao vingi vimechakaa na vilijengwa zamani. Sisi wakati ule ndio tulikuwa tunakwenda tunawafuata mama zetu tunaita wanaenda kwenye *community center,* huko ndiko walikuwa wanakwenda kujifunza vitu. Majengo yale tunaomba yakarabatiwe ili yawe ya kisasa yapendeze na watu wapate hamu ya kwenda kujifunza kutoka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nilikuwa naomba bajeti ya wizara hii iongezwe. Wizara hii ina mambo mengi kama unga wa ngano, kwenye chapati, kwenye mandazi, kwenye sambusa, kwenye nini, ndio wizara hii. Sasa iongezewe pesa ili iweze kufanya kazi zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wizara hii pia ndio inayoongea na jamii yetu kwa haraka zaidi. Ninaomba wakaongee na wajasiriamali kuhusu suala la mikopo. Mheshimiwa Waziri, kama huna taarifa huko mitaani kuna mikopo inaitwa kichefu chefu, kuna mikopo inaitwa kibangala, kuna mikopo ya rusha roho, kuna mikopo ya komandoo, kuna mikopo ya miyeyusho, kuna mikopo pasua

moyo. Haya yote ni mikopo ambayo wakinamama wanahangaika nayo na mingine inawadhalilisha. *(Makofi)*

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nani amesimama? Mheshimiwa Felista Njau.

## TAARIFA

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ninataka nimpe taarifa Mama anayechangia kwamba kuna mkopo unaitwa Kausha damu na sasa umesababisha wanawake wengi wameachika kwenye ndoa na kufirisika kabisa. Kwa sababu una riba kubwa na unalipa kila siku. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Malembeka, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya mikopo ya kausha damu ninaipokea. Ninaipokea kwa sababu hiyo ni moja ya ile mikopo ninayosema inawadhalilisha wakinamama. Kuna mikopo ambayo wakinamama unaenda kulipa mwili badala ya pesa. Kuna wanaume wamekaa huko *standby* wanaitwa mzee wa vikoba. Yaani mama akakope yeye kazi yake kulipa tu lakini analipa mwili, hii inatudhalilisha wanawake. Waziri, pita huko kwenye vikoba, pitia angalia wanakwendaje, tutakwisha magonjwa mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala la mabinti mama. Tunao mabinti wetu ambao wamepata watoto wakiwa na umri mdogo. Familia nyingi zimekuwa kwamba akishapata yule mtoto, wanamsusa au wanamtenga badala ya kumuweka karibu, kumwelekeza na kumsaidia. Jinsi wanavyozidi kumtenga ndivyo ambavyo wanatupa watoto, mara utasikia kaokotwa

kwenye jalala, mwingine anampelekea bibi yeye mwenyewe aingie mtaani kwenye biashara nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuwapunguzie mzigo wakina bibi kulea wajukuu. Basi wale mabinti-mama tukae nao tuongee nao, tuwape elimu ya ujasiriamali, tuwape mikopo wafanye kazi ili walee watoto wao waache kuwapeleka kwa bibi zao lakini pia nao waache kazi hiyo nyingine ya ziada wanayokwenda kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia maeneo ya vitambulisho vya wajasiriamali. Vitambulisho vilitolewa na baadae vikasitishwa wakasema wanaenda kuboresha, waziri atakapokuja naomba aje aniambie hivyo vitambulisho vimeboreshwa nini na vitapewa lini kwa hawa wajasiriamali? Kwa sababu huko mtaani usumbufu uko pale pale, haijulikani aliyepewa kitambulisho wala asiyepewa kitambulisho. Wanasumbuliwa maeneo ya biashara, wanasumbuliwa mara leseni, yaani ili mradi shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kwa hao hao wajasiriamali na wafanyabiashara, ilizungumzwa kwamba watengewe maeneo kwa ajili ya kufanya biashara zao. Kuna halmashauri nyingine maeneo wametenga lakini wametenga tu eneo, vile vitu muhimu vya kupeleka pale havipo ni sawa sawa na hakuna. Unamwambia mtu kafanye biashara pale hakuna wateja, hakuna maji, hakuna usafiri, hakuna choo yaani ili mradi tu kero. Sasa, waziri atakapokuja hapa atwambie wapi ambapo wameandaa vizuri wakashinda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwapongeze wa Dodoma. Tumeona pale Dodoma aneo lao la wajasiriamali ni zuri na lina huduma nzuri. Sasa tunaomba na halmashauri nyingine zifuate hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala lingine la baba lishe na mama lishe. Hawa kila siku mimi nasema unaongea nao, kwa sababu nimekuona maeneo mengi ukiwa unafanya vikao na mama Lishe na baba Lishe na wajasiriamali wadogo wadogo kwenye vikundi. Pamoja na kuwatengea maeneo, je, yale maeneo mnayowatengea kweli yanawateja? Kwa sababu mtaji wao ni mdogo, unapompeleka kwenye eneo akafanye biashara wateja hana unajikuta kwanza hata kile chakula anakula mwenyewe na watoto wake. Kwa hiyo, hafanyi biashara. kwa hiyo, mnapowapangia maeneo ya kufanya biashara muangalie je, hapa wateja wapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mchango wangu huu wa leo ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munira Khatib, nimeipata hukumu ya Elizabeth Michael, alitiwa hatiani na Mahakama. Kwa hiyo, pamoja na kwamba ulikuwa umefuta nikupe nafasi kwa sababu ni haki yako. Nimetafuta huku hukumu na nimeiona alitiwa hatiani. Kwa hiyo, alitoka kwa msamaha wa Rais.

Mheshimiwa Munira Khatib, mchango huo unaweza kuurejesha kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, naomba nifute kama nilivyokwisha kufuta lakini nilikuwa naonesha watoto baadhi wanaweza na wao kupata msamaha lakini nimefuta.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira, wewe nisikilize mimi hao majirani kidogo wanapoteza mambo hapa. Nisikilize mimi, nasema hivi maelezo ya mchango wako uliyokuwa umeyaeleza kuhusu kesi hii kwamba, Elizabeth Michael, alihukumiwa, ndipo lilikuja swali langu “una uhakika

alihukumiwa au aliachiwa?" Sasa Mahakama kwa taarifa zilizopo kwenye hiyo kesi alihukumiwa.

Sasa kama unataka kuurejesha ule mchango wako kama unavyosema kwamba nia yako ilikuwa ni kwamba kuna mambo hayo yanatokea. Kwa hiyo, weka sasa mchango wako vizuri umepewa hiyo nafasi. Kwa hiyo, unaweza kuurejesha ama ukaufuta lakini ni uchaguzi wako maana umefuta hoja baada ya mimi kusema na nimerejea tena kwako baada ya kujiridhisha lazima upewe haki yako.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, naomba kurejesha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Mwanaidi Ali khamisi, Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambae anataka Bunge lako liweze kumpitishia bajeti ya bilioni 74.2 ili aweze kutekeleza majukumu yake. Pia, mimi nitangulie kuunga hoja mkono kwamba Waziri tutakupitishia bajeti hiyo ili uweze kwenda kushughulikia ustawi wa jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitangulie kumpongeza waziri pamoja na naibu wake na watendaji wake kwamba, wizara yao ndani ya muda mfupi tangu imeundwa wameweza kutengeneza miongozo na kuanzisha madawati ambayo watatathimini utendaji kazi wao ili mwishowe tuweze kuona kwamba wanafikia ule ufanisi ambao unatarajiwa baada ya kuandaa hiyo miongozo pamoja na madawati waliyoanzisha mahali pote yalipo aanzishwa. Lengo ni jamii yetu iendelee kupata

ustawi na maadili yaweze kupatikana lakini pia kushughulikia changamoto ambazo zinaikabili jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, asubuhi ya leo ningependa kutoa mchango wangu kuhusu sehemu moja ya kwanza inayohusiana na elimu ya makuzi pamoja na malezi ya mtoto.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa tabia ya mtu inafanyika katika miaka saba ya awali. Katika miaka saba hii ya awali ndipo mtoto katika akili yake changa anaweza kuelekezwa mambo yaliyo mema na akili yake changa iko tayari kupokea kutoka kwa wazazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunaambiwa kwamba katika miaka hiyo saba ile mitatu ya awali ndiyo ya msingi kabisa maana ndipo tunapojenga msingi wa kupokea maadili, msingi wa kuchambua yaliyo mema na ndio maana napenda nitumie mitahli moja inayotoka katika kitabu cha Mithali 22:6 inasema "Umlee mtoto katika njia impasayo naye hataiacha hata atakapokuwa mzee".

**MBUNGE FULANI:** Haleluya.

**MHE. PROF. SHUKRAN E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, sasa, kama hilo ndilo hoja ya kwamba malezi ya mtoto angali mtoto mdogo akilelewa vizuri hataweza kuiacha njia hii hata uzee wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni nini? Katika kipindi hiki cha miaka ya awali na ndio mana tunapendekeza miaka hii ya awali, mtoto aweze kukaa na wazazi wake. Wazazi wake wapate namna ya kumuingizia maadili wanayoyataka wao. Kwa hiyo, ndio muda wa kumlinda mtoto yaani *first line of defense* (hatua ya kwanza ya ulinzi wa maadili ya mtoto ni

akiwa nyumbani kwao) ndipo ambapo anawekewa misingi ambayo ataweza kuiishi hata huko baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anapokuwa amelindwa ndio muda wa kumweleza mtoto kwamba wewe ni wa jinsia ya kike, wewe ni wa jinsia ya kiume na wala hakuna *trans gender* wakati huo akiwa mdogo. Yaani asifike mahali eti akishakuwa mtu mzima anakutana na mafundisho ya kwamba eti kuna jinsia ya katikati hapa, hapana. Akiwa mtoto mdogo ndio wakati wa kumweleza, ndio wakati wa kumweleza mtoto, wewe unapaswa kujitambua kwamba ukiwa wa jinsia ya kiume au ya kike hakuna kuguswa na mtu yeyote yule sehemu zako za siri. Huu ndio wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ndio wakati wa kumuonesha mtoto upendo, ndio wakati wa kumuonesha mtoto imani, kujenga naye imani na ujasiri wa kwamba iwapo mtu awae yote si mjomba, si baba mdogo, si shangazi, mtu awae yote atakapo kutendea jambo lolote ambalo si jema baada ya kumfundisha jema, apate imani na ujasiri wa kuja kumwambia baba yake au mama yake kwamba fulani amaenitendea hivi, huu ndio wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kwa jinsi hiyo kama hivyo ndivyo, huu wajibu unawaangukia wazazi na hasa akinamama. Na ni wajibu ambao haupaswi kuahirishwa wala haupaswi kupokezana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi hiyo niombe sana, yawezekana kweli jamii yetu inahangaika kutafuta mali, yawezekana kweli tunajaribu kutengeneza namna ya kujenga chumi zetu za familia, ni kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni wajibu ambao hauhamishiki, kwa sababu ni wajibu ambao hauwezi

kuahirishwa, wazazi tusiseme huu usemi ambao tunapenda kusema kila wakati "sina muda" hapana. Wazazi tutenge muda hata kama majukumu yetu ni makubwa kiasi gani yanatutaka, ni lazima kila siku inayopita tutenge muda wa kukaa na watoto wetu na usemi wetu wa kusema sina muda hiyo sio usemi unaopaswa kusemwa na mtu aliye na mtoto mdogo ambae ni mzazi anaetambua kwamba huu ndio wakati wa kujenga maadili ya mtoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbona hata kama tunakuwa busy mbona tunakuwa na muda wa *whatsApp, twitter* na *facebook* katika simu? Si ni bora tuache hiyo *Facebook,* tuache hiyo t*witter* lakini tupate muda wa kujenga maadili ya Taifa lijalo. Tukifanya hivyo, mafundisho yote yanayokuja yale ambayo ni potofu hata haya ya kumwandaa mtu katika kumuingiza mtindo wa ushoga, kama ameandaliwa vizuri mtoto atakuwa anajitambua na mtoto atakataa kushawishiwa katika maadili potofu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wazazi lazima turudi tuchukue sehemu yetu, tukae kama wazazi, tufanye wajibu unaotuangukia na wala tusisingizie shughuli za kuingiza mali au shughuli za uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa namchukua huyu mtoto kwamba pale nyumbani ameandaliwa vizuri, baadae anatamani kwenda kwenye jamii, yawezekana ni shule au yawezekana kupata masomo ya dini huko. Lazima tuweke mifumo thabiti na salama inayomhakikishia huyu mtoto ulinzi wake.

Mheshimiwa Spika, ninaposema hivi ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri, atasema ameanzisha madawati lakini ni lazima tuweke mifumo rahisi na myepesi ya kushughulikia iwapo hawa ambao wamepewa dhamana ya kumlinda na kumtunza wanakwenda njia ambayo sio. Maana kama walivyosema

wenzangu, watu wengine ambao wameaminiwa ni shule, viongozi wa shule, wameficha maovu haya wakitamani kuyamaliza kwa njia nyepesi, hapana. Kwa hiyo, Serikali iweze kuweka mfumo ambao ni rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kama muda wangu umekwisha.

**SPIKA:** Dakika moja.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, niongelee hoja ya mtoto yatima. Mtoto yatima akiwa *private school* (shule ya binafsi) inakuwa vigumu kurudishwa katika mfumo wa shule za Serikali. Kwa hiyo, katika dawati lake inapotokea mtoto yatima wazazi wake wamefariki, Serikali iweze kurahisisha namna ambayo huyu mtoto anaweza akasaidiwa kutoka shule ya binafsi kurudishwa katika shule ya Serikali ili wazazi wasiweze kupata shida sana katika kumhudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja ya hotuba ya bajeti ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Kwanza kabisa ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Dorothy Gwajima pamoja na Naibu Waziri, Mwanaidi na viongozi wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaifamnya.

Mheshimiwa Spika, natambua jitihada za Bodi ya Uratibu wa *NGOs* chini ya uongozi mahiri wa Mama yangu Mheshimiwa Mwantumu Mahiza pamoja na jitihada za Ofisi ya Msajiri wa

*NGOs* katika kuhakikisha kwamba *NGOs* zote ambazo zinasajiriwa hapa nchini zinafanya kazi kwa kile ambacho wamekiombea lakini pia kwa kufuata mila tamaduni na desturi zetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda pia kutumia fursa hii kuwasihi sana viongozi wa dini, viongozi wa kisiasa pamoja na viongozi wa Serikali ngazi ya jamii na katika maeneo yetu yote waweke jitihada ya kuhakikisha kwamba tunazitambua *NGOs* ambazo zifanya kazi katika maeneo yetu ili nasi tuwe sehemu ya mabalozi wa kuhakikisha ya kwamba *NGOs* kwenye maeneo yetu wanafanya kazi kulingana na mila tamaduni na desturi, ikiwemo yale ambayo walisajiriwa nato.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua mchango mkubwa wa *NGOs* katika maendeleo ya jamii. Na kipekee nakishukuru tena chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kutambua umuhimu wa mchango wa mchango wa *NGOs* na hata kupelekea kutenga nafasi zake mbili za viti maalum kwa ajili ya *NGOs* ndani ya Bunge lako Tukufu. Niko mimi nawakilisha *NGOs* kwa upande wa Tanzania Bara lakini yupo pia na Dada yangu Mheshimiwa Khadija Aboud ambaye anawakilisha *NGOs* kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii mimi nitajielekeza kwenye maeneo matatu, eneo la kwanza ni *local content* kwenye sekta ya *NGOs.* Lazima tuweke jitihada za makusudi kabisa kuhakikisha kwamba *NGOs* za ndani zinaweza kunufaika na miradi mbalimbali inayoingia nchini pamoja na ufadhiri. Kwa takwimu za Ofisi ya Msajiri wa *NGOs* kwa mwaka jana jumla ya tirioni 1.1 zimeingia na kuratibiwa kupitia *NGOs* hapa nchini; lakini cha kusikitisha asilimia 70 imepita kwenye *NGOs* za nje kwa maana za kimataifa na ni asilimia 30 tu ambayo imepita kwenye *NGOs* za ndani kwa maana ya *NGOs* za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kupendekeza kwa Serikali kuputia Wizara hii waone namna ya kuweka mwongozo ambao utaratibu vizuri, kwamba fedha zinapoingia Tanzania kwa ajili ya miradiya maendeleo ngazi ya jamii lazima *NGOs* za ndani zipewe kipaumbele. Hiyo itasaidia moja, kuhakikisha kwamba *NGOs* zetu zinafanya kazi kwa kuzingatia mila tamaduni na desturi, lakini pili kuhakikisha kwamba *NGOs* zetu zinaweza kukua na miradi inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kuzungumzia ni kwamba bado kuna sintofahamu kubwa katika sekta ya *NGOs* na masuala mazima ya kikodi. Natambua kwa upande wa sekta binafsi wanayo kamati ya maboresho ya sera za kodi, yaani wanaita *thick tank,* ambayo mara nyingi sekta binafsi inakaa na Wizara ya Fedha na Mipango na wanajadili changamoto mbalimbali za kikodi na wanazipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Mimi ningependa kupendekeza kupitia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum sekta ya *NGOs* iweze kupata kamati ya kikodi ambayo itakuwa inakaa inajadiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu changamoto za kikodi na kupata utatuzi wake.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo ningependa kulichangia katika eneo hili ni kwamba, kuna umuhimu mkubwa sana wa *NGOs* kushirikishwa katika mipango mbalimbali ya Serikali Wizara hii inagusa masula ya jinsia masuala ya wanawake ambapo masula ya uongozi na ushiriki wa wanawake katika siasa ni moja ya majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, kama ambayo tunatambua Serikali inakwenda kufanya maboresho ya Sheria za Vyama vya Siasa, Sheria za Taifa za Uchaguzi na hata pia mchakato wa katiba mpya. Mimi niombe sana Wizara hii kupitia Mheshimiwa Waziri

kuhakikisha kwamba katika michakato ya sheria hizo *NGOs* zinashiriki ipasavyo lakini pia katika mchakato wa katiba mpya *NGOs* si tu zinashiriki lakini pia zinawakilishwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, naomba niwapongeze tena Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania tutambue mchango mkubwa ambao unafanywa na *NGOs* ngazi ya jamii kwa sababu NGOS ndizo ambazo zinashirikiana na Serikali kufikisha huduma pale ambapo Serikali haiwezi kufika, kufikisha maendeleo pale ambapo Serikali haiwezi kufikisha, kwa hiyo ni muhimu tufanye kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini naendelea kusisitiza pia sisi kama viongozi na viongozi wa dini viongozi wa kisiasa viongozi wa kiserikali lazima nasi pia tuwe tunajukumu la kuhakikisha ya kwamba *NGOs* hizi zinafanya kazi kwa matakwa ya sheria zetu, Katiba yetu mila tamaduni na desturi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, nasisitiza tena umuhimu wa kuwa na Kamati ya kikodi baina ya Sekta ya *NGOs* na Wizara ya Fedha na Mipango ili tuweze kuhakikisha tunatatua changamoto za kikodi zilizopo. Nasisitiza umuhimu wa kuhakikisha kwamba Serikali inakuja na mwongozo ambao utapelekea *NGOs* za ndani ziweze kupata rasilimali fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii, pia naipongeza Serikali kwa bajeti hii, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Serikali kwa kuisaidia Wizara kuweza kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu Maafisa Ustawi wa Jamii wanafanya kazi kubwa sana na wanafanya maamuzi ya kesi mbalimbali za wakubwa na Watoto, lakini hawapewi posho yoyote kwa kazi kubwa wanazofanya. Utakuta wanaamua kesi moja kuanzia asubuhi mpaka usiku. Kazi kubwa sasa wanafanya maafisa hawa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara hii kwa kutoa mikopo kwa vijana na kuwezesha mikopo hiyo kurudishwa. Si jambo rahisi sana kwa wakati tulionao hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni vyema wale wanaohusika na fedha za Halmashauri wakajifunze kwa Wizara hii.

Kuhusu ongezeko la watoto watukutu mitaani naomba sana Serikali isaidie kuwatoa watoto wanaoombaomba mitaani kwani wanajifunza tabia mbaya. Ni bora waombe watu wazima lakini wasiwe na watoto wao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja bajeti hii ipite kwa kishindo.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dkt. Dorothy Gwajima

na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi 74,223,193,000 kutekeleza shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kuhusu hali ya wazee hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika vipaumbele 10 vya Wizara kwa mwaka wa 2023/2024, kipaumbele namba nane kinasema; "kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki za watoto na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee."

Mheshimiwa Spika, kutokana na kipaumbele hicho cha Wizara hapo juu, ni dhahiri kwamba masuala ya wazee yanahitaji msukumo wa kipekee. Tunaishukuru Wizara kwa kutenga shilingi bilioni 1.8 kusaidia wazee kwa mwaka huu wa pesa wa 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, wazee ni watu muhimu ambao wengi wametulea. Wazee wengi huko vijijini wamechoka, hawana uwezo na inalilazimu Taifa kuwatazama.

Mheshimiwa Spika, wazee wengi wanachukuliwa kama tabaka lililotengwa, hivyo ni vyema wakahudumiwa na kupatiwa matibabu, makazi, vyakula, kuwasaidia fedha za kujikimu kama ilivyo kwenye mataifa mengine na majirani zetu wa Zanzibar kupitia *Pension Jamii.*

Mheshimiwa Spika, kuna sera inayosema matibabu ni bure kwa wazee, lakini wakienda hospitali wanaambiwa ni wale wasiojiweza na wanakosa dawa na matibabu.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayowakabili wazee wetu ni ukatili dhidi yao. Ukatili huu umekuwepo kwenye baadhi ya jamii yetu kwa miaka mingi. Jambo hili halijatiliwa mkazo unaostahili katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, ukatili huu unafanywa katika ngazi ya kaya na vijiji na watu wa karibu ambao ndiyo hutambulika kama wasaidizi wa karibu wa wazee katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu, ninaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

Kwanza, Serikali ishiriki kwenye kujengea uwezo mashirika yanayojihusisha na masuala ya wazee, mabaraza ya wazee ngazi ya mikoa na wilaya, asasi za kutetea haki za binadamu na kuchukua juhudi za kuielimisha jamii juu ya haki za wazee na umuhimu wa kumlinda mzee.

Pili, Serikali ipange bajeti ya kutosha ya kuwahudumia wazee wasiojiweza na kuhakikisha wanapata tiba, makazi na chakula. Kiasi cha shilingi bilioni 1.8 zilizotengwa kwa mwaka 2023/2024, hazitoshi.

Tatu, Serikali iwalipe wazee *Pension Jamii* kama ilivyo huko Zanzibar.

Nne, Serikali itenge fungu maalumu kuwasaidia wazee waanzishe miradi ya kujiongezea kipato kama vile ufugaji wa kuku, nyuki, mbuzi na ng'ombe.

Tano, Serikali ifikirie kuwa na wawakilishi wa wazee huku Bungeni kama kundi maalumu kwani makundi ya vijana na akina mama wana uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaidi Ally Hamis, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mwanyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo kuwa na hali ya uzima wa afya na kushuhudia bajeti ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum ambayo leo inasomwa tarehe 18 Mei, 2023.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Waziri kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hasan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipendelea na kuniamini kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalum. Lakini pia niwashukuru viongozi wote wa Wizara na watendaji kwa kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya pekee naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum kwa maelekezo na ushirikiano wa hali ya juu anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wangu wakuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Isdor Philip Mpango kwa kuendeleza vyema na kutusimamia katika Wizara yetu hii na kuhakikisha tunakwenda vyema na tunatekeleza majukumu yote ambayo tunahitaji. Lakini pia sina budi kuwashukuru familia

yangu kwa kunipa wepesi na kufanya kazi zangu kwa urahisi ili kuhakikisha kazi zangu zote zinakwenda kwa salama na amani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba nitamke rasmi kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia 100, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hizi. Niishukuru Kamati ambayo imeungana na sisi katika kutuelekeza hoja zetu na kutupa maelekezo ambayo tutayafanyia kazi kadri wanavyotuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru waunga hoja wote ambao wamechangia katika Wizara yetu hii ya Maendeleo ya Jamii, wengi wamezungumzia masuala ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wetu. Ni kweli Serikali yetu sasa hivi tuna kazi kubwa ya kuelimisha na kutoa elimu kwa wananchi kwa ajili ya watoto wetu kutokana na mmonyoko wa maadili ambao unaendelea katika nchi yetu. Suala hili limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, na sisi kama Wizara tutaendelea kutoa elimu kuhakikisha kwamba watoto wetu wanakuwa salama. Nitoe msisitizo kwa wazazi, wazazi, ukatili wa kijinsia unaanzia katika nyumba zetu, kwa hivyo wazazi tuhakikishe tunapata muda wa kushirikiana na watoto wetu na kukaa na watoto kuwapa elimu ili wao waweze kuelewa mila na desturi za utamaduni wetu katika nchi yetu hii ambazo zinaendelea ambapo nchi nyingi wanapenda mila zetu na desturi zetu katika nchi hii na wanapenda kuziiga; lakini wanakuja kwa mlango wa nyuma kuhakikisha kubomoa utamaduni wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai tu kwa wazazi walezi jamii kujumuika katika malezi makuzi na matunzo ya ukuzi wa mtoto ili kuwawezesha famila kuwa sehemu salama kwa watoto, kuishi na kufurahia haki zao katika hatua mbalimbali. Hatua kali tutazichukua kwa wale wazazi ambao wanajua kama mtoto wao huyu ana matatizo lakini akamwachia kwa makusudi tunaomba wazazi kwamba mtoto ukimuona ana matatizo basi

Wizara ipo, mfikishe pahali salama, sisi Wizara tutaweza kumhudumia.

Mheshimiwa Spika, mtoto ambaye unamuona nyumbani humuwezi sisi Wizara tuna vituo vyetu vya kulelea Watoto, tunalea watoto kwa kutumia haki zote zile ambazo wanazozihitaji. Mtoto anahitajika kupewa haki zote za msingi kuanzia elimu mavazi na kila kitu ili aweze kukua vizuri na kukua katika saikolojia nzuri, kwa sababu tunawahitaji sana. Watoto tunawahitaji kwamba, ni viongozi wetu wa kesho, tusipowapa malezi bora hivi sasa basi tutakuwa na taifa ambalo halina viongozi bora. Hivyo tujitahidini wazazi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu niwaombe Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa katika majukwaa basi watoe elimu hii kwa wazazi na walezi ambao wanalea watoto hawa ili kuhakikisha malezi na makuzi yanaenda salama.

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa wito kwa jamii na watu wenye moyo wa kutoa huduma kwa malezi na makuzi kwa watoto wa kambo kuhakikisha kwamba wanawalea watoto hawa kwa kuzingatia ubora na haki zote ambazo zinahitajika. Lakini pia kuna Waheshimiwa wengine hapa wamezungumzia kuhusu mmonyoko wa ndoa na mirathi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mmonyoko wa ndoa unaotokana na ukatili wa jinsia kwa wanawake. Kuna waume wengine wanakuwa hawana imani kwa wake zao. Jambo linaweza kuwa dogo lakini wao wanalichukulia kubwa na kuwapiga wengine hadi kufikia kuua. Niwaombe wazazi wenzangu wanapofikia hadi hali hiyo watoe taarifa katika vyombo husika, wasikae kimya, sheria zipo zinaowalinda.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kuwa na haki kamilifu basi unatakiwa utoe uwazi wote mahakama itakusikiliza na ikupa

haki yako. Na ndoa ambazo tunazihitaji zote zitasikilizwa. Ili mtu aweze kupata urithi basi ndoa hizo tujitahidini tunapokutana na wapendanao basi tukazisajiri ndoa zetu, ili kuhakikisha kwamba mirathi ile inakwenda kutokana na taratibu; na kila mtu anadini yake ambayo anapokea mirathi kutokana na mtiririko wa usawa na ugawaji wa mirathi hiyo.

Pia nizungumzie kuhusu watoto wa mitaani. Ni kweli kuna tatizo la watoto wa mitaani, lakini watoto hawa wanatokana na mmonyoko wa maadili kwa wazazi. Wazazi wanapokuwa hawafahamiani, wanapogombana basi hawashughulikii watoto na watoto wale wanaanza kuingia mitaani. Hili linaipa mzigo mkubwa Serikali. Serikali sasa hivi tumeamua, tumeunda Kamati ambayo itawasimamia watoto hawa ili kuhakikisha kwamba watoto ambao wapo mitaani tunawarejesha kwa wazazi wao, na mpango huo, tunamhitaji mzazi huyo tutapomkabidhi basi tutampa masharti ambayo mtoto atakaporudi tena mtaani basi tutamkamata yeye kwa sababu vipo vituo ambavyo vya kupeleka malalamiko na vipo vituo ambavyo mtoto anaweza akasaidiwa kuhakikisha anapata haki zake zote.

Mheshimiwa Spika, pia kuna vituo vyetu vya malezi ya Watoto, ambapo tuna Kikombo – Dodoma na Dar es salaam – Kurasini. Watoto hawa tunawalea na tunawapa haki zao zote za msingi na malezi bora, kwa hivyo watoto wetu hawa tuwatunze.

Mheshimiwa Spika, mmomonyoko wa maadili upo lakini tuhakikishe tunafanikisha sisi wazazi. Mtoto halelewi na mzazi mmoja au mzazi peke yake. Utamaduni wetu huko nyuma wazazi tunalelewa mpaka na majirani. Mama Salma hapa ana msemo, anasema mtoto wa mwenzio ni wako. Wahakikishe kwamba tunashirikiana, na wazazi tuwape watoto malezi bora.

Mheshimiwa Spika, pia kuna jambo jingine ambalo limesemwa hapa na Waheshimiwa kuhusu wafanyabiashara wadogowadogo. Ni kweli wafanyabiashara wadogowadogo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaamini na amewajali na kuwaleta katika Wizara yetu hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ili kuhakikisha na wao wanapata fursa mbalimbali za kufanya biashara ili waweze kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii Mheshimiwa Rais ameiunda kuhakikisha kwamba amaeona kwamba wanawake wengi walikuwa wanapata tabu na biashara zao, hawana sehemu za kuzipeleka hawana sehemu za uhakikika kuhakikisha biashara zao zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametoa fedha takriban mikoa yote 26 na kuhakikisha kwamba kunawekwa Wizara ambazo zitawasaidia hawa wajasiliamali wadogowadogo, hasa wamachinga, nao watajisaidia katika Wizara zile na malalamiko yao yote basi katika ofisi hizo ambazo ametoa pesa Mheshimiwa Rais basi zitasaidia katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwaona na kuwajali wananchi hawa na kuhakikisha na wao wanakua kiuchumi ili nchi yetu iwe na usawa. Kama yeye mwenyewe alivyoamua kuwa kinara wa usawa wa kijinsia basi tumshike mkono ili kuhakikisha Taifa letu linakua na linaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mbalimbali ambayo yamefanyika katika Wizara hii. Tunazidi kutoa elimiu Wizara yetu kuwaelimisha wananchi kuhakikisha wanapata elimu ya ukuaji wa maendeleo yao. Kwa hivyo tunawakaribisha sana katika

Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ili kupata elimu na kuhakikisha mambo yao yote yanakwenda sawa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi zimesemwa hapa na wajumbe, lakini Mheshimiwa Waziri wangu ataendelea kuzijibu na hoja nyingine zitajibiwa kwa maandishi. Nikushukuru sana na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa hapa mmetoa hoja zenu na kwa ushirikiano mliotupa. Nawatakieni kila la kheri katika mafanikio ya bajeti hii ili ipite na tuendelee kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum ili aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kuhitimisha hoja yangu ambayo imepokelewa na kujadiliwa siku ya leo hapa Bungeni kwenye kipindi hiki cha asubuhi.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuisimamia Wizara hii na kutupatia miongozo na maelekezo ambayo imetufikisha mpaka hapa ambapo Waheshimiwa Wabunge mmeweza kutoa pongezi zenu, tumezipokea, na kutuasa tuendelee na kazi kadri tunavyozidi kuwezeshwa na jemedari wa kwanza Mheshimiwa Dkt, Samia Suluhu Hassan aliyeiunda hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Shukrani zangu ziende kwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Isdor Mpango kwa jinsi anavyotusaidia katika miongozo pamoja na maelekezo na kufuatilia masuala ya usawa wa kijinsia. Kila anapokwenda kwenye shughuli zake za utekelezaji tumekuwa tukimskia akiweka mkazo kwenye masuala ya maadili tuweze kudhibiti mmomonyoko wa maadili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile shukrani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa (Mb), kwa jinsi ambavyo ametoa uongozi kwa mawaziri pamoja na Wizara yetu katika kuendelea kupambana kuboresha huduma za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, nikushuru wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo umekuwa ukiliongoza Bunge lako pamoja na sisi wenyewe Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Kwanza umetuundia Kamati nzuri kabisa ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na kutupatia viongozi mahiri kabisa ambao wameendelea kutupatia uongozi na maelekezo ambayo yametufikisha tulipo. Shukrani kwa Kamati yangu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Toufiq (Mb), ambaye ndio mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa jinsi wanvyoendelea kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wote kwa maswali ambayo mmekuwa mkiuliza na michango ambayo mmekuwa mkitupatia. Hoja mbalimbali ambazo mmekuwa mkizilta zimekuwa chachu ya kutufanya sisi tufikiri zaidi jinsi ya kwenda mbele katika hii Wizara kubwa ambayo leo hapa nimeona ikifananishwa unga wa ngano, na kweli kabisa ni sawa, ina mambo mengi sana kwa sababu jamii na ina mambo mengi sana. Hii ni bahari inayounganisha Wizara zote zingine kwenda kufikia jamii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wenzangu wote ambao wameendelea kufanya kazi hizi kwa ushirikiano wa kisekta na wameweza kuchangia pakubwa hasa katika suala la ajenda ya jukwaa la usawa wa kijinsia ambayo nimeielezea hapa. Haiwezi kutekelezwa na mtu mmoja, hii inatekelezwa na sekta zote. Ukigusa maji, ukigusa kilimo, ukigusa nishati, sisi wote, biashara tunatekeleza masuala haya ya kwenda kumkomboa mwanamke na kumwezesha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi kwa kazi nzuri anayofanya na kunipa ushirikiano, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wangu na watendaji wote, kuanzia ngazi ya makao makuu hadi kwenye mikoa, halmashauri na kata zote. Sifa hizi tunazopata si kwa sababu yangu ni kwa sababu wao wanagusa maisha ya wananchi. Niwashukuru wadau wote niliowataja mpaka dakika hii ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya ya utangulizi niseme kwamba hoja hii ukiacha hoja za Kamati zilizowasilishwa hapa, nakiri kuzipokea hoja hizi na niliahidi Kamati yangu Tukufu kwamba tutazifanyia kazi na kuwasilisha kwa maandishi masuala yote yaliyozungumzwa mle, kuanzia ukarabati wa miundombinu, upatikanaji wa fedha kwa wakati tufuatilie pamoja na kuwezesha upatikanaji wa watumishi ambao ni wachache hasa kundi hili la Maafisa Ustawi wa Jamii. Tutafanya kazi na Wizara za Kisekta kuweza kuona tunafanyaje ili kuendelea kuwezesha upatikanaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, sitaweza kupita kwenye kila hoja ya mchangiaji mmoja mmoja, kwa heshima na taadhima naomba nikuombe niweze kuyaangalia yale masuala machache ambayo yamechangiwa sana na kuweza kuyatolea ufafanuzi kadri muda utakavyo ruhusu. Nikiri hoja zote tumezichukulia kwa

uzito stahiki, tutazifanyia kazi na kuziwasilisha kwa utaratibu wa Bunge kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, nami naomba nianze kuongeza kwenye eneo hili la mmomonyoko wa maadili. Mmomonyo wa maadili limekuwa ni janga kubwa kwa sababu kwanza linagusa watoto ambao ni Taifa la kesho na watoto hawa wanajifunza kutoka kwetu sisi watu wazima, ambao tumepewa baraka na Mungu tuwalete watoto duniani na tumepewa dhama ya kuwalea na kuwakuza.

Mheshimiwa Spika, tunayo mikakati mingi eneo hili, lakini niseme kwamba tumejiongeza tumekwenda mbele. Ukiacha masuala haya ya kusema kwamba tuwawezeshe kina mama kiuchumi kwa kuunda majukwaa haya ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, ambapo Jukwaa Kuu la Taifa tumelizundua jana, tumehakikisha kwamba tutakuwa na kampeni mbalimbali tukishirikiana na haya majukwaa ya kupeleka sauti ya fursa zilizopo kiuchumi maana tuna benki nyingi, tuna wadau wengi na sisi wenyewe Serikali tuna mifuko mingi ya kuwezesha wanawake kiuchumi ili wasiweze kuingia kwenye ukatili lakini taarifa zinakuwa hazifiki kwa wananchi hasa wale wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikizunguka kule, unamuuliza mwananchi unafahamu kama kuna mkopo wa asilimia 10 anakwambia nasikia tu labda hii mikopo ni ya huko kwa wafanyakazi pamoja na watu wa halmashauri. Kwa hiyo tunaona kuna *gap* kule chini kwenye vijiji na kwenye kata. Kwa hiyo kupitia jukwaa hili na kupitia kampeni zetu hizi tumesema ZIFIUKUKI zijuwe fursa, Imarisha Uchumi, Kata Ukatili Kazi Iendelee. Tutahakikisha tunafikisha sauti ya uwepo wa fursa za uwezeshaji kiuchumi mpaka kwenye kata na mpaka kwenye kijiji. Kila mwanamke mmoja mmoja atajua na atajiunga na

jukwaa hili ambalo ndio litakuwa *platform* ya kuwafundisha, kuwajengea uwezo, wataweza kujifunza kutoka kwa wenzao ili tuwakomboe kama mkakati mmoja wa kutokunyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, tuna madawati pia ya jinsia ambayo yapo kwenye Jeshi la Polisi karibu madawati 420, yaani Vituo vyote vya Polisi vina haya madawati na pale tu sio madawati tuna msaada wa kisheria tunaoutoa kupitia Sheria Namba moja, Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017. Wasaidizi wa kisheria wako wengi sana lakini bado wananchi pia hawafahamu. Kwa hiyo, kupitia haya majukwaa pia tutapeleka hii elimu na tutafanya haya matamasha tukiwa tunahusisha na hizo huduma kuzipeleka, sio matamasha tu ya hivi ya kukaa kwenye majumba ni kupeleka zile huduma. Kama ni usaidizi wa kisheria huu hapa, kama ni fursa za kiuchumi hizi hapa.

Mheshimiwa Spika, tumezindua hilo tamasha la kwanza Dar es Salaam, mwishoni mwa Aprili ambapo tulileta taasisi zote zenye fursa za kiuchumi ambapo walihudumiwa wananchi takribani 4,040. Kwa hiyo tunataka tuendelee hivyo kwenye mikoa yote tuifungue nchi, kila mtu ajue uwepo wa hizi fursa isije ikawa wachache tu ndio wanazisikia.

Mheshimiwa Spika, tunakuja na mpango wa pili wa MTAKUWA uliofanyiwa maboresho. MTAKUWA ni Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto baada ya ule wa kwanza kuwa umeisha Juni 2022. Mle ndani tumeboresha, masuala ya ukatili wahusike na Wakuu wa Wilaya wahusike na Wakuu wa Mikoa, wanapojadili taarifa zao za Kamati ya Ulinzi na Usalama kwenye halmashauri na mikoa, wakajadili majambazi, wakajadili na hali ya usalama, wajadili na masuala yanayotishia unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto na wanawake.

Mheshimiwa Spika, tunataka kuzijua hizi *data* zikitokea mikononi kwao, kwa sababu wanafanya hiyo kazi na wana vyombo vyote. Kwa hiyo taarifa zikifika pale na Afisa Ustawi wetu akawasilisha pale, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa ataweza kuviagiza vyombo vichukue hatua kwa wakati badala ya mama huyu kuwa anahangaika pengine yuko mbali kule kijijini, pengine hana hata usafiri, pengine hata Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa hawajui.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaikaribisha hii mifumo yote ya ulinzi na usalama ili pia iangalie hili suala la watoto pamoja na wanawake wanaonyanyaswa. Tumekuja na kampeni nyingine ya "Taifa letu, Maadili Yetu", tumeizindua hapa juzi. Nimemsikia Mheshimiwa Mbunge Mwakagenda akisema tupige sana kelele, sasa tutapiga sana kelele kupitia hii kampeni kwa kipindi cha miezi sita inayokuja na ndio maana tumewaunganisha na vilabu vya mipira, tumewaunganisha na wanahabari, tumeunganisha na jamii yenyewe kupitia wenzetu wa SUMAUJATA, *FAGDI* na tunapata wito na mwitikio mkubwa sana wa wananchi na kila mtu anasema nataka kwenda mstari wa mbele, hasa kupitia hii kampeni. Tutapiga sana kelele ili kufikisha hii sauti kule, sio tu sauti ya kwamba kuna ukatili bali na fursa za kiuchumi kwamba ziko hivi na fursa za kisheria, misaada ya kisheria ili wananchi wajue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru utoaji taarifa sasa unaongezeka si kwa sababu pengine matukio yanaongezeka sana. Awali kasi ya kutoa taarifa ilikuwa asilimia 12, sasa tunainyanyua kwa sababu wanapata ujasiri na kuona kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan yupo kwa ajili yao, Wizara ipo kwa ajili yao, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wako kwa ajili yao. Tunaamini hawa watu sasa kama ilivyo kwenye nyumba ya mtu mmoja ameweka askari wa asili ambao tunasema wanalinda ile nyumba, wakibweka, mwizi anakimbia. Lazima hawa wakatili wajue kwamba Serikali ya Dkt. Samia Suluhu

Hassan iko kiganjani kwa huyu wanayetaka kumkatili na ndio maana tunatengeneza namba za mawasiliano 116 na Wizara inazindua dawati lake hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee eneo lingine kuhusu masuala ya *NGO* hizi ambazo zimekuwa zikihusishwa na masuala haya ya kuchochea mmomonyoko wa maadili. Tulipata hivi karibuni taarifa za wanaharakati ambao pia walikuwa wakishirikiana na Mwakyembe ambaye alikuwa ni Waziri mstaafu kusema kwamba kuna hii hali huko kwenye jamii, baadhi ya mashirika yanahusishwa na kuchochea hivi vitendo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imechukua hatua ya kuyaita yale mashirika yote yaliyokuwa yametuhumiwa kule, kupitia Sheria ya Msajili wa haya mashirika wakaambiwa watoe maelezo. Baadhi yao wameshawasilisha maelezo na wengine wanayawasilisha. Sasa kwa sababu suala hili ni la kisheria, tukasubiri hayo maelezo yakamilike ili yaweze kuchanganuliwa na Bodi yetu ya Usajili ili wasilishwe kwa mujibu wa sheria. Kama kutakuwa na mtu ambae anaona ameonewa sheria inasema rufaa iende kwa Waziri. Mimi nitapokea, lakini sasa hivi mchakato unaendelea wa uwasilishaji hayo maelezo kujibu zile tuhuma ambazo wamehusishwa nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisemee kuhusu suala la hela hizi za Machinga ambazo bilioni 22.9 zilipaswa tupewe, lakini hatukuweza kupewa kwa wakati. Kupitia Wizara ya Fedha ambayo tumekuwa tukiwasiliana nayo ilikuwa inafanya uratibu wa Mifuko sio tu huu wa Machinga ili waweze kuweka mifumo vizuri ikiwepo Mfuko wa Maendeleo wa Vijana wa Wanawake, Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu na Mfuko huu wa Wamachinga. Sasa taarifa iliyoko ni kwamba hatua zimekamilika na hiyo taarifa itapelekwa kwenye kikao cha kazi cha *IMTC* kujadiliwa. Baada ya hapo, utolewaji wa hizo fedha utaanza, lakini kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha

atakapo kuwa analeta hotuba yake atakuwa ameweza kutolea mwongozo sambamba na tathmini hii iliyokuwa inafanywa na ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwenye suala lingine linalohusu malezi na makuzi, kwa nini tumeweza kufanya mikoa 10 tu, lakini pamoja na *WDF* huu mkopo tunaoutoa pale Wizarani tumekwenda mikoa minne tu. Hili suala la mikopo hii ya *WDF* tulipokuwa tumepewa kibali tuendelee kutoa hizi fedha, kulikuwa na maombi tayari yapo pale ofisini ya siku nyingi. Kwa hiyo, ilikuwa mtu aliyeanza kuleta ndio apewe. Tulipoweza kuwachambua wale wapewe ile mikopo ndio ikaangukia hiyo mikoa lakini kwa sababu marejesho yanakwenda vizuri, tumejipanga kuhakikisha kwamba taarifa zinakwenda mikoa yote na halmashauri zote. Hata kama ni milioni ishirini ishirini tunatenga waombaji wajue kuna hilo fungu. Watakaokidhi hivyo vigezo waweze kupatiwa ili hata kama tunampa mmoja mmoja lakini kila mtu aonje uzuri wa hiyo *WDF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Serikali ni kwamba, mikopo hii sasa yote tuipeleke benki, kwa sababu wengi wamekuwa katika mikopo kwa mfano ya asilimia 10 hawarejeshi na huu tukaona nao tuupeleke benki. Kwa hiyo utakapokuwa umeshafika pale benki, maana kwa sasa hivi tumesitisha kutoa, watapewa taarifa wote watachukua huko. Sisi tuta-*regulate* kuhakikisha majukwaa ya uwezeshaji wanawake kichumi yanaleta watu waliokidhi kupata hii mikopo kwenye benki za karibu na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa nini yamepewa mafunzo kwenye mikoa kumi tu. Ndio ilikuwa hivyo kwa sababu mikoa ile ilikuwa imeweza kutekeleza maelekezo mapema ya kwamba yaundwe hayo majukwaa. Kwa hiyo yale yaliyokuwa yameundwa tuliweza kuyapa mafunzo na sasa kwa sababu

Jukwaa la Kitaifa limeundwa jana yote hii inakwenda kuingia kwenye kupata mafunzo. Semina kubwa inaandaliwa, wataitwa waweze kupewa ili waweze kuweka mipango ya mikoa yao, kwamba wanataka kuwafikisha wale wanawake katika ngazi ipi ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wajane; wajane ni kundi maalum na nashukuru tunao hapa viongozi wa wajane, tumekuwa tukiwasiliana nao. Tatizo la wajane kweli limekuwa kubwa na mwishoni mwa mwezi huu wa Juni tutakuwa na siku ya wajane, Kitaifa tutaifanyia Mkoa wa Mbeya. Tutakusanyika nao pale na baada ya hapo wale viongozi na wenyewe watapewa mafunzo, kisha wataweka mpango ingawa wao ni sehemu ya wanawake, lakini tutayaangalia mahitaji yao kwa utofauti, kwa jicho la hali ile ya maisha yao yalivyo. Hasa masuala ya kisheria, wananyanyaswa sana, wananyang'anywa mali zao baada ya mwanamume kufariki wanapitia kwenye mateso makali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilishaagiza tupewe *list* yao wote ambao kesi hazisogei ili tuwaunganishe na watoa huduma za msaada wa kisheria. Kwa hiyo ole wao wale waliobeba mali za wajane, wajue kwamba moto unakuja, tumejipanga, baada ya Siku ya Wajane Mbeya, mkikutwa huko mjue kwamba sheria inakuhusu. Lazima tuwaheshimu kwa sababu ujane ni hali ya kutokujichagulia, bali kudra za Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utitiri wa mikopo umelalamikiwa sana. Nashukuru sasa kwamba jukwaa hili la uwezeshwaji wanawake kiuchumi limeanza. Wanawake wote wanaolia machozi sasa ya mikopo hii isioeleweka wanakwenda kupona. Wanakwenda kuziona fursa zingine tofauti kabisa za mikopo nafuu kupitia haya majukwaa. Sasa na hawa wanaoitwa mikopo ya makomandoo, sijui mikopo ya pasua kichwa, damu na nini, niwaombe huko mliko majukwaa yameanza mtaniona mpaka

kwenye ofisi zenu, mniambie mlisajiliwa na nani, mlipewa kibali na nani katika kuwapatia wanawake hawa mikopo ambayo pengine hata haikidhi hadhi ya utoaji mikopo. Waende wakajisajili kwenye utaratibu sahihi, wapewe miongozo ya utowaji mikopo. Kwa hiyo ukombozi wa wanawake umefika kupitia haya majukwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie eneo moja kuhusu vitambulisho vya Wamachinga. Vitambulisho vya Wamachinga sasa vinavyokuja ni vya kidijitali, vinaweza kuwezesha Mmachinga huyu kutoa fedha na kupokea fedha, lakini vimeunganisha na *NIDA* pamoja na *e-GA* pamoja na maeneo yote ambayo Machinga atakuwa anapita kwenye mzunguko wake wa kupata fedha. Akikionyesha kile kitambulisho wanamsoma, mifumo inasomana. Kwa hiyo ni kipindi cha mpito hiki Mwaka huu wa Fedha 2022/2023, kama nilivyosema tayari umekamilika, unafanyiwa majaribio, tutaanza na baadhi ya mikoa, kisha tutaenda nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala hili litakuwa limeweza kuwanyanyua Wamachinga kuaminika na kupewa mikopo na taasisi zingine zote, kwa kuwa vitambulisho vyao vitakuwa vimekidhi vigezo vyote vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *pension* ya wazee; niseme kwamba tumepokea wazee ni tunu ya Taifa, wazee tunawapenda na sisi wote tutazeeka. Tunafanya mapitio ya sera ya mwaka 2003 na mwaka jana tulifanikiwa kuunda Baraza la Taifa la Wazee ambapo tuliongea mambo mengi kuhusu mwelekeo wa kuboresha masuala ya wazee. Sera hii tumeshaiwasilisha, hatua nzuri itafanyiwa mapitio. Kwa hiyo humo ndani yake ndio tutakuja mpaka na Sheria ya Wazee, lakini tutakuja mpaka na masuala haya ya *pension* ya hawa wazee. Kwa hiyo utaratibu unaendelea na tutaendelea kuwasiliana nao kupitia Baraza la Wazee tunalofanya nalo kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haya machache kwa kibali chako niombe kuwasilisha mengine yote kupitia maandishi, tukizingatia hoja za Wabunge wote ambao wamezitoa hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo niliyoyaeleza, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kitabu cha pili, matumizi ya kawaida, kwenye vishikwambi vyetu ni ukurasa wa 546.

## Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*……..........…………...Sh. 4,418,492,200

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kifungu hiki kina mshahara wa Waziri, kuna majina hapa ya Wabunge ambao wanataka ufafanuzi wa jambo mahususi na la kisera, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka ufafanuzi kuhusu uwazi wa fedha za wamachinga ambazo mpaka sasa hazijulikani ziko wapi na hazijafanyanyiwa *allocation*. Mheshimiwa Waziri alivyosimama alisema kwamba zinafanyiwa utaratibu na Waziri wa Fedha na mifuko mingine yote ambayo ipo ikiwa ni ya vijana, mifuko ya wanawake na mifuko tofauti ndilo jibu ambalo alilitoa Mheshimiwa Waziri. Kwa bahati fedha hizi hatutaki kufanya *disbursement* tunataka zinafanyiwe *allocation* maana yake hata katika Fungu lake yeye hazionekani kwamba ameahidiwa sasa hicho ndicho ndicho ambacho nachotaka, sasa tukasema hakuna uwazi na kwa nini hakuna uwazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimekuja kwa mkopo wa *ECF* na fedha hizi zilikuja zipo siyo kama za kukusanya zipo zishakuja, isitoshe fedha hizi zina masharti, unazipata katika awamu ya pili baada ya kufanyiwa *review* na fedha hizi zilipelekwa katika *General Budget Support (GBS)*. Fedha zinavyopelekwa katika *General Budget Support* wafadhili walikuwa walishaanza kukataa kwa sababu zinafanyiwa matumizi mengine siyo yale yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na mimi hoja yangu ndiyo ipo hapo. Nataka Serikali itupe *commitment* kwamba hizi fedha

kwa ajili ya hawa wamachinga kwamba zitakwenda, kwa sababu hii Mifuko kufanyiwa tathmini hatutaki *disbursement,* zionyeshwe na zipelekwe, hicho ndicho tunachotaka na hilo halimhusu Waziri Gwajima linaihusu Serikali.

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga. Unasema linamuhusu nani? Ngoja Mheshimiwa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, linamhusu yeye Waziri Gwajima kwamba yeye amelibeba sasa, lakini sasa hilo jawabu ambalo alilolitoa silo. Sasa tunataka Serikali itupe *commitment* kwa sababu hili alivyoeleza haitoshelezi kutokana na uwazi ambao sisi tunautaka. Kwa sababu hizo fedha…

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana kengele imeshagonga.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa hii. Suala ambalo analiongelea Mheshimiwa Mbunge, Kaka yangu Mheshimiwa Omar King ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mara tu baada ya tathmini hiyo kukamilika tutatoa fedha hiyo na kuweka katika mfuko husika kwa wakati muafaka hivi karibuni. Ninaomba amuachie shilingi yake Mheshimiwa Waziri, fedha hiyo itawekwa kwa wakati muafaka. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Mimi katika mchango wangu nimezungumzia sana juu ya umuhimu wa malezi na makuzi kwa Watoto, hasa katika kipindi hiki ambapo mmomonyoko wa maadili umekuwa ni mkubwa sana. Kelele zimekuwa ni nyingi kwa makuzi ya watoto na wajibu wa wazazi, ningependa kujua je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na hali hii? Nisipopata majibu ya kuridhisha nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kufafanua hoja ya Mheshimiwa Aysharose Mattembe nzuri kabisa kama ifuatavyo ili asishike shilingi yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazingatia suala la malezi na makuzi tena linazingatiwa kwa nguvu kubwa inayoanzia na mamlaka yenyewe ya nchi kuingiza agenda ya malezi na makuzi katika mpango mzima wa jukwaa la kizazi chenye usawa la uwezeshaji wanawake kiuchumi. Sasa hivi tunavyo vituo ambavyo vimeanza kujengwa vya kijamii, tunavyo vituo mpaka vya watu binafsi vimejengwa na bado kuna fedha inakuja katika kufanikisha hii agenda ambayo Rais wetu ni kinara kujielekeza kwenye kuhakikisha hivi vituo vinakuwepo nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi siyo tu kwamba vitahudumia watoto wanaachwa pale wanaondoka wazazi, wazazi watakuwa sehemu ya kupata mafunzo kuanzia pale kwenye kile kituo na wana tengeneza vikundi vya umoja wa malezi, pamoja hata kukopeshwa fedha hizi za uwezeshaji wanawake kiuchumi ili wakienda majumbani kwao wapate

nafuu ya huo uchumi wanaouhangaikia pasipo kujali watoto wao. Kwa hiyo lina uzito mkubwa sana, naomba aachie tu shilingi yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Sina nia ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri ila ninataka tu nipate kujua namna ambavyo wamejipanga kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa mateja kwenye jamii yetu ni kwa sababu kuna watu wanauza madawa ya kulevya na Serikali inapinga vikali sana madawa ya kulevya. Kuwepo kwa mashoga kwenye jamii yetu ni kwa sababu kuna wanaume hawa ambao wao ni wanajiita mabasha kama sijakosea hilo neno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi wa Tatu tuliona kuna *clip* ambayo ilikuwa inazunguka ikimuhusu Askari wa Zanzibar akishiriki tendo lile na yule ambaye alikuwa ni mume wake. Swali langu liko hapa, Serikali mmejipangaje kupitia Wizara hii kuanza kuwatafuta wanaume hawa, kama wauza madawa ya kulevya, ambao kwenye jamii tulioko huko nje inasemekana wako baadhi ya watu kwenye ndoa wanaingiliwa kinyume na maumbile na wanaume hao hao, ziko baadhi ya jamii mabinti wanashiriki tendo la ndoa kinyume na maumbile ili watakapoolewa waolewe wakiwa ni wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuongezeka kwa matukio haya ni kwa sababu wako wanaume ambao wao wanasababisha jambo hili. Je, mnaonaje kama Wizara hii mkianza kuwatafuta kwanza wanaume hawa ili hata hawa

mashoga wasipate watu wa kuwaingilia? Mmejipangaje? Ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naona Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi amesimama. Eh! Haya naona mmesimama wengi, basi itifaki inataka Waziri. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Waheshimiwa Wabunge wamejadili sana jambo hili ambalo mada yake kubwa inahusu mmomonyoko wa maadili. Limetumika hili neno sana kwa sababu ya kulinda heshima, utu na ustaarabu wa Kitanzania katika kujadili mambo yanayohusu tabia za kibinadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni gumu hata mjadala wake ni mgumu, tunalifahamu kwa kiasi ambacho limejadiliwa na kiasi ambacho kimebakizwa katika kujadiliwa. Anachokiuliza Mheshimiwa Mbunge kwanza kabisa kinakatazwa kwa mujibu wa sheria. Katika Kanuni zetu kwenye *Penal Code* tumeeleza sheria iko wazi kabisa, kwamba kujamiiana kinyume na maumbile ni kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo *bottom line* kwamba sheria tunayo, limeelezwa ni kosa na kwamba anayekosea kwa mujibu wa adhabu zilizowekwa na makosa yaliyowekwa ataadhibiwa. Sasa kuuliza kwamba Serikali imejipanga vipi, inaweza ikawa ni jambo mahsusi mno ambayo kwa *nature* na kwa namna alivyolifafanua linaweza likaleta mkanganyiko mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe tu Serikali tumesikia, jamii imesikia. Jambo hili ni la kijamii ni la kibinadamu ni la kiutu ni la kiheshima. Maneno yaliyosemwa yametosha sana kuwa

yamesikika lakini tuendelee kila mmoja kwa namna anavyoweza kuhakikisha kwamba tunakomesha mmomonyoko huu wa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana aridhike Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua ambazo zitazingatia maoni haya yaliyotolewa humu Bungeni lakini yaliyotolewa na wadau mbalimbali kwa ustaarabu huko nje yote Serikali inayasikia na inaendelea kusikiliza. Kwa hivyo, atuachie tuone namna ya bora ya ku-*approach* mambo haya kistaarabu zaidi kuliko pengine kufanya oparesheni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Victor Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Sisi sote ni mashuhuda tunaona jinsi mmomonyoko wa maadili ulivyokithiri katika nchi yetu pia tunaona jinsi matendo ya ukatili yalivyo katika nchi yetu. Watoto wananyanyasika, wanabakwa lakini tunaona wazee wamekuwa wakinyanyaswa pia, tumeona jinsi ambavyo matendo haya yamekuwa yakiendelea pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia kuwa kuna changamoto ya msongo wa mawazo kwa wananchi walio wengi. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo limejitokeza. Hata Mheshimiwa Waziri wa Afya alivyokuwa akihitimisha alizungumza kwamba kumekuwa na changamoto ya watu kutokuwa na afya ya akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amezungumzia huduma za ustawi, Maafisa wa Ustawi wa Jamii na ameeleza katika Ibara ya 72 kama utaniruhusu ningesoma.

**MWENYEKITI:** Wewe enedelea tu ilishasomwa, wewe tengeneza hoja yako.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 61 amekiri kwamba kuna upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii kwa asilimia 95.3. Ukiangalia katika mitaa ambako ndiko watu wapo wengi kuna upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii 14,559 ambayo ni asilimia 99, na yupo kwenye Kata mmoja tu…..

**MWENYEKITI:** Kengele imegonga hoja yako ni ipi?

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba wanaajiri angalau zaidi ya asilimia 45. Nisiporidhika nitaomba kutoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri ambalo linaonyesha ameguswa sana na haya masuala na anahitaji kuona Serikali inafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna upungufu wa hawa watumishi kwa kiwango hicho, kama tunavyoona Serikali baada ya Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan kuunda hii Wizara, kwanza ina mwaka tu mmoja, ameshaajiri Maafisa Maendeleo 800 na tumewanunulia pikipiki 85 kutoka kwenye Wizara yangu tumekabidhi jana, Wizara zingine zimefanya hivyo kuwawezesha hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata hawa Maafisa Ustawi wa Jamii hoja zipo zilishakwenda kama ilivyoenda hii

wakaajiriwa. Mpango wa ajira unakuja. Tumeenda mbele tukajiongeza tukasema sasa mbona kuna wengine sokoni wapo wamesoma hawana kazi? Tukasema tutengeneze Sheria ya Taaluma ya Ustawi wa Jamii na Huduma za Ustawi wa Jamii. Wataalam wameshaanza kufanya ili tuanze kuwasajili wawe na msajili wapate leseni. Kutakuwa na *private services* vilevile za kada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutaona vituo vikifunguliwa vya kisaikolojia. Tunashirikiana na wataalamu wa saikolojia chini ya Rais wao Taasisi ya *Tanzania Psychology Association (TAPA)*. Kwa hiyo, kuna mambo yanakwenda mkitupitishia hizi fedha, mwaka wa pili mtaona mambo mazuri zaidi katika eneo hili tukishirikiana na Wizara ya Afya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayapo humu kwenye taarifa basi naomba.

**MWENYEKITI:** Wewe sema, unashika shilingi, unarejesha?

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja wenzangu waweze kuchangia.

**MWENYEKITI:** Wewe umesema unataka *commitment* na yeye ndiyo kaitoa hapa *commitment*. Endelea nakusikiliza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, hoja imeungwa na watu wa upande wako. Mtachangia watu watatu lakini muwe mmeielewa hoja yake kabla sijaanza kuwakalisha chini. Hoja yake inahusu ajira

ya Maafisa. Maana kule kwenye mmomonyoko alishatoka akaenda huku kwingine. Haya nimesema mtachangia watatu naona bado mmesimama wengi. Kwa hiyo, jichagueni wenyewe, watatu mmeshasimama. Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Commitment* anayoiomba Mheshimiwa Grace Tendega ni kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii na siyo Maafisa Maendeleo ya Jamii, hiyo moja. Pili, *commitment* ya Mheshimiwa Waziri inatakiwa ionekane kwenye mipango yake.

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja ngoja. Hizo ni kada mbili tofauti?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni kada mbili tofauti? Mheshimiwa Waziri hizi ni kada mbili tofauti?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kada mbili. Tuna Kada ya Maendeleo ya Jamii *(Community Development Officers)* na tuna kada ya Maafisa Ustawi wa Jamii. Nilichosema…

**MWENYEKITI:** Uliosema wewe wanaajiriwa ni wapi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, walioajiriwa hawa 800 ni wa Maendeleo lakini hawa wa Ustawi wa Jamii nao tulishapeleka maombi nikasema Wizara ina mwaka mmoja, kupanga ni kuchagua, tumeanza wa Maafisa Maendeleo ya Jamii hata hao hao Maafisa Ustawi wa Jamii nao wataajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda mbele kujiongeza kwamba ajira hazijawahi kutosha Serikalini kwenye sekta yoyote, tufanyaje? Wako wastaafu wanataka kufungua huduma binafsi za kutoa huduma za kisaikolojia tuwatengenezee sheria ili nao waweze kufanya huduma hizi tuongezee wigo wa wataalam nchini na hayo nimeyaandika kwenye hotuba yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia. Hoja ya Mheshimiwa Tendega tunahitaji Maafisa Ustawi wa Jamii. Ukiangalia *instrument* ya Mheshimiwa Waziri, *instrument* yake, *key function* ya Wizara ni hii ipo kwenye watu wa Ustawi wa Jamii. Hawa watu ndiyo wanatoa ushauri nasihi, hawa watu ndiyo wanaohusika na kuwafanyia *counselling* watoto, hawa watu ndiyo wanakaa kwenye haya madawati ya kijinsia. Watu wa Ustawi wa Jamii ndiyo kazi kubwa ya Wizara hii tunayoijadili leo, hiyo moja.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana, kengele imegonga. Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Tendega ya kutaka Serikali iweke *commitment* walau ya kuajiri asilimia 45 ya Afisa Ustawi wa Jamii. *As we stand now* ni asilimia 7.5 tu. Ukiangalia hapo wametoa kipaumbele mwaka wa fedha 2022/2023 wametueleza wanaenda kuajiri Afisa Maendeleo ya Jamii 800, wakati ukiangalia kwa hotuba yake mwenyewe amekiri kwamba upungufu kwenye upande wa Afisa Maendeleo ya Jamii ni asilimia 43 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wana upungufu wa asilimia 43 Afisa Maendeleo ya Jamii *yet* unaenda tena kuongeza ajira 800 kwenye upungufu mdogo ukilinganisha na Ustawi wa Jamii. Kwa hiyo, hii inaonyesha kabisa kwamba Serikali licha ya kwamba hii Ustawi wa Jamii ndiyo *the key role* kwenye Wizara hii, hawajaipa uzito, *that's what we are saying.* Mimi nimepitia hotuba yake yote hamna sehemu ameweka mpango, mwaka wa fedha 2023/2024 anaajri Afisa Maendeleo ya Jamii, ndiyo maana tunasema watoe *commitment* ya kuajiri Maafisa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagonga, Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kutoa hii nafasi ili tujadili. Kupanga ni kuchagua, leo tunaona kwamba tuanze na Maafisa Maendeleo ya Jamii lakini tulipaswa kuanza na Maafisa Ustawi wa Jamii. Ukiangalia msingi wa jamii hata neno lenyewe lina *connotate* ustawi wa jamii, hapa ndiyo tunaangalia wanaowasikiliza watoto kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna *incidence* za watoto kubakwa kuanzia kwenye familia, kuja kwenye vituo wanakolelea lakini siyo hiyo tu, leo kuna changamoto hata ya ndoa zinazovunjika, watoto wanaobaki pale wanaenda kueleza changamoto zao wapi? Narudia pale, kama kupanga ni kuchagua tulipaswa kuanza na Maafisa Ustawi wa Jamii hata kabla ya Maafisa Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana hili suala mliangalie kwa upana wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia upande wa Serikali hoja na kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, naomba nichukue nafasi hii kuwajulisha kwanza mtoa hoja lakini pia na wote waliochangia na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imeliona jambo hili na kwa mwaka wa fedha unaokuja tumepanga kuanza na 350. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tulionao ni wachache siyo kwamba hawapo kabisa ni wachache, Wizara inajitahidi kuja na mpango wa kuzibaziba kwa kuja na mpango wa kuchukua hata waliostaafu lakini nasi tumeanza na watumishi 350 kwa kibali kitakachotolewa na Mheshimiwa Rais kwa mwaka huu na tumeshatenga kwenye bajeti. Kwa hiyo, kadri tutakavyokwenda na mahitaji yanavyoonekana na uhitaji huu ambao unalazimishwa na *situation* tuliyonayo sasa ya masuala ya mmomonyoko wa maadili, nadhani kwa mwaka unaokuja tutakubaliana hapa tutaongeza nafasi zaidi hizo kwa sababu tujue tuna mahitaji mengi, tunao upungufu wa maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwepo jana Wizara ya Elimu hapa mlizungumza masuala ya upungufu. Kwa hiyo, upungufu ni mkubwa lakini tutaanza na hao 350. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *logic* peke yake, huku kuna upungufu wa watumishi 21,000 na 82,000 lakini huku kuna upungufu wa watumishi 996. Sasa ukiangalia tu hapo unaona jinsi ambavyo wamepeleka kule 800 huku wakapeleka hata wakiongeza hao 300 bado asilimia ni ndogo, angalau basi wakiongeza wakaongezeka

hata asilimia zikafika hata 30 inaweza ikasaidia kupunguza adha ambayo ipo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe tu Mheshimiwa Waziri kwa kweli uwe na *commitment* kwa Maafisa Ustawi wa Jamii. Nitakurudishia shilingi yako lakini uhakikishe kwamba wanakuwepo katika jamii ili waweze kusaidia wananchi huko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tukumbushane tu kwamba sisi kwenye jamii tupo. Huyo Afisa mmoja tu kwenye Kata kama ndiyo tunategemea ataleta muujiza wa haya maadili kwenye jamii sina hakika sana, tunataka kulitazama kwa sura hiyo lakini yote ni muhimu ila pia ni muhimu zaidi. Kila mtu afanye kwa sehemu yake maana huyo Afisa sasa tutataka kila kitu afanye yeye hataweza, maana nasi tunahusika moja kwa moja.

Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kwenye mafungu. Katibu.

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.................................Sh. 4,418,492,200
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 815,564,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*................Sh. 1,139,894,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*............................Sh. 615,854,000
Kifungu 1005 - *Government Communication Unit*....................................................Sh. 352,480,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.....Sh. 567,558,000
Kifungu 1007 - *Information, Communication and Technology*...............................Sh. 450,692,000
Kifungu 1008 - *Legal Service Unit*……………………Sh. 413,950,600
Kifungu 2001 - *Community Development Institutes*.......................................Sh. 14,218,400,800
Kifungu 2002 - *Community Development*...........Sh. 1,229,666,000

Kifungu 3001 - *Gender Development*..................Sh. 1,797,195,650
Kifungu 3002 - *Children Development*……………Sh. 1,051,706,000
Kifungu 3003 - ……………………………………………Sh. 1,743,572,000
Kifungu 4001 - *Non-Governmental Organizations*................................Sh. 2,991,277,350
Kifungu 5001 - *Social Welfare Division*…………..Sh. 11,858,660,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*……………Sh. 400,000,000
Kifungu 2001 - *Community Development Institutes*.......................................……..Sh. 3,100,000,000
Kifungu 2002 - *Community Development*................................Sh. 0
Kifungu 3001 - *Gender Development*...................Sh. 5,257,993,831
Kifungu 3002 - *Children Development*……………Sh. 1,253,236,169
Kifungu 3003 -…………………….……………………Sh. 18,500,000,000
Kifungu 5001 *Social Welfare Division*………………Sh. 2,047,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3) (a) na (3),(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono na sasa nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono na kwa hivyo, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yamepitishwa rasmi na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa bajeti yenu na Bunge, tunawatakia kila la kheri katika utendaji kazi katika kutekeleza yale ambayo mmeliahidi Bunge kupitia hotuba yenu pia yale ambayo mmewaahidi Waheshimiwa Wabunge wakati mkihitimisha hoja zenu. Tunaamini yote mmeyasikia na hata yale ambayo hamjajibu mtajibu kwa maandishi, mtayafanyia kazi yale ambayo yanapaswa kulisaidia Taifa letu kusonga mbele.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie pia fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri wanayoifanya, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote na Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia na wale ambao hamjapata nafasi bado ofisi iko wazi, kama mlivyosikia simu ya Mheshimiwa Waziri iko wazi mnaweza kuendelea kutoa mawazo yenu ili Taifa letu liweze kusonga mbele katika kila eneo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa hapa kuhusu ile Miswada ambayo tuliisoma asubuhi kwa mara ya kwanza na niliwaeleza utaratibu namna utakavyokuwa. Nitumie sasa fursa hii kuelekeza Miswada hii katika Kamati zifuatazo:-

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa Mwaka 2023 *(The Laws Revision Miscellaneous Amendment Bill, 2023)* itaenda Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023 pia utaenda Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria na Muswada

wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Services Amendment Bill, 2023)* pia utaenda Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 8.28 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 19 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*